

# Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TANO

Kikao cha Nne – Tarehe 11 Novemba, 2011

(Mkutano Ulianaza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. George B. Simbachawene) Alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Na. 41

**Serikali Kuwatengea Maeneo Wafanyabiashara Ndogondogo**

**MHE. JOSEPHINE T. CHAGULLA** aliuliza:-

Biashara ndogondogo kama Wamachinga na Mama lishe, huwawezesha wananchi kujajiri na kujipatia vipato ili kukabiliana na ugumu wa maisha:-

Je, kwa nini Serikali isiwajengjee wafanyabiashara hao wadogowadogo maeneo ya kufanya biashara ili kuondoa kero na usumbufu wanaoupata?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Josephine Thabitia Chagulla, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ndogondogo ni biashara zinazoendeshwa katika mfumo wa wa sekta isiyo rasmi (*Informal Sector*) zikiwa na mitaji midogo. Serikali inatambua kuwepo kwa wafanyabiashara ndogondogo katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu kwa maana ya Vijiji na Mijini. Kundi hili la Watanzania linachangia katika ukuaji wa ajira za kujajiri, kuongeza kipato cha mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikitenga maeneo kwa ajili ya wafanyabiashara ndogondogo likiwemo Jiji la Dar-es-Salaam ambapo katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilala, maeneo yaliyotengwa ni Mchikichini, Mtaa wa Kilwa, Kibasila, Kigogo Sambusa, Mtaa wa Lumumba, Soko la Kisutu, Ilala na Buguruni, masoko mapya ya Kitunda, Tabata, Segerea na Ukonga.

Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, maeneo ya TAZARA, Tandika, Mbagala Rangi Tatu, Soko la Temeke Stereo na masoko mengine na Manispaa ya Kinondoni maeneo ya Kapera, Babati, Manzese, Msufini, Mikocheni, Sinza I na II, Mabibo, Mburahati, Urafiki, Tegeta, Makumbusho na Kawe. Zoezi hili ni endelevu na linasisitiza Mamlaka za Serikali za Mitaa kuendelea kutenga maeneo na kutoa elimu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika kuititia Mpango wa Urasimishaji wa Rasilimali na Biashara za Wanyonge, Tanzania inawezesha Watanzania kwa kuwapa mafunzo kwa lengo la kuwajenglea uwezo wamiliki wa biashara ili waweze kutambuliwa rasmi katika mfumo wa Sekta rasmi na kukuza mitaji yao na kupanua wigo wa shughuli zao.

Kupitia Mpango huu wafanyabiashara wapatao 1,030 wamepatiwa mafunzo katika Jiji la Dar-es-Salaam kuhusu usajili wa biashara na manufaa yake, utunzaji wa kumbukumbu na hesabu za biashara, usimamizi wa biashara na utumiaji wa huduma za kibenki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia fursa hii kuziagiza Mamlaka zote za Serikali za Mitaa kutekeleza agizo la Serikali la kutenga maeneo kwa ajili ya wafanyabiashara ili kuwaondolea adha na kuongeza tija ya biashara hizo. Aidha, Halmashauri za Wilaya, Manispaa na Miji, ziweke kipaumbele cha kujenga masoko ya biashara ndogo ambayo yatakodishwa kwa wafanyabiashara hao.

**MHE. JOSEPHINE T. CHAGULLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri kabisa ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kumekuwa na ongezeko kubwa sana la wafanyabiashara ndogondogo na mama lishe katika Mikoa yenyе maeneo ya machimbo, kama Mkoa wa Geita. Je, Serikali haioni kuna haja ya kuwapa mikopo wafanyabiashara hawa ili angalao waweze kuinua hali zao za maisha?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkoo, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Josephine Thabitah Chagulla, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili wala hatuna ubishi nalo. Suala hili la kuwasaidia wafanyabiashara wadogowadogo, ukiangalia llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, inawazungumzia kwa kina sana na ndio maana hapa tumetoa maelekezo.

Lakini utaratibu tunaoutumia katika Halmashauri tulikuwa tunashauri kwamba, hawa wafanyabiashara, wawe wanajiunga na *SACCOS* ili iwe ni rahisi kuweza kuwakopesha kama inavyoelekezwa hapa. Wizara ya Maendeleo ya Jamii nayo imekuwa inatoa mikopo kwa ajili ya kuwasaidia hawa akinamama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninataka nimpongeze sana Mheshimiwa Tabitha, kwa mpango huu anaokuja nao na awe na hakika kwamba tutamuunga mkono huko Geita, kwa ajili ya kuwasaidia hawa akinamama ambao siku hizi tunawaita mama lishe na wala sio mama ntilie.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kuniona. Katika majibu yake ya msingi kuna maeneo yametajwa ambayo yako ndani ya Jimbo la Ubungo, maeneo ya masoko ya Manzese, Sinza, Mabibo pamoja na Urafiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wakati wa uchaguzi Mkoo wa Mwaka 2010, Rais Kikwete alipohutubia Dar-es-Salaam aliahidi kwamba, katika kipindi hiki Serikali itajenga *Machinga Complex* kwa kila Manispaa za Dar-es-Salaam.

Sasa kwenye haya maeneo yote yalijotajwa ya Manispaa ya Kinondoni, hakuna eneo ambalo lina ukubwa wa kuweza kujenga *Machinga Complex*. Je, Ofisi ya Waziri Mkoo, iko tayari kwa kushirikiana na Wizara nydingine za Serikali, kwa kuwa eneo la Ubungo, kuna eneo pale la *Ubungo Industrial Area*, ambalo lina maeneo makubwa ambayo mengi yametelekezwa kwa sababu ya matatizo ya ubinafsishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali iko tayari kuchukua eneo mojawapo ili kuweza kupata eneo pana zaidi la wafanyabiashara pale Ubungo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkoo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mnyika, Mbunge wa Ubungo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa anachosema kuhusu Mheshimiwa Rais, ni kweli. Hakuagiza tu kwa ajili ya Manispaa hizi za Temeke, llala pamoja na Kinondoni, ameagiza kwa nchi

nzima, yaani na Geita na wapi, wote. Kwamba, tuwe na utaratibu ambao tutakuwa tunawasaidia vijana wetu hawa wanaofanya biashara hizi tunazozungumzia ili wake mahali, badala ya kuwa wanatembea na soksi mkononi na sahani na kanda na nini, tuwe na utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tunachozungumza hapa ni *the political economy of capitalism* na *the political economy of socialism*. *The relations of production* ambazo zinatengenezwa pale, ndicho kinachozungumzwa hapa; mahusiano ya uzalishaji mali, ndicho kinachosemwa hapa. Kwa hiyo, sasa sisi kwa muelekeo tunaokwendanao sasa hivi hapa, tuna mwelekeo huo unaokwenda unaangalia pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Mnyika, amekuja na hili wazo analolizungumza hapa. Mimi najua yeye ni Mjumbe, anaingia katika Jiji na kule kwenye Jiji, Jiji ndilo linalosimamia hizi biashara zote. Hata hii *Machinga Complex* ambayo tumeizungumzia hapa iko chini ya Jiji la Dar es Salaam.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, sogeza *Mic.*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii tunayoizungumza hapa sasa hivi, iko chini ya Jiji. Kwa hiyo, hili eneo analosema hili la *Ubungo Industrial* hili, mimi siwezi kulijibia hapa kwa sababu siwezi kujua kwamba wamepanga nini. Kinachotakiwa sasa ni kuchukua wazo hili. Mimi nitamsaidia Mheshimiwa Mbunge, kuzungumza hapa na akina Kingobi pamoja na Meya, ili tuone kama hilo eneo nalolisema hapa linaweza likatumika, Kwa sababu nikijibu hapa unaweza ukakuta kwamba kule kuna mipango mingine. Kwa hiyo mimi ninakaribisha mawazo yako ni mawazo mazuri. Tutashirikiananayo ili kuhakikisha kwamba tunawasaidia katika jambo hili.

**MHE. ABAS Z. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Mheshimiwa Naibu Waziri, kama swali linavyoijeleza ni kweli kwamba majukumu ya Machinga ni ya Jiji. Lakini kutokana na uwezo wa Jiji, Jiji linategemea Serikali iwape uwezo, kwa hiyo, bado suala hili liko chini ya Serikali Kuu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, pamoja na hilo lakini ni lini wale Machinga wa Mchikichini watahamia kwenye jengo la llala?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mtemvu na swali lako Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwa heshima yako, hili la wale wafanyabiashara wa Mchikichini pale, najua ndicho kinachosemwa. Kwa hiyo, basi wale walioko katika *Machinga Complex* hawaruhusiwi kuendesha biashara pale...

**MBUNGE FULANI:** Hatusikii.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani watanisikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili tatizo la Mchikichini linalosemwa hapa, hili ambalo umelizungumza hapa, tatizo hilo ni kwamba wanachozungumza ni kwamba wafanye mpango wale walioko katika lile soko la mchikichini waondoke pale ili sasa warudi kwenye hii *Machinga Complex* wafanye biashara pale. (*Makofi*)

Sasa suala hili, lilinahusu Manispaa ya llala; wamezungumza mle na wamevutana pale, hawajaelewana. Mpaka sasa hivi tunavyozungumza pale hawajaondoka na walio wengi pale ni 30% tu ndio ambao wameingia katika hii *Machinga Complex* ambayo tunaizungumzia hapa. Nimecheki nao, hata asubuhi hii nimezungumza nao; tumesema hivi, waendeleze mjadala ule, wazungumze namna ya kuliondoa lile soko pale ili sasa liweze kuruhusu hili jingine. Mamlaka hizi za

Serikali za Mitaa zina madaraka kamili, kwa hiyo, zenyewe ndizo zinazoamua kufanya hivyo kama unavyozungumza hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la pili analolisema Mheshimiwa Mtemvu, ni kweli hata hii *Machinga Complex* ambayo tumeijenga pale, Serikali Kuu ilichofanya ni ku-*facilitate*, kusaidia kwa maana ya kupata mkopo kutoka *NSSF*, ndicho kilichofanyika pale. Kwa hiyo, sasa anachosema ni kweli na sisi tunajua kabisa kwamba, Serikali Kuu tunatakiwa kuona kuona kwamba, tunasaidia kwa maana ya kuingilia kati katika jambo hili ili tuweze kusaidia yale maendeleo. Na kama anavyosema ni kweli, uwezo wao ni mdogo ni lazima kusaidiwa pale. Sasa kusaidia sio maana yake moja kwa moja *directly* unapeleka hela pale, lakini tunaweza tukaweka mazingira ambayo yatasaidia kama walivyopata mkopo kutoka *NSSF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Mtemvu, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, mimi ninaomba tukae wote kwa pamoja tufikirie namna ya kupanua wigo ili tuweze kupata hela zaidi kwa ajilli ya kufungua masoko haya. (*Makofi*)

Na. 42

### **Serikali Kuwezesha Wanawake**

**MHE. DAVID E. SILINDE** aliuliza:-

Serikali inakiri wazi kuwa kumwezesha mwanamke ni sawa na kuiwezesha jamii:-

(a) Je, mpaka sasa ni wanawake wangapi wamewezeshwa kupatiwa mikopo ili kuwainua kiuchumi na kielimu?

(b) Je, ni kada zipi za wanawake ndizo zenyeye fursa zaidi kupata mikopo yenye lengo la kuwainua kiuchumi?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, David Ernest Silinde, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Silinde kuwa ukimwezesha mwanamke ni sawa na kuiwezesha jamii. Kwa kuzingatia ukweli huu Serikali imekuwa mstari wa mbele katika kuwawezesha wanawake, kisiasa, kiuchumi, kielimu na kijamii.

Hivyo, naomba nitumie fursa hii kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa, kuitia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, takribani wanawake 300,000 wameweza kupatiwa mikopo tangu Mfuko huo uanzishwe mwaka 1993.

Aidha, Benki ya Wanawake Tanzania, imetoa mikopo kwa wanawake 3,862 tangu ianzishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika wanawake 26,261 wamepatiwa mikopo kuitia Mfuko wa Uwezesaji Wananchi Kiuchumi na Kuongeza Ajira, maarufu kama Mabilioni ya JK hadi kufikia Aprili 2010. Mfuko wa uwezesaji (*Mwananchi Fund*), umetoa mikopo kwa wanawake 1,341 hadi kufikia Aprili 2010 na Mfuko wa *SELF* umewakopesha wanawake 47,430 katika kipindi cha 2000 – 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa elimu Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kuwainua wanawake kielimu. Hatua hizo ni pamoja na kuanzisha mifuko ya kuwasomesha katika ngazi mbalimbali za elimu, upendeleo maalum wa mikopo kwa wanaoingia vyuo vikuu, Mpango maalum wa kuwawezesha kuijunga na masomo ya sayansi chuo kikuu (*Pre-entry Qualification*), na kadhalikia.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wote wa Kitanzania wanastahili kupata mikopo kutoka taasisi na mifuko mbalimbali ya kifedha. Hata hivyo msisitizo umewekwa kwa wanawake wajasiriamali wadogo wadogo ambao hukosa dhamana ya kupata mikopo kwenye Benki za Biashara kutopteka na kutomiliki mali ye yote kama vile ardhi, nyumba na mashamba.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipouliza swali la pili, ni Kada zipi zinapata fursa. Kada zipi za wanawake ndizo zenye fursa zaidi ya kupata mikopo yenye lengo la kuwawezesha kiuchumi. Nilikuwa hasa ninalenga wanawake wa vijijini.

Mheshimiwa Spika, takwimu zilivyoonesha, ukirudi katika maeneo kama ya Jimbo la Mbozi Magharibi na maeneo mengine yanayofanana na hayo, wanawake wa vijijini asilimia kubwa hawafikiwi na hii mikopo.

Je, Serikali sasa ina mkakati gani wa kuwasaidia wanawake wa vijijini ambao fursa hizi za mikopo haziwafiki? (*Makofii*)

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali sasa inaweza ikakubaliana na mimi kuanzisha benki za wanawake vijijini zenye lengo moja la kuwasaidia wanawake vijijini ili kuweza kuwainua kiuchumi?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ningependa kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, Silinde, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza ni vipi wanawake wa vijijini wanaweza kufikiwa na hizi *services* za mikopo; tuna Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake na unatakiwa uwepo katika Halmashauri zote Tanzania.

Mheshimiwa Silinde, kwa taarifa yako Mfuko huu, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, inatoa hela kuanzia 4,000,000/=, 8,000,000/= mpaka 16,000,000/= na Halmashauri, kwa mujibu wa agizo la Waziri Mkuu, inatakiwa itoe 10% ya mapato yao.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge ni kwamba, kwa kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake, lengo letu ni kuwafikia wanawake wa vijijini. Na wale wanawake wa mijini wakubwa, tunategemea watapata mikopo katika mabenki ya kibishara hata benki ya wanawake.

Naomba tu nikupe changamoto uihamasithe Halmashauri yako ya Wilaya, ihakikishe kwamba inaboresha Mfuko wa Maendeleo ya wanawake ili kuhakikisha wanawake wote wa vijijini wanapata fursa. Lakini pia niongeze tu kwamba, tuna mifuko mbalimbali ambayo tunashirikiananayo kuhakikisha kwamba, wanawake vijijini wanafikiwa.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Serikali ianzishe Benki ya Wanawake vijijini. Ni wazo zuri, lakini tayari tuna Benki ya Wanawake Tanzania. Lengo letu ni kuhakikisha kwamba mtaji unakua ili kuweza kuhakikisha matawi yanaanzishwa katika mikoa yote. Tukiwa na matawi mikoani, maana yake tutafika katika *level/za Wilaya*, tutafika katika *level/za vijijini*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tayari niongeze tu kwamba, kwa kupitia Benki ya Wanawake, tunafanya kazi na vikoba, *SACCOS*, kuhakikisha kwamba tunawafikia wanawake wa vijijini.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri sana ambayo Naibu Waziri amefafanua hapa, nina swali moja tu dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wanaozungumziwa hapa, tunakubaliana wote hapa na tunaona vijiji ni kwamba wanajitahidi sana kuanzisha miradi ya kiuchumi, ambayo kwa kiasi kikubwa sana haina mitaji.

Ni kweli kabisa wanachotegemea ni mikopo wala si misaada bali ni mikopo, zipo taasisi nyingi sana za kifedha hapa nchini. Taasisi kama *FICA*, taasisi kama *PRIDE*, taasiai kama *FAIDA* na nyinginezo. Hizi zote tukubaliane kwamba nyingi zimejikita mijini, nyingi. (*Makof*)

Je, Serikali inafanya jitihada gani kuwahamasisha na kuwaamsha hawa wenye taasisi hizi waende huko vijiji ni wakawasaidie hawa wanawake ambao wanajitahidi kufa na kupona kuondokana na umaskini wao?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge Cynthia Hilda Ngoye, kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na Mheshimiwa Ngoye kwamba ni kweli taasisi nyingi kama *FICA*, *PRIDE*, *BANCOP* ziko mijini. Lakini hii ni changamoto na kila siku katika vikao vyetu na taasisi hizi tunajaribu kuwasisitiza siyo tunajaribu tunawahamasisha wafike vijiji. Lakini kutokana na kwamba hizi ni taasisi zisizo za kiserikali zinafanya biashara hatuna ile kwamba tukasema ni lazima tuwalazimishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado sisi tunaona mkombozi wa wanawake wa vijiji ni Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake na Benki ya Wanawake Tanzania ndiyo lengo letu kwa sababu huu ni mfuko wa Serikali na Benki ya Serikali tutahakikisha kwamba wanafunga madirisha madogo vijiji lakini Mheshimiwa Ngoye nikusitisizie tu kwamba tutaendelea kuwahamisha wafike vijiji na tunategemea katika ile mabilioni ya JK two kuna pesa ambazo tutazitoa kwa haya mashirika yanayotoa mikopo vijiji ili yaweze kuwafikia wananchi wengi zaidi. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anne Killango Malecela kwa kifupi sana.

**MHE. ANNE K. MALECELÀ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mwenyezi Mungu alipokuwa anaumba ulimwengu alianza kumwumba mwanaume kwanza na baadaye ndiyo akamwumba mwanamke. Na Mwenyezi Mungu alifanya hivyo kwa sababu mwanaume ni mwepesi kumwumba kuliko kumwumba mwanamke. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia ndani ya jamii duniani hasa mimi nazungumzia Tanzania, mtendaji mkuu anayefanya nchi iwepo ni mwanamke. (*Makof*)

Mwanamke ndiyo anayejenga nchi hii, naomba kurudia, je, Serikali haioni kuna umuhimu wa kuwa na kitu kikubwa cha kuondoa umaskini wa mwanamke ili wanawake waweze kujengwa nchi yao kwa urahisi zaidi? Naomba majibu mazuri.

Hii kali maana sasa kumwumba mwanamke ni vigumu sana kuliko mwanaume? (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri nimekuona.

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu swali lake la nyongeza Mheshimiwa Anne Kilanga Malecela, kama ifuatavyo:-

Kwanza nakubaliana naye kabisa kwamba, mwanamke ni muhimu sana katika jamii na kwamba ndiye yeye aliyeshika usukani katika maendeleo ya nchi. (*Makof*)

Aidha, ukimwendeleza mwanamke umeendeleza jamii yote. (*Makof*)

Kwa hiyo, ndiyo maana Serikali hata imekuwa na Wizara ambayo inashughulika na masuala ya jinsia lakini ina kitengo kinaitwa kitengo cha wanawake. Kazi yetu kubwa ni kuangalia wanawake wanawezeshwa kwa kiasi kikubwa iwezekanavyo na katika masuala wanawezeshwa

kwa kiasi kikubwa iwezekanavyo na katika masuala yote tumejitahidi kwamba masuala ya *gender* yanaingizwa katika Wizara zote katika masuala yote ambayo tunazungumza lazima masuala ya wanawake yaweke mbele. Kwa sasa KILIMO KWANZA pia tumesema wanawake wapewe kipaumbele katika kukopeshwa matrektu na vitu vingine. Hiyo yote ni katika kumwendeleza mwanamke. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante tunaendelea na swalii linalofuatia linaenda Wizara ya Kazi na Ajira na litaulizwa na Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Riziki Omar Juma.

Na. 43

### Ajira kwa Wanawake

**MHE. RIZIKI O. JUMA** aliuliza:-

Utafiti uliofanyika mwaka 2006 unaonesha kuwa katika maeneo ya mijini idadi ya wanawake wasio na ajira ni kubwa kuliko wanaume:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwanyanya wanawake katika ajira ili waweze kuboresha maisha yao ikizingatiwa kuwa wanawake ndio watanza familia?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kazi na Ajira, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, utafiti wa nguvu kazi (*ILFS*) wa mwaka 2006 unaonesha kuwa ukosefu wa ajira kwa wanawake ni mkubwa ukilinganisha na wanaume na pia ni mkubwa katika maeneo ya mijini ukilinganisha na vijijini. Hata hivyo ni vyema kutambua kwamba, utafiti huo wa mwaka 2006 (kama zilivyokuwa tafiti za nyuma) ulizingatia zaidi ajira rasmi na hasa za kuajiriwa.

Lakini tunatambua kwamba, wanawake wengi wanajajiri katika sekta isiyo rasmi kama ajira za nyumbani (*household enterprise*) na ujasiriamali, hasa katika uzalishaji, biashara, ushonaji, urembo na sanaa. Ikiwa tafiti zijazo zitazingatia ajira hizi zote zisizo rasmi, huenda takwimu za ajira kwa wanawake (kwa maana ya kuajiriwa na kujajiri) zikaonesha hali tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudii hizi binafsi za wanawake kujajiri, Serikali imekuwa ikitekeleza mikakati kadhaa ili kuwanyanya wanawake katika ajira, kwa mfano:-

(i) Maboresho katika mfumo wa elimu na mafunzo ili kuwezesha idadi kubwa ya watoto wa kike kupata elimu na ujuzi kama njia pekee ya kuwawezesha kuhimili ushindani katika soko la ajira.

(ii) Kutunga Sera na Sheria ikiwemo Sheria ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2002 na marekebisho yake ya mwaka 2007 ambayo imeainisha kuwa iwapo sifa za waombaji wanawake na wanaume zitalingana, kipaumbele cha ajira kitatolewa kwa mwanamke.

(iii) Kuendesha Programu mbalimbali za kisekta zinazotoa mafunzo ya ujasiriamali, stadi za kazi na uwezehaji kiuchumi ya wanawake na ushiriki wao kwenye maonesho kama vile nguvu Kazi/Jua Kali ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(iv) Kuwahamasisha wanawake kujungu katika vyama vya akiba na mikopo (*SACCOS*) na *VICOBA* ili kuwezesha kunufaika na huduma mbalimbali za za kibiashara ikiwa ni pamoja na mafunzo na mikopo. Aidha, kuanzhishwa kwa Benki ya Wanawake Tanzania (*TWB*), Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake (*WDF*) na Mfuko wa Uwezeshaji (*JK Fund*), kumepanua wigo wa wanawake kupata mitaji yenyewe masharti nafuu. (*Makofi*)

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa moja katika ajira zisizo rasmi ambazo wanategemea sana wanawake ni ajira za majumbani. Lakini wanawake hawa ambao wanaajiriwa majumbani wanakumbana na uzalilishaji mkubwa na unyanyasaji na wengine kupelekea hata kunyimwa chakula au mapumziko yaani kwa maana ya likizo au hata mishahara yao haitambuliki.

(i) Waziri au Serikali inasemaje kuhusiana na hili na lini itaunda chombo rasmi cha kuwashughulikia wanawake hawa kujua ni wangapi wako wapi na wameajiriwa namna gani na mishahara yao na mafao yakoje, ili waepukane na unyanyasaji huu mkubwa ambao unawakuta? (*Makof*)

(ii) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali ina juhudhi kubwa sana za kuhakikisha kwamba wanawake wanapata ajira na wanaondokana na usumbufu huu ambao unawapata na hasa kwa vile wana juhudhi kubwa za kujajiri wenye.

Lakini juhudhi hizo inaonekana zinakizana na Serikali Kuu pamoja na Serikali za Mitaa. Kwani hivi karibuni nimeshuhudia mwanamke akinyang'anya biashara yake na askari wa Jiji ugomvi anamkanyagia kanyagia na kumdhaliilisha jambo ambalo linapeleka kama mkopo ule ameukopa Mheshimiwa Mwenyekiti.

Je, atakwenda kulipa mkopo ule ambao tayari anao, ana watoto nyumbani wanasubiri kupata chakula na kulingana na fedha ile aliyokopa?

Je, Serikali inasemaji kutokana na sakata hil la kuharibiwa mali na unyanyasaji? (*Makof*)

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kazi na Ajira napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Riziki Omar Juma, kama ifuatavyo:-

Kuhusua suala la wafanyakazi wa majumbani nataka niseme hapa kwamba wafanyakazi hao au kazi hizi za majumbani ni kazi kama kazi nyingine. Nataka nisisitize kwamba watu watambue kwamba hizi ni kazi kama kazi nyingine na zinatakiwa ziwe na mikataba ya kazi. Kwa hiyo kinachofanyika kutokuwa na mikataba ni makosa. Lakini niseme kwamba kuhusu chombo kwanza hawa wanacho chama chao ambacho kinatetea haki zao cha wafanyakazi.

Lakini vilevile kuhusu mishahara, sasa hivi tumeunda tayari Bodi za vima vyta chini vya mshahara vya sekta mbalimbali. Sekta hii ya wafanyakazi wa majumbani tayari na yenye ina Bodii, hivi karibuni Bodii hii baada ya kufanya tafiti zitaleta kima cha chini kinachotakiwa kulipwa kwa ajili ya wafanyakazi hao na baada ya hapo sisi kama Wizara ya Kazi, tutahakikisha kwamba sheria hiyo inatekelezwa kwa maana waajiri wote wanawalipa hawa wafanyakazi wa majumbani kama inavyostahili.

Kuhusu wanawake kunyanyaswa wanapofanya shughuli zao, lazima niseme tu hapa kwamba sisi tunahitaji kuwawezesha wanawake vijana na watu wengine wote ambao wanajajiri. Lakini tunazo sheria zetu, sheria za namna ya kufanya kazi, mahali pa kufanya kazi na tumekuwa tu kitekeleza sheria hiyo hasa Serikali zetu za Mitaa.

Sasa katika utekelezaji ule wa sheria ni kweli kwamba watu wanakuwa wakorofi ni jukumu la Serikali ni kuonyesha maeneo ambapo wafanyakazi hawa akinamama wanafanya kazi. Lakini hatutakiwi kwa mfano wale mgambo wa Manispaa kuwanyanya na kuwanyang'anya vitu vyao, wanatakiwa wawaondoe kistaarabu. Lakini na wenye wene wanapoonyeshwa mahali pa kufanya kazi watii na waende kwenye maeneo hayo ambayo wanatakiwa wafanyie kazi bila kurudi tena kwenye yale maeneo ambayo waliyondolewa mara kwa mara. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa sasa mimi najua majina mengine Mwamoto.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona nina swali la nyongeza kwa Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa kumekuwa kuna hasa wakinamama wengi sana

huko vijiji wamejajiri katika sekta binafsi na wamekuwa na bidhaa nzuri sana. Lakini inapotokea kwenda kufanya maonesho labda Dar es Salaam au sehemu yoyote wamekuwa hawana uwezo wa kuzipeleka zile bidhaa zao ili ziweze kupata masoko. (*Makofii*)

Je, Serikali inasemaje ili kuweza kuwasaidia hao wakina mama ili wakaweze kupata masoko na kuweza kukidhi haja zao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kazi na Ajira, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ritta Kabati, kama ifuatavyo:-

Serikali imekuwa ikiweka mazingira mazuri ya kuweka masoko na maonyesho ya biashara mbalimbali hasa za hawa wajasiriamali. Lakini ni kweli tu kwamba kuhusu hawa wajasiriamali mimi ningeshauri kwamba ni vyema wakawa wanashirikiana kama kikundi ili kuwa na uwezo hata kuweza kufika kusafiri kwa pamoja na kufika maeneo ambapo kuna maonyesho ambapo bidhaa zao zinaweza zikaonwa na wateja na wakapata soko. Kwa hiyo, mimi nadhani mmoja ndiyo wanapata shida, lakini kama wakiungana nadhani wanaweza wakafikia masoko na maonesho hayo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali nimekuona umesimama sana, kwa kifupi.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Katika majibu ya Mheshimiwa Waziri wa Kazi, ameeleza kwamba mkakati mmojawapo wa kuwasaidia wanawake ni pamoja na suala zima la kuanzishwa kwa Benki ya Wanawake. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri atueleze ndani ya Bunge letu na Watanzania amba wanatuona hivi sasa, ni lini Benki hii itaweza kuwa na mtandao wake nchi nzima ikiwemo Wilaya ya Kasulu, ili kusudi wanawake waweze kunufaika na mikopo mbalimbali kuweza kuinua kipato chao?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhesimiwa Mbunge kuhusu Benki ya Wanawake kama ifuatavyo:- Benki ya Wanawake ndiyo imeanza miaka michache iliyopita. Benki ya Wanawake ndiyo imeanza miaka michache iliyopita na ili kuwa benki nchi nzima kunahitajika *capital* kubwa zaidi.

Kwa hiyo, huo mtandao utapatikana kutokana na uwezo ambaa ile Benki utaupata, ile ni mwanzo tu lakini nia ya kupeleka mikoa mingine kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri ipo pale pale, lakini benki inafunguliwa ikifuata sheria tulizoweka hapa Bungeni za Benki Kuu ambayo ndiyo inayo *control* biashara ya benki hapa nchini.

Kwa hiyo hatuwezi tu kupeleka kwa sababu ya kisiasa ni lazima tufuate utaratibu. Lakini tunachosema ni kwamba tutakachokifanya sasa hivi ni kujaribu kuongea na mabenki mengine tuwe na madawati yetu katika benki mbalimbali ili tuweze kuwashudumia wanawake na wanaume ambaa wanataka kupata huduma ya benki ya wanawake. (*Makofii*)

Na. 44

**Kuridhia Mkataba wa Shirika la Kazi Duniani Juu ya  
Haki ya Uzazi kwa Wafanyakazi Wanawake**

**MHE. ANGELAH J. KAIRUKI** aliuliza:-

Mwaka 2000 Tanzania ilisaini Mkataba Na. 183 wa Shirika la Kazi Duniani (*ILO*) unaohusu Haki za Uzazi kwa Wafanyakazi Wanawake.

Je, ni lini Serikali itaridhia Mkataba huo?

## **NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kazi na Ajira, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Angella Jasmine Kairuki, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Ili kuridhia mkataba wa kimataifa, upo mchakato unaopaswa kufanyika ikiwa ni pamoja na kurekebisha sheria na sera za nchi ili zifuate matakwa y a mkataba husika na kuwajengea uelewa wadau wote na wasimamizi wa sheria husika. Kuhusu mkataba namba 183 wa Shirika la Kazi Duniani ILO, unaohusu haki za uzazi kwa wafanyakazi wanawake Serikali imechukua hatua mbalimbali kuhusiana na suala hilo kama ifuatavyo:-

(i) Imezingatia na kutambua matakwa ya mkataba huu kwa kuweka katika sheria ya ajira na mahusiano kazini ya mwaka 2004 vifungu vinavyotoa haki, na kinga ya uzazi mahali pa kazi. Kifungu cha 33 cha Sheria tajwa kinatoa haki ya likizo ya uzazi ya siku 84 zenye malipo au siku 100 iwapo watazaliwa watoto zaidi ya mmoja.

Kifungu hicho kinakataza mama mjamzito na anayenyonyesha kufanya kazi hatarishi na kinatoa muda wa masaa mawili kila siku wakati wa kazi kwa mama anayenyonyesha kuweza kumnyonyesha mwanaye. Kwa mujibu wa kifungu hicho, endapo mtoto aliyezaliwa atafariiki katika kipindi cha mzunguko wa likizo ya uzazi yaani miaka mitatu, mfanyakazi huyo atastahili kupata likizo nyingine ya uzazi yenye malipo kamili.

(ii) Kifungu cha 20 cha Sheria ya Ajira na Mahusianao Kazini Na. 6 ya mwaka 2004 kinakataza mama mjamzito au anayenyosha kufanya kazi za usiku.

(iii) Ili kupitia ufadhili wa Shirika la Kazi Duniani, mradi wa pamoja wa umoja wa Taifa yaani *United Nations Joint Programme two* Wizara ikishirkiana na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi TUCTA na Chama cha Waajiri Tanzania ATE, imeweza kuwapatia mafunzo wafanyakazi 600 na waajiri 400 ili kuwajengea uwezo na uelewa kuhusu haki na kinga ya uzazi mahali pa kazi kwa mujibu wa mkataba huo na sheria ya kazi wa ajira na mahusiano kazini.

(iv) Aidha, maafisa kazi katika ofisi zetu zote wamejengewa uwezo na uelewa ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao ya usimamizi wa sheria za kazi katika eneo hilo la haki na kinga ya uzazi mahali pa kazi.

(v) Mwisho, baadhi ya mifuko ya Hifadhi ya Jamii kama NSSF, na GEPF inatoa mafao ya uzazi kwa mujibu wa matakwa ya mkataba huo wa ILO Na. 183.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua na michakato hii inayoendelea kuchukuliwa na Serikali hatimaye itafikisha Tanzania wakati muafaka wa kuridhia mkataba huu wa ILO. Tukumbuke tu kwamba hadi sasa ni nchi 22 tu duniani zilizoridhia mkataba huu Namba 183.

**MHE. ANGELAH J. KAIRUKI:** Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri na pamoja na maelezo kwamba nchi 22 tu ndiyo ambazo zimeridhia, bado hii halalalishi Tanzania kuchelewa au kutokuridhia. Ningependa kufahamu sasa kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri ni nini kinachokwamisha nchi yetu kuridhia mkataba huu hasa ukizingatia katika maelezo ambayo ametoa ni haki chache tu ambazo zinapatikana katika sheria yetu ya kazi ambazo bado hazimo katika mkataba huu wa kimataifa. (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kazi na Ajira, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Angella Kairuki kama ifuatavyo, ni kama nilivyosema zile nchi 22 dunia kwamba tu ndiyo zimeridhia ilikuwa tu kama taarifa na ufahamu.

Lakini nieleze kwamba kitu cha msingi ni huu mchakato ambao tunaendelea nao bado kuangalia sera na sheria zetu mbalimbali ili hatimaye tutakaporidhia mkataba huu tuwe na hakika kwamba tunaweza tukautekeleza vipengele vyote ambavyo sasa vitakuwa vinaoana na sera na sheria zetu ambazo tunazo nchini kwa sababu tukikurupuka tukaridhia tukakuta kuna mambo

ambayo bado kwa mujibu wa sheria na sera zetu hatuwezi tukatekeleza kwa wakati huu tunaweza tukajikuta katika matatizo ya kisheria.

**MWENYEKITI:** Nilimwona Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya!

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona.

Kwa kuwa, mtoto anahitaji malezi ya Baba na Mama kuanzia siku anapozaliwa mpaka anapokuwa mtu mzima na kwa kuwa, nchi nyine wamekuwa wanatoa likizo kwa akina Baba kusaidiana na akina Mama wakati wa kulea mtoto anapozaliwa.

Je, nchi yetu sasa haioni kwamba kuna haja kuendana sambamba na mikataba inayoingia ili iweze kutoa likizo pia kwa akina Baba ili kuweza kumsaidia Mama kulea mtoto hasa katika kipindi cha miezi sita ya mwanzo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri ni swali zuri sana hilo, majibu tafadhalii!

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kazi na Ajira, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sakaya kama ifuatavyo:-

Suala alilozungumza Mheshimiwa Sakaya ni muhimu sana na inatakiwa kwa kweli hata sis wazazi wa kiume tuwasaidie akina Mama wanapoifungua, ndio maana katika Sheria yetu tumeshalizingatia hilo na kwa kuanzia Sheria inasema mwanaume naye achukue likizo angalau ya siku tatu ama kable ya uzazi au baada ya uzazi yeje atapanga vizuri.

Lakini kwa sasa tunazo siku tatu ambazo wanaume tunaruhusiwa kuchukua likizo wakati wake zetu wamejifungua.

**MWENYEKITI:** Jamani tatizo ni muda kwa hiyo, twende swali linalofuatia la Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki na litaulizwa na Mheshimiwa Hussein Mzee.

Na. 45

#### Faida ya Jumuiya ya Afrika Mashariki

**MHE. HUSSEIN MUSSA MZEE** aliuliza:-

- (a) Je, Serikali inaweza kutueleza faida gani Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imepata katika Jumuiya ya Afrika Mashariki tangu juhudhi za kufufuliwa kwake zilipoanza mwaka 1999?
- (b) Je, ni kati ya faida hizo Tanzania Zanzibar imepata faida gani?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki najibu swali la Mheshimiwa Hussein Mussa Mzee Mbunge wa Jang'ombe lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, tangu kuanzishwa upya kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1999 Tanzania kama nchi mwanachama wa Jumuiya hiyo imepata faida mbalimbali. Baadhi ya faida zilizopatikana ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuongezeka kwa mauzo ya Tanzania katika Soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka hadi mwaka. Kulingana na takwimu, mapato yaliyotokana na mauzo ya Tanzania katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki yameongezeka kutoka dola za Kimarekani milioni 96.40 mwaka 2005 hadi kufikia dola za Kimarekani milioni 450.10 mwaka 2010 kufuatia kuanzia kutekelezwa kwa Umoja wa Forodha.

(ii) Kuimarka kwa urari wa biashara kati ya Tanzania na nchi wananchama wa Jumuiya pamoja na kuongezeka kwa bidhaa za viwandani vinazouzwa katika nchi hizo. Urari wa biashara kati ya Tanzania na nchi wananchama umeimarika kutoka nakisi (*deficit*) ya dola za Kimarekani milioni 64 hadi mwaka 2005 hadi kufikia ziada (*surplus*) ya dola za Kimarekani bilioni 164 kwa mwaka 2010.

(iii) Kuongezeka kwa uwekezaji katika sekta za Viwanda, Ujenzi, Utalii, Usafirishaji na Kilimo kutoka miradi 14 yenye thamani ya dola za Kimarekani milioni 18.96 iliyozalisha ajira 378 mwaka 2005 hadi kufikia miradi 197 yenye thamani ya dola za Kimarekani milioni 480.22 iliyozalisha ajira 12.052 mwaka 2010.

(iv) Kuongezeka kwa soko la bidhaa, ajira mitaji na biashara kutoptana na utekelezaji wa Soko la Pamoja ambapo Watanzania wengi wameanza kuzitambua fursa hizo na wamehamasika kuanza kuzitumia; na

(v) Kuimarka kwa miundombinu ya kiuchumi kutoptana na utekelezaji wa miradi ya pamoja ya kikanda. Kwa mfano ujenzi wa barabara za Arusha – Namanga – Athi -River na barabara ya Tanga – Horohoro, matumizi endelevu ya Ziwa Victoria, ujenzi wa Makao Makuu ya ndani ya Tanzania, vijiji Arusha.

(vi) Kuimarka kwa huduma za usafiri wa anga kutoptana na kuanzishwa kwa Wakala wa Udhibiti wa Usalama wa Anga wa Afrika Mashariki (*Civil Aviation Safety and Security Oversight Agency*) (*CASSOA*).

(b) Mheshimiwa Spika, Tanzania Zanzibar ikiwa ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa ikipata faida kama zilivyoainishwa katika jibu langu la sehemu (a) Lakini pamoja na hayo, miradi ya Zanzibar imejumuishwa katika miradi ya Kikanda ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa ajili ya kuombewa fedha na ufadhili ikiwemo mradi wa ujenzi wa uwanja wa ndege Pemba na Zanzibar unaoendelea hivi sasa kwa ufadhili wa Benki ya *Exim* ya China. Hali kadhalika, mradi wa Bandari ya Maruhubi ni mojawapo ya miradi ya Tanzania iliyopendekezwa katika miradi ya vipaumbele katika Mkakati wa Uchukuzi.

Vilevile, mradi wa ujenzi wa Chelezo (*Dry-Dock Construction*) na Kivuko (*Roll on Roll – Off – RORO*) kati ya Bandari ya Zanzibar, Dar es Salaam na Mombasa, Tanga na Mtwara ni mionganoni mwa miradi ya vipaumbele vya Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyowasilishwa katika Ushirikiano wa Utatu wa COMESA- EAC-SADC.

Mheshimiwa Spika, nina furaha kiliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Tanzania imepewa heshima ya kuwa mwenyeji wa Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo Makao yake Makuu yatakuwa Zanzibar

**MHE. HUSSEIN MUSSA MZEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongenza.

Je, Wizara haioni kuna haja ya kujenga ofisi ndogo Zanzibar ili kuwaongezea karibu watu wa kule kupata nafasi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri umesikia ? Hebu rudia tena swali lako.

**MHE. HUSSEIN MUSSA MZEE:** Je, Wizara haioni haja ya kujenga ofisi ndogo Zanzibar kwa ajili ya kuwasogezesa huduma hizo watu wa Zanzibar?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu!

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza hapo awali kwamba Wizara yetu katika mtangamano wa Afrika Mashariki sasa hivi mtangamano mzima una karibu miaka kumi na kipindi cha mwanzo kilikuwa ni kipindi cha matayarisho na kujaribu kuoanisha baadhi ya mambo.

Kwa hiyo, pamoja na hamasa ambazo zinaendelea katika sehemu nyingi, jibu la Mheshimiwa Hussein ni kusema kwamba upo umuhimu na Wizara inaona umuhimu wa kuwepo ofisi pale lakini kwa hivi sasa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kitengo au Idara ya Uhusiano wa Kimataifa na *Diaspora* ina maafisa maalum ambao wanahusika katika kuratibu mambo ya Afrika ya Mashariki palepale Zanzibar.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonyesha kuwa 70% ya wafanyabiashara wanaofanya biashara mpakani mwa soko la Afrika Mashariki yaani Holili Namanga Mkoa wa Kilimanjaro, Namanga, Arusha na Sirari Mkoa wa Mara ni Sekta isiyo rasmi hususani wanawake.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuweka mazingira muafaka kwa wanawake hawa ikizingatiwa kwamba hakuna huduma za jamii wala miundombinu rasmi ya soko na hata Zahanati?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Katika jibu langu la msingi nilisema kwamba Jumuiya ya Afrika Mashariki ilikuwa na awamu mbili kubwa ambapo awamu ya kwanza ni ya matayarisho na awamu ya pili sasa hivi ni kuanza kutekeleza makubaliano ambayo yamekubaliwa.

Katika kujibu swali lake Mheshimiwa Mbunge ni kwamba, hivi sasa kuna harakati nyingi sana za kusajihisha wananchi hasa hawa ambao anawazungumzia ambao wapo mipakani katika kutumia fursa ambazo zinapatikana kwenye Jumuiya hii ya Afrika Mashariki.

Hivi juzi tu mimi mwenye binafsi nilifanya ziara za mipakani Shimoni na Mtukula na vilevile ziara kama hizi zilikuwa zinafanya kwa mfano sehemu za Murongo na hata Holili tuna mpango wa kwenda ili kuwasajihisha wananchi wa pale wajue namna gani ya kuweza kutumia fursa kwa sababu ni fursa ambazo ni nyepesi sana na nyingine zinaweza kuwaletaa faida.

Pamoja na hayo kuna mipango kama ilivyoonyeshwa kwenye semina zinazotolewa, matangazo, mabango na kadhalika, kwa hiyo, namwomba tu Mheshimiwa Mbunge wakati utakapofika tushirikiane naye na twende sambamba pamoja na Wabunge wetu wa Afrika Mashariki katika kuwasajihisha wanawake na wawananchi wengine ili kutumia fursa hizi zinazopatikana Afrika Mashariki.

Na. 46

#### **Ushiriki wa Zanzibar Katika Jumuiya ya Afrika Mashariki**

**MHE. MWANAMRISHO T. ABAMA** aliuliza:-

Tanzania ambayo ni Muungano wa Serikali mbili za Tanganyika na Zanzibar ni mionganoni mwa nchi zilizoasisi Jumuiya ya Afrika Mashariki; katika *protocol* ya Afrika Mashariki ni mambo manne tu ambayo ni ya Muungano:-

- (a) Je, kwa mambo yasiyo ya Muungano Zanzibar itawezaje kuyasimamia yenewe kama nchi?
- (b) Je, matatizo na kero zilizopo za Muungano wa Tanganyika na Zanzibar haziwezi kuwa ni kero na vikwazo kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa sababu haziwaondolewa?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mwanamrishi Taratibu Abama, Mbunge wa Viti

Maalum, naomba kutoa ufanuzi kuwa Jumuiya ya Afrika, Mashariki inaongozwa na Mkataba (*Treaty*) wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Vilevile, kila baada ya makubaliano nchi wananchama husaini itifaki (*Protocol*) ambazo zinakuwa sehemu ya mkataba. Baada ya ufanuzi huo sasa najibu swali la Mheshimiwa Mbunge lenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika nyongeza ya kwanza ya Ibara ya 4 imeainisha kuwa masuala ya Mambo ya Nje ni Masuala ya Muungano.

Kwa kuzingatia matakwa ya Katiba na kwa kutambua kuwa masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ni kati ya masuala ya Mambo ya Nje, Wizara imeendelea kuwashirikisha wadau kutoka pande zote mbili za Muungano katika utekelezaji wa masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ushirikishwaji huo umefanyika katika vikao vyote vya maandalizi na majadiliano, mikutano ya Baraza la Mawaziri na Mabaraza ya Jumuiya.

Aidha, washiriki toka pande zote mbili za Muungano hushirikisha kikamilifu katika Kamati na Vikosi Kazi mbalimbali ambavyo huundwa kuchambua na kuandaa misimamo ya Tanzania, na Vikosi Kazi hivyo ni Kikosi Kazi cha Majadiliano ya Kuunda Jumuiya ya Afrika Mashariki, Kikosi Kazi cha Majadiliano ya Kuanzisha Umoja wa Forodha, Kikosi Kazi cha Majadiliano ya Uanzishwaji wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia imeishirikisha kikamii fu Tanzania Zanzibar katika majadiliano ya Itifaki mbalimbali zinazosimamia masuala yasiyo ya Muungano. Utekelezaji wa hizo kwa upande wa Zanzibar utasimamiwa na Sera na Sheria za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Itifaki hizo ni pamoja na:-

- (a) Itifaki ya kuzuia usafirishaji na usambazai wa Madawa ya Kulevyia katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.
- (b) Itifaki ya uhakiki wa ubora, vipimo na udhibiti katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.
- (c) Itifaki ya kusimamia mazingira na maliasili katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.
- (d) Itifaki ya kusimamia utalii na wanyamapori katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.
- (e) Itifaki ya kuanzisha Kamisheni ya Sayansi na Teknolojia ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.
- (f) Itifaki ya kuanzisha Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.
- (g) Itifaki ya kuanzisha Kamisheni ya Ultafiti wa magonjwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu umeiwezesha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuzingatia maslahi ya pande zote mbili za Muungano katika shughuli zote za uendelezaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikisha Bunge lako Tukufu kwa Tanzania Zanzibar itaendelea kushirikishwa kikamii fu katika masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na kwamba kero za Muungano haziwezi kuwa kikwazo kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Kamati ya Kutatua Kero za Muungano iliyopo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais inaendelea kuzitatutia ufumbuzi kero zinazowasilishwa na pande zote mbili za Muungano.

**MHE. MWANAMRISHO T. ABAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri lakini nina swali dogo la nyongeza.

Je, kuna vikwazo gani vinavyopelekea Zanzibar isiingie kama nchi katika Shirikisho la Afrika Mashariki?

**MWENYEKITI:** Huo ndiyo uulizaji mzuri wa maswali. Mheshimiwa Naibu Waziri maswali, safi sana!

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyezekiti, napenda kuchukua nafasi hii kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwanamrisho Taratibu Abama kuwa kuna vikwazo gani vinavyofanya Zanzibar isishirikishwe katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kama ni Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyezekiti, kwa kusema kwamba kuna vikwazo hilo siwezi kulzungumzia kwa sababu vikwazo havipo lakini isipokuwa tuna taratibu ambazo tumezipanga wenyewe kama nilivyosema katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwamba Mambo ya Nje yatakuwa yanashughulikiwa na Serikali ya Muungano.

Kwa hiyo, katika yale mambo ambayo hayamo katika mjumuisho wa shughuli za Muungano kama tulivyo sema kwamba wataaalamu wa Sheria wanasema palipokuwa hapakuzungumzia kwenye Sheria basi pana uhalali wa kilitenda na kama hakuna uhalali wa kutenda basi unatafuta mwongozo amba o unaweza kufanya lile jambo likawa linashughulikiwa.

Kwa hiyo, mwongozo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki juu ya kujadili mambo ndiyo unaotuongozwa sisi sasa hivi kushughulikia mambo ya Zanzibar ambayo hayapo katika Muungano. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Muda si rafiki kwa kweli na swali linalofuata linakwenda kwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na litaulizwa na Mheshimiwa Abbas Zuberi Mtemvu Mbunge wa Temeke.

Na. 47

#### **Ukweli Juu ya Kikombe cha Babu wa Loliondo**

**MHE. ABABAS ZUBERI MTEMVU** aliuliza:-

Tanzania imejipatia sifa kubwa ndani na nje ya nchi kutokana na huduma ya kikombe cha Mchungaji Mstaafu Ambilikile Mbetwa Mwaisapile (Babu wa Loliondo) kinachosemekana kutibu magonjwa sugu ukiwemo UKIMWI, Kisukari na kadhalika.

(a) Je, kuna ukweli wowote juu ya kikombe kutibu magonjwa hayo sugu ukiwemo UKIMWI?

(b) Je, ni watu wangapi wamekufa hadi sasa toka Babu huyo wa Loliondo aanze kutoa huduma hiyo?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibuu:-

Mheshimiwa Mwenyezekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abbas Zuberi Mtemvu, Mbunge wa Temeke, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyezekiti, baada ya kujitokeza Mchungaji Mstaafu Ambilikile Mbetwa Mwaisapile, kwa jina maarufu Babu wa Loliondo na kikombe cha kutibu magonjwa sugu ukiwemo UKIMWI, Kisukari, Pumu, Kifafa na Saratani, Wizara kuititia Taasisi zake za utafiti ilianza zoezi la utafiti ili kubaini kama dawa hii ina madhara kwa binadamu, matokeo yalionyesha kuwa dawa hii haikuwa na madhara yoyote kwa matumizi ya binadamu.

Mheshimiwa Mwenyezekiti, baada ya hapo Taasisi hizo zilianza maandalizi ya utafiti kuhusu ufanisi wa dawa hiyo kutibu ikiwa ni pamoja na kuandaa andiko la utafiti (*Research Proposal*). Baadaye Wizara ilipokea ombi toka Shirika la Afya Duniani (*WHO*) Kanda ya Afrika Mashariki (*Brazaville*) kuwa wangependa kushirkiana na Tanzania katika utafiti huo. Hivyo, ikabidi andiko

(*Proposal*) hilo liandikwe upya ili kujumuisha masuala ya itifaki ya tafiti za kimataifa ambazo WHO wanazisimamia.

Mapendekezo yaliotolewa ni pamoja na kuandaa wagonjwa 200 ambaao watafanyiwa tafiti hiyo (*Multi – Centre Study*). Tafiti ya namna hii ni ya gharma kubwa, hivyo utaratibu wa kuandaa andiko (*Proposal*) pamoja na kituo cha kuwaweka wagonjwa yanaendelea na pindi maandalizi hayo yatakapokamilika pamoja na andiko (*Proposal*) hilo litawasilishwa Tume ya Sayansi na Teknolojia (*COSTECH*) ili kupata fedha zinazotakiwa katika utafiti huo. Suala hili limesababisha kuchelewa kuanza kwa tafiti hiyo.

Naomba kwa Wabunge na Bunge lako Tukufu na wananchi kwa ujumla kuwa na subira juu ya utafiti huu.

(b)Mheshimiwa Spika, kwa kuwa utafiti haujakamilika siyo rahisi kujua idadi ya watu waliofariki kutokana na tiba ya kikombe cha babu wa Loliondo. Aidha, hakuna taarifa za vifo viliviyotokana na matumizi ya moja kwa moja ya dawa hiyo.

Hata hivyo, jumla ya watu 116 walifariki dunia kutokana na sababu mbalimbali wakiwa Samunge au wakitoka kituo cha Arusha kupitia Mto wa Mbu, Bunda kupitia Serengeti wakielekea Samunge kupata tiba hiyo. Katika kufuatilia ilibainika kuwa watu hao waliofariki walikuwa wakisumbuliwa na magonjwa sugu kama ifuatavyo:-

Kisukari – 43, Shinikizo la juu la damu - 20, UKIMWI – 17, Pumu – 19, Saratani – 6, magonjwa mengine -11.

**MHE. IDD M. AZZAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri ni kwamba utafiti utachukua muda mrefu na utafiti ule unahusisha pia kujua kwamba kikombe kile kilikuwa kinatibu ama haktibu.

Je, Mheshimiwa Waziri ama Serikali haioni ni busara tu ama haioni kwa nini isitumie busara ya kawaida tu kwa sababu mionganoni mwa watu ambaao wamekwenda kupata matibabu yale au kupata kikombe kile ni pamoja na Waheshimiwa Mawaziri, Wabunge na Viongozi mbalimbali?

Ili kujua kama kikombe hiki kinatibu au la kwa nini Serikali isifanye utafiti wa kawaida tu kuwaauliza hawa waliokwenda mionganoni mwao wangapi wamepona na wangapi hawakupona? (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu. Maana kwa kweli utafiti uanze humu humu. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:**Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ieleweke kwamba kwa sababu tulikuwa tunataka majibu ya uhakika kwa ajili ya faida ya Watanzania na ndio maana tuliweka utaratibu ambaao tuliweza kuufuatilia tuweze kupata majibu ya kisayansi hasa.

Kwa hiyo, tulibidi tufuate utaratibu ambaao unapotaka kuanza tafiti za kisayansi lazima utekeleze. Kwa hiyo, tumeona angalizo hilo kwamba wananchi wanataka majibu ya haraka, lakini tu naomba kwa niaba ya Watanzania wenzangu hapa inaelezwa kwamba kwa nini tusifanye haraka haraka. Kwa wao ambaao tayari wamekunywa hiyo dawa na sisi tuwafuatilie. Hiyo ni ridhaa yao lakini tunesema kwamba utaratibu wetu sisi tunaupanga na hivi karibuni tunaukamilisha na tutaanza zoezi hili na tutawapa taarifa ambayo itakuwa ni sahihi zaidi kuliko hiyo njia fupi mnayoitaka ambayo baadae nayo italeta utata hata majibu yetu kwa Wanasyansi wengine.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa kumezuka wimbi la waganga wa kienyeji wakijitangaza katika redio, televisheni na wengine wakiweka mabango na wengi wao wanatoka maeneo ambayo Mheshimiwa rafiki yangu na mtani wangu Mheshimiwa Shekifu anakujua wakidai kutibu magonjwa sugu na yaliyoshindikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii inawatia wananchi wengi hasara na inawezekana wananchi wengi wanlishwa sumu. Je, Serikali kwa kutumia Wizara ya Afya inacho Kitengo chochote au sheria yoyote inayodhibiti wimbi hili kwa manufaa ya watu wetu wasiendelee kutapeliwa na kulishwa mambo ambayo hayafai?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inacho Kitengo na sheria ipo ambayo inasimamia utaratibu na utendaji wa hawa wenzetu wanaotoa tiba ya asili. Hawa ambao wanatangaza hayo matangazo nao tunawafuutilia na baadhi yao tumeshaanza kuwachukulia hatua za kisheria ili tuweze kuwadhibiti wasiendelee na matangazo kama hayo.

Na. 48

**Kutungwa Sheria ya Kulinda na Kuendeleza**  
**Ustawi wa Wazee**

**MHE. MARY P. CHATANDA** aliliza:-

Serikali ilianzisha "Sera ya Taifa ya Wazee" ya Mwaka 1999 ya kuwatambua na kuwathamini wazee; lakini bado wanakabiliwa na matatizo ya huduma za afya, pensheni, umaskini na kutoshirikishwa katika maamuzi:-

Je, Serikali haioni ni wakati muafaka sasa wa kutunga Sheria itakayolinda na kuendeleza ustawi wa wazee?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mary Pius Chatanda, Mbunge wa Viti Maalum, naomba kuliariifu Bunge lako Tukufu kwamba Sera ya Taifa ya Wazee ilitungwa mwaka 2003 n siyo 1999 kama inavyoonekana kwenye maelezo ya swali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya masahihisho hayo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kuwa baada ya kupitishwa kwa Sera ya Taifa ya Wazee, ingefuatiwa na kutungwa kwa Sheria ya Wazee kwa utekelezaji wa Sera hiyo ili kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazowapata wazee zikiwamo huduma za afya na ustawi wao.

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeanzisha taratibu za maandalizi ya Muswada wa Sheria ya Wazee na kuuwasilisha katika vikao mbalimbali vya Serikali ili hatimaye iletwe katika Bunge lako Tukufu. Tayari Baraza la Mawaziri lilishapitia Muswada huo na kutoa maelekezo ya kuuboresha ambayo sasa Wizara yangu inaifanyia kazi na Wizara ikikamilisha zoezi hili nitawasilisha Bungeni.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Kwa kuwa Sera hii ilipitishwa mwaka 2003 sasa ni miaka minane, ni lini sasa Serikali itakuwa imekamilisha na kuboresha Muswada huu na kuuleta hapa Bungeni?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli ni muda mrefu umepita toka sera hii ilivyopitishwa, lakini jibu langu la msingi ni kwamba tulishaanza taratibu za maandalizi na sasa hivi tunamalizia. Naomba niliahidi Bunge lako Tukufu huenda katika vikao vya karibuni vya Bunge tutawasilisha hapa Bungeni. (*Makofii*)

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru sana majibu ya Wizara. Lakini suala hili la wazee hasa kutibiwa limezungumzwa kwa muda mrefu sana. Serikali imetoa maelekezo na ahadi zimetolewa nyngi humu Bungeni kwamba wazee watapewa matibabu bure. Hivi ni lazima Muswada uje Bungeni, Serikali haiwezi ikatoa maelekezo kwa Watendaji na utekelezaji ukafanyika?

**MWENYEKITI:**Ahsante sana, swali zuri.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasubiri kuanzisha sheria hii sio kwamba tumekaa kimya. Kama utakumbuka mwaka 2009 Waziri Mkuu katika Kuazimisha Siku ya Wazee alitoa maelekezo kwamba wazee hawa waanze kupata huduma hizi kwa kutengewa maeneo maalum katika vituo vyetu vinavyotoa huduma za tiba vikiwemo hospitali, vituo nya afya na zahanati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshaanza na karibuni mikoa yote kuna madirisha maalum katika Hospitali za Wilaya ambao wanatoa huduma hizi kwa wazee.

Vilevile tumeangalia na sasa hivi tunaweka utaratibu pale ambapo inashindikana kumpa matibabu huyu mzee tunaona sasa kuna mazingira ya kutumia Mfuko wa Afya ya Jamii ambao Serikali tutawaingiza wanachama hawa wazee ili nao wanufaikie wapate huduma hizo bure bila ya kipingamizi. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Muda sio rafiki mtaniwia radhi sana na swali linalofuata linakwenda Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na litaulizwa na Mheshimiwa Dr. Faustine Englebert Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni.

Na. 49

#### **Ujenzi wa Mji wa Kisasa Kigamboni**

**MHE. ESTER A. BULAYA (K.n.y. MHE. DR. FAUSTINE E. NDUGULILE)** aliuliza:-

Mwaka 2008 Serikali ilitangaza azma ya kujenga Mji Mpya katika eneo la Kigamboni na hivyo wakazi wa maeneo hayo hawajaweza kujenga au kuuza nyumba zao:-

- (a) Je, ni lini Serikali itaanza rasmi ujenzi huo na utaanzia wapi?
- (b) Je, Serikali itakuwa tayari kulipa fidia kwa hasara na usumbufo kwa wananchi wa Kigamboni kwa kushindwa kuuza au kuendeleza maeneo yao?
- (c) Je, wananchi wa Kigamboni watanufaikaje na uwekezaji utakaokuja?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** aliijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Faustine Englebert Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni, lenye sehemu (a), (b) na (c ) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Mji Mpya wa Kigamboni unatarajiwa kuanza mwaka huu wa fedha (2011/2012) kwa kupima njia za barabara kuu eneo zima la Mji Mpya, maeneo ya umma (*public areas*) na maeneo ya kujenga makazi mbadala (*resettlement areas*) ambapo hawa wakazi watakaa kwa muda pamoja na kufanya uthamini wa mali zilizo ndani ya maeneo hayo.

Aidha, Mamlaka ya Kusimamia na Kuratibu Ujenzi wa Mji Mpya (*Kigamboni Development Authority*) itaundwa. Wizara imeshateua Wajumbe wa Kamati Maalum itakayoshauri juu ya Muundo na majukumu ya Mamlaka hiyo. Mheshimiwa Mbunge wa Kigamboni ni Mjumbe wa Kamati hiyo.

Sambamba na hatua hiyo, Shirika la Nyumba la Taifa litaandaa michoro kwa ajili ya ujenzi wa makazi mbadala katika eneo la hekta 100 litakalotolewa kwa Shirika hilo katika eneo la Kibada. Baada ya kukamilika hatua hizo za awali, fidia kwa wananchi wote watakaoathirika italipwa mwaka wa fedha 2012/2013, na ujenzi wa nyumba na miundombinu utaanza.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haitalipa fidia wakazi wa eneo la mradi kwa sababu haikuwazuia wananchi wanaoishi kwenye eneo hilo kuendelea na shughuli zao za kawaida isipokuwa kwamba Tamko la Serikali la Oktoba 2008 lilitisha maendelezo ya ardhi wanayomiliki ikiwemo ujenzi wa majengo mapya ya kudumu. Tamko hilo la Serikali lilitolewa kwa mujibu wa Kifungu cha 24 cha Sheria ya Mipangomiji Na. 8 ya Mwaka 2007 ambacho kinahusu kusitisha maendelezo ndani ya maeneo husika kwa muda wa miaka miwili. Vilevile Tamko la Serikali halikumzuia mmliki yejote wa mali Kigamboni kuza mali zao katika kipindi hicho cha Mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa amri ya kusitisha ujenzi ilikoma mwezi Oktoba, 2010. Baada ya hapo hakukuwepo na pingamizi la Kisheria la kuendeleza maeneo husika kuanzia wakati huo kwa kuzingatia matumizi ya ardhi illoainishwa kwenye Mpango Kamambe wa Mji Mpya na maelekezo ya Kanuni ya 124 ya Kanuni za Udhibiti wa Ujenzi zilizotolewa chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Sura 288) zinazoolekeza kwamba kila anayeendeleza eneo katika Mji ni sharti awe na kibali cha ujenzi kabla hajafanya maendeleo ya aina yoyote.

Kwa kuzingati Kanuni hiyo mwezi Februari, 2011 Wizara ya Ardhi, Nyumba na Makazi ilitoa tamko liliowakumbusha wanaomiliki ardhi katika eneo la Mji Mpya kuwa hawana budi kuomba na kupewa vibali vyta ujenzi kabla ya kufanya ujenzi wowote, ili ujenzi huo uzingatie matumizi ya ardhi yaliyoainishwa katika rasimu ya Mpango Kabambe wa Mji Mpya wa Kigamboni, kama ilivyotakiwa chini ya Sheria ya Mipangomiji, Kifungu cha 41.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kigamboni watanufaika kutokana na ujenzi wa Mji Mpya Kigamboni kutokana na kupata fursa ya kuwa na makazi bora na kupata ajira wakati wa ujenzi wa mji huo.

Vilevile watanufaika kutokana na miundombinu na huduma za kijamii kuboreshwa, na wataishi katika Mji wenye hadhi na mandhari nzuri. Wananchi wa Jiji la Dar es Salaam watanufaika kutokana na ujenzi wa Mji Mpya kwa kusaidia kupunguza msongamano wa shughuli, watu na magari katika eneo la katikati ya Mji na Watanzania wote watanufaika kutokana na upanuzi na uboreshaji wa miundombinu ya Jiji, hususan bandari ya Dar es Salaam ambayo sehemu yake ipo katika Mji Mpya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri kiasi ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kuna taarifa na malalamiko kutoka kwa wananchi wa Kigamboni hususan wanaohusika kwamba *Master Plan* ya Mradi Mpya wa Ujenzi wa Kigamboni haikuzingatia Sheria ya Ardhi Na. 4 ya Mwaka 1999 na Sheria ya Mipangomiji ya Mwaka 2007 ambayo pamoja na mambo mengine inaitaka Wizara kabla haijaanza kubadilisha matumizi ya eneo husika hususan ambayo ina makazi ya watu kwenda kufanya vikao na wananchi na kupanga ni jinsi gani ambavyo huo mradi utaendeshwa na makubaliano yote kuhusiana na gharama kitu ambacho hakijafanyika kama sheria ambavyo inataka.

Je, Serikali haioni kwamba ni wakati muafaka wa kurudi na kuanza mchakato mpya kwa kuwashirikisha wananchi wa Kigamboni kwa kufanya vikao na kukubaliana kabla ya wataalam kuingiza mpango huo kwenye makaratsi kwa ajili ya utekelezaji ili kuondoa *contradiction* na malalamiko yaliyojitekeza sasa hivi kwamba kuna mazingira ya dhulumati kuhusiana na suala zima la fidia kutokana na ardhi kuwa na thamani.

Swali langu la pili, kama Mheshimiwa Naibu Waziri ambavyo amejibu kwenye swali lake la msingi kwamba lengo ni kutaka kuufanya Mji wa Kigamboni kuwa wa kisasa na kwamba lengo la Serikali kuanzisha mradi huo wa Kigamboni ni pamoja na kumwezesha Mtanzania hususan wa Kigamboni kumuinua kiuchumi na kumuondolea umaskini.

**MWENYEKITI:** Kwa kifupi.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Lakini kwa uzoefu tulionao inaonyesha kwamba wawekezaji ambao wanaokuja wanatumia ardhi yetu kukopa benki ili kuendeleza sehemu ambayo wamepewa. Je, Serikali haioni kwamba kama kuna nia ya dhati ya kumnufaisha mwananchi wa Kigamboni kwa nini mwananchi huyo wa Kigamboni asiwe mbia akawezeshwa kutokana na ardhi yake ili yeze kuendeleza eneo hilo kwa kushirikiana na Serikali badala ya mfadili. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Limeeleweka Mheshimiwa. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyelekiti, kwanza kuhusu ushirikishwaji wa wananchi wa Kigamboni katika maandalizi ya Mpango Kabambe wa Kigamboni napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba wananchi wa Kigamboni walishirikishwa viliyo. Mikutano ya hadhara iliendeshwa katika Kata na Mitaa yote ya Kigamboni kuanzia tarehe 2 Desemba, 2008 hadi tarehe 24 Machi, 2009.

Mheshimiwa Mwenyelekiti, zaidi ya hayo mapema mwaka huu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Makazi alifanya Mikutano ya hadhara katika maeneo ya Kigamboni ili kwa mara nyingine tena kuwashirikisha wananchi kuwaelewesha umuhimu wa wao kushiriki sio kuwa watazamaji tu bali kushiriki kwa vitendo kuwekeza katika Mji Mpya wa Kigamboni.

Mheshimiwa Mwenyelekiti, suala la pili kuhusu ushirikishwaji wa wananchi katika uwekezaji napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Sera ya Serikali yetu ni kuhakikisha kwamba wananchi wanakuwa wabia katika miradi yote ambayo inawekezwa na wageni.

Tusingependa kuona Mji wa Kigamboni, tungenesema kwa Kiingereza unakuwa *foreigners* tungependa kuona kwamba Mji ule mandhari inabadilika lakini unabaki kwa Watanzania kwa maana ya kwamba wamiliki wa ardhi pale Kigamboni hivi sasa wanaendelea kuwa ni Watanzania wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyelekiti, hivi sasa kuna wawekezaji kadhaa wameanza kuwekeza hapa nchini na sisi pale ambapo tumeshiriki katika kujadili taratibu za uwekezaji tumehimiza kwamba walau basi Serikali katika eneo hilo au wananchi kupitia Serikali yao wamiliki kiwango kisichopungua asilimia 25 ya kile kitakachowekezwa katika eneo hilo.

Kwa hiyo natoa wito kwa wananchi wa Kigamboni kwamba wale wote wanaomiliki maeneo katika eneo hilo wajitokeze wakitaka wao wenye waa like wawekezaji popote wanapopatikana waje washirikiane wajenge kile ambacho kimesanifiwa katika eneo la Mpango wa Mji mpya na Serikali itaidhinisha. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante maswali yalikuwa marefu na majibu marefu kwa hiyo tunaendelea. Swali linalofuata linaelekezwa kwa Wizara ya Katiba na Sheria na linaulizwa na Mheshimiwa Faki Haji Makame.

Na. 50

#### **Mikataba ya Uwekezaji**

**MHE. FAKI HAJI MAKAME** aliuliza:-

- (a) Je, Serikali inaposaini mikataba hasa ya miradi ya huduma za jamii inazingatia gharama za huduma hizo kwa wananchi wenye uwezo mdogo kifedha?
- (b) Je, Serikali inasimamia vipi wajibu wa Makampuni husika kwa jamii inayozunguka miradi (*Corporate Social Responsibility*)?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyelekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Faki Haji Makame, Mbunge wa Mtoni, lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya Serikali kutia saini mikataba ya uwekezaji ikiwemo mikataba ya huduma za jamii, mikataba hiyo hujadiliwa kwanza na Kamati ya Majadiliano. Kamati hii huhakikisha kuwa vipengele vya Mkabata husika vinazingatia maslahi ya taifa.

Mikataba ihusuyo huduma za jamii kama vile maji, simu, reli na afya nayo pia hupitia utaratibu huo. Majadiliano haya huangalia Nyanja zote zikiwemo Sheria, fedha, uchumi, teknolojia, mazingira na huduma inayokusudiwa kutolewa huangaliwa na hujadiliwa na wataalam husika.

Gharama, ada au tozo zozote huangaliwa kwa mapana yake ikiwemo pia kuoanishwa na ada gharama au tuzo inayotumika nchini kwa wakati huo. Kimsingi, gharama, ada au tozo huangaliwa kabla ya Serikali kutia saini mikataba hiyo kwa kuzingatia maslahi ya taifa na kuangalia uwezo wa wananchi.

(b)Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa makampuni hufanywa na sekta husika kwa mujibu wa Sheria taratibu na kanuni zinazohusu sekta hiyo. Kwa mfano, katika Sekta ya Madini, Wizara ya Nishati na Madini ndio yenyeye mamlaka na wajibu kwa niaba ya Serikali kusimamia kampuni husika ili kuhakikisha kuwa zinatekeleza wajibu wake kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya Madini Na. 14 ya mwaka 2010. Sekta ya Mawasiliano husimamiwa na Wizara ya Mawasiliano, Sekta ya Maliasilia husimamiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii. Hao ndio wasimamizi na wafuatilaji wa mikataba hiyo kama inatekelezwa ipasavyo.

**MHE. FAKI HAJI MAKAME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusu yako, pamoja na majibu mazuri yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria naomba nimwulize maswali mawili madogo yafuatayo:-

Pale IMTU au Herbert Kairuki kama mifano y huduma za jamii watoto wa wakulima mara nyingi wanalamika kwamba wanapata taabu sana kulipa kwa kufuata dola na kwa kufuata dola inavyopanda na kwamba wanashindwa kulipia gharama za masomo ipasavyo na kwa mara kadhaa imekuwa inawadhalilisha kwa sababu wanashindwa kusoma hawajalipa na hawaingii darasani.

Sasa hizi gharama ni kubwa je, Serikali haioni kwamba umefika wakati wa kuachana kabisa na mtindo wa kusaini mikataba ambayo inasisitiza dola au sarafu ya kigeni na kuwadhalilisha wananchi?

Pili, hii mikataba ya dola hasa ya kimarekani ambayo inatiwa saini pale. Serikali haioni kuwa yaweza kuwa ni cheche ya kuweza kuwashaa moto wa migomo?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mikataba mbalimbali kutozwa kwa dola. Hiyo kama Serikali tuna discourage ni vyema mara nyingi ikatumika fedha yetu shilingi badala ya kutumia dola na hata katika hotel mbalimbali ni vyema na ni busara ikatumika shilingi yetu.

Kwa hiyo, suala la IMTU linashughulikiwa na Serikali kwa upana wake, tunaangalia ni jinsi gani tunaweza tukawasakiida wale wanafunzi wa IMTU.

Saula la kuchochea migomo. Migomo inachochewa na sababu mbalimbali sio suala la dola peke yake. Kwa hiyo suala la migomo sio suala jema na si suala zuri. Ni vyema watu tukamaliza matatizo yetu kwa njia ya maelewano badala ya njia ya migomo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa kweli muda si rafiki. Swali linalofuata litaulizwa na Mheshimiwa Moses Machali.

**Miradi ya Umwagiliaji – Rungwe Mpya**

**MHE. MOSES J. MACHALI** aliuliza:-

Mradi wa Kilimo cha Umwagiliaji wa Kijiji cha Rungwe Mpya, Wilayani Kasulu unabomoka hata kabla ya kukamilika na kutumika.

Je, Serikali inachukua hatua gani dhidi ya Makandarasi na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu kwa kushindwa kujenga mifereji imara na kusababisha mifereji kubomoka?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Moses Joseph Machali, Mbunge wa Kasulu Mjini, napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Umwagiliaji wa Rungwe Mpya ulikumbwa na mafuriko makubwa tarehe 14/01/2010 na 15/01/2010 baada ya mvua nyingi kunyesha katika vyanzo (*Catchment Areas*) vya Mto Nyamongo katika vijiji vya Bugaga, Rusesa, Nkundutsi, Muze, Kasangezi, Kigembe na Muhanga. Katika kipindi hicho cha siku mbili maji yalongezeka na kufikia kiwango cha juu na kuharibu mfereji mkuu. Mafuriko haya yalielezwa na wanakijiji cha Rungwe Mpya kuwa yanafanana na yaliyoonekana hapo mwaka 1998 (wakati wa *El-Nino*) na 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa maelezo hayo mafupi, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Moses Joseph Machali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 4/10/2011 mimi mwenyewe nilifanya ziara katika mradi wa Umwagiliaji wa Rungwe Mpya nikifuatana na Mheshimiwa Agripina Buyogera, Mbunge wa Kasulu Vijiji, alikuwepo pia Mheshimiwa Josephine Genzabuke Mbunge wa Viti Maalum, ambapo nilikagua kazi ya marekebisho iliyokwishafanywa na kujiona juhudzi za wakulima wa mpunga katika mradi huo. Nawapongeza sana wakulima wa Rungwe Mpya kwa kazi walioianza na Serikali itaendelea kuwaunga mkono kwa kuboresha mradi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mafuriko ni janga la asili hivyo kama yalivyo majanga mengine ya asili yanaweza kupita kwa usalama au yakaacha madhara. Mradi wa Rungwe Mpya ulidhurika katika eneo la mita 59 kati ya mita 685 za mfereji mkuu. Mkataba wa ujenzi unatambua hata yasiyotarajiwa kama *forces majeure* na yanashughulikiwa chini ya kifungu cha *Employer's Risks* ambapo Mkandarasi na Mwajiri wanachangia gharama za uharibifu, kulingana na tathmini iliyofanywa. Kazi ya kurekebisha uharibifu huu tayari ilishafanywa na ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kasulu baada ya kuripotiwa kwenye kitengo cha maafa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo katika tukio hili hakuna wa kuwajibishwa maana mafuriko hayakuletwa na Mkurugenzi wa Halmashauri au mtu ye yote bali ni janga la kawaida.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali madogo mawili ya nyongeza. Moja sijaridhishwa na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Hii ni kwa sababu nimefika katika eneo hilo mara kadhaa na kujiona. Ukweli ni kwamba mradi ule ulionekana kujengwa chini ya kiwango kwa sababu mafuriko ambayo yamekuwa yakijitokeza katika mto ule ni suala la kawaida na laiti kama saruji iliyotumika ingewekwa ya kutosha kusingetokea matatizo ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri anatueleza. Kwa hiyo, kuna uwerekano mkubwa katika maeneo yale saruji iliyotumika au mradi ulijengwa kwa kiwango cha chini. Mimi nimwombe Mheshimiwa Waziri akubaliane tufanye uchunguzi juu ya hilli. Sasa sijui kama Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari tuweze kushirikiana twende kuangalia?

Swali la pili, ametuambia kwamba imebidi wafanye kuchangia gharama kutokana na mafuriko yaliyoweza kujitokeza. Naomba njue Serikali imechangia shilingi ngapi na yule mkandarasi aliyefanya kazi ya ujenzi amechangia kiasi gani?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Mheshimiwa Machali nilishazungumza naye suala hili huko nyuma nami nikamwahidi kwamba ningetembea kuona mradi ule. Napenda tu Mheshimiwa Machali kwanza tujenge tabia ya kuuliza wataalam wanaofanya kazi hizi. Mradi ule unapojengwa wahandisi ndiyo wanaoandika *certificate* kwamba tumefikia hapa sasa mkandarasi alipwe. Sasa kama yametokea mafuliko yakaharibu vilevile wataalam wanakwenda kukagua kuangalia *extend ya damage*. Sasa kama bado Mheshimiwa Machali haridhiki na anasema ulijengwa chini ya kiwango lazima kuwe na ushahidi huo wa kitaalam chini ya kiwango, kiwango ni kipi? Kitaalam wametoa viwango ambavyo vilitumika pale. Lakini mpaka hivi sasa hatujaletewa malalamiko yoyote kwamba *damage* ilitokana na kujengwa chini ya kiwango; na kweli nilipopita juzi nimekuta marekebisho yamefanyika na mradi sasa unaendelea kuzalisha. Mimi nafikiri ni vizuri Mheshimiwa Machali tuendelee sasa kuboresha mradi ule badala ya kufikiria kufukua maiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuchangia naomba niseme sina *figure* sasa lakini nasema inapotokea *forces majeure* kama hiyo si tatizo la mkandarasi si tatizo la mwajiri lazima pande zote mbili tunakaa pamoja kuchangia. Lakini kwa sasa sina *figure* kamili kwamba Serikali imechangia kiasi gani.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba mtanisamehe tatizo ni muda jamani na napenda sana maswali yaulizwe. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Juma Nkamia Mbunge wa Kondoa Kusini.

Na. 52

#### **Wananchi Walionyang'anywa Mashamba Kiteto**

**MHE. JUMA S. NKAMIA** aliuliza:-

Kilimo ni msingi wa mtaji kwa wananchi walio wengi nchini ambao wanategemea kilimo kukimu maisha yao. Lakini licha ya ukweli huo wananchi wa vijiji vya Mlongia, Itolwa, Jangalo, Chuvuku na Mrijo Wilayani Kondoa wamekuwa wakinyang'anywa mashamba yao yaliyoko Wilayani Kiteto Mkao wa Manyara jambo ambalo Serikali inalifahamu. Je, Serikali inatoa tamko gani juu ya tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** aliuliza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Selemani Nkamia, Mbunge wa Kondoa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vijiji vya Wilaya ya Kiteto asilimia 80 ya vijiji tayari vina mipango ya matumizi bora ya ardhi, vikiwemo vijiji vyote vinavyopakana na Wilaya ya Kondoa ambavyo ni katikati, Mwitikira, Njoro, Kiperesa na Ilkiushibor. Katika mipango ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji hivyo, maeneo yake yamehuishwa kwa shughuli za malisho ya Mifugo, maeneo ya wanyamapori (WMA) na maeneo ya makazi na kilimo. Aidha, mwananchi yeyote anayetaka kuanzisha shughuli za uzalishaji mali au makazi anatakiwa awasiliane na Serikali ya kijiji husika na kuzingatia Sheria ya Ardhi ya vijiji Na. 5 ya mwaka 1999.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa ya mwezi Juni 2011, jumla ya wakulima 125 kutoka vijiji vya Wilaya ya Kondoa wallingia katika kijiji cha Katikati kilichopo Wilaya ya Kiteto na kuanza kufyeka misitu na kuchoma moto kwa nia ya kuanzisha mashamba mapya pamoja na makazi katika maeneo yaliyotengwa kwa shughuli za malisho na hifadhi ya wanyamapori bila ridhaa ya kijiji husika.

Aidha, Wakuu wa Wilaya ya Kiteto na Kondoa katika mukutano wa ujirani mwema uliofanyika katika kijiji cha Katikati tarehe 6 Juni, 2011 ulioshirikisha pia wananchi wa vijiji vya Mlongia na Itolwa Ulibaini uvamizi wa maeneo ya vijiji vya wafugaji toka kwa wakulima bila kufuata utaratibu.

Mkutano huo uliazimia kuwa wale wote walioingia au kuvamia maeneo yasiyokusudiwa kwa kilimo waondolewe mara moja. Vile vile wale wote walioingia kijiji kwa kufuata utaratibu wa sheria wasibughudhiwe na wahesabike kama wanakijiji halali wa kijiji husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetafakari mgogoro uliopo katika maeneo haya na baada ya kutafakari jambo hili, Wizara yangu imeona ni busara sasa kushirikisha Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na TAMISEMI kupata suluhu ya mgogoro wa ardhi uliopo ili wananchi wa pande zote mbili yaani Kondo na Kiteto wawewe kuendelea na shughuli za kilimo bila bughudha. Tayari nimeziomba Wizara na Mamlaka zote zinazohusika kushughulikia mgogoro huu. (*Makof*)

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri. Lakini tatizo hili ni la muda mrefu sana na kila mara Serikali imekuwa ikihidi kutafuta suluhu ya tatizo hili. Mheshimiwa Rais alipokuja wakati wa kampeni aliahidi kwamba wananchi 75 walionyang'anywa mashamba yao yaliyopo Kiteto yarejeshewe mashamba yale. Lakini leo Naibu Waziri anasema bado anaendelea kutafakari kutafuta suluhu ya jambo hili. Lini?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kama niliviyotangulia kusema niliwahi kuzungumza suala hili na Mheshimiwa Nkamia pale kwenye corridor na jana mimi nimeomba Wizara ya Ardhi na tumeona kwamba ni vizuri sasa Mikoa ya Manyara na Mkoa wa Dodoma na kwa sababu tulitarajia kwamba wao wakishindwa ndiyo *waappeal*/kwenye vyombo vingine.

Sasa tunaona kwamba ni vizuri tuingilie kabisa tuwaombe mikoa hii ya Manyara na Dodoma na Wilaya husika na Wizara hizi tulizozitaja tukae kwa pamoja tuhakikishe kwamba sasa tatizo hili linapata suluhu kwa sababu wakilima kubughudhiwa hata ujasiriamali unakuwa unapungua. Naomba nimhakikishie kwamba sasa litashughulikiwa kabisa kwa nguvu zote, nimeshawasiliana na mamlaka zote zinazohusika.

Na. 53

#### Kuchelewa kwa Mradi wa Maji wa Benki ya Dunia – Njombe Kaskazini

**MHE. DKT. BINILITH S. MAHENGE (K.n.y. MHE. DEO K. SANGA)** aliuliza:-

Wananchi wa vijiji vya Kata za Lupembe Ikondo, Matembwe, Kindandilo na Mahongole katika Jimbo la Njombe Kaskazini walichangia fedha kwa ajili ya Mradi wa Maji wa Benki ya Dunia, lakini bado miradi hiyo hajaaanza kutekelezwa:-

(a)Je, ni kwa nini miradi hiyo imechelewa wakati wananchi tayari wameshachanga fedha na ziko Benki?

(b)Ni lini sasa utekelezaji wa Mradi huo utaanza ili kuondoa kero ya maji katika vijiji hivyo?-

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Jimbo la Njombe Kaskazini, lenye sehemu a na b kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijiji ulichelewa kutokana na ukosefu wa uzoefu wa kuandaa mchakato wa manunuzi katika Halmashauri. Wataalam wengi katika Halmashauri za Wilaya hawakuwa na uzoefu wa kuandaa mchakato wa manunuzi ya wataalam washauri kutokana na vigezo viliviyowekwa na Benki ya Dunia. Pia upo uhaba wa wataalam washauri nchini hivyo kusababisha usumbufu kwa baadhi ya Halmashauri kukosa idadi iliyotakiwa hivyo kulazimika kurudia mchakato wa manunuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijiji ilianza kutekelezwa mwezi Julai, 2007 katika Halmashauri zote nchini. Katika miaka miwili ya kwanza

Serikali ilianza Programu kwa kukarabati na kujenga miradi yenyе kuleta matokeo ya haraka huku ikiendelea na taratibu za manunuzi ya wataalam washauri kwa ajili ya miradi ya vijiji kumi (10).

Katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe Miradi iliyokarabatiwa ni Idunda, Lilombwi, Ibiki, Mtila, Lulanzi, Wang'ing'ombe na Mahombola. Jumla ya shilingi 333,764,000/- zilitumika kutekeleza miradi hiyo na watu 31,057 walinufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtaalam mshauri kwa ajili ya mradi wa vijiji 10 aliajiriwa mwezi Julai, 2009 na tayari amekamilisha usanifu wa miradi ya maji na kuandaa zabuni kwa ajili ya kumwajiri mkandarasi wa kujenga miundombinu.

Tarehe 10 Septembra, 2011 Halmashauri ilitangaza zabuni na ujenzi unatarajiwa kuanza Januari, 2012. Katika mwaka wa fedha 2011/2012 Halmashauri ya Wilaya ya Njombe imetengewa shilingi milioni 656 ambazo zitatumika kutekeleza miradi kwa vijiji vya Ihang'na Kata ya Lupembe, Image Kata ya Kidegembye na Kifumbe Kata ya Mahongole. Miradi katika Kata zilizobaki za Ikondo, Matembwe Kindandilo na vijiji vingine vitakavyobaki itatekelezwa katika Awamu ya Pili ya Programu. (*Makofii*)

**MHE. DKT. BINILITH S. MAHENGЕ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu aliyoyatoo Mheshimiwa Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba moja ya vikwazo vinavyochelewesha Miradi hii ya Maji ya Benki ya Dunia ni mchakato mrefu, kukosa wataalam na vikao vingi vinavyofanywa katika Wilaya, Mkoa na Kitaifa na hivyo kuchelewesha Mradi mzima uweze kuanza. Je, ni mkakati gani Wizara yake imeuweka ili kupunguza urasimu huu wa maamuzi na kuona kama wataalam wanapatikana?

(ii) Kwa kuwa kutoptana na matatizo ya fedha, Wilaya ya Makete ilipunguziwa Miradi katika Vijiji kumi kufikia sita, lakini bado ikaonekana fedha hazitoshi, ikabakiza Miradi minne ya Vijiji vya Mpangala, Matamba, Mbela na Ubinuko; na kwa kuwa kwa kutumia barua ya tarehe 26 Aprili, ambayo Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji alimwandikia *RAS* wa Mkoa wa Iringa amtaarifu Mkurugenzi wa Makete kwamba wameridhika na usanifu na uandaaji wa zabuni na hivyo waendelee kutangaza ile *tender* iliyotangazwa na Wananchi watajulishwa na wazabuni watapatikana:-

Cha kushangaza, nimekutana na Mhandisi Wizara ya Maji akihaha kutafuta zile fedha akiambiwa kwamba, kutoka vijiji vinne vinapunguzwa vinakuwa vitatu. Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kufuatilia kuona hili halitokei ili tusiwakatishe tamaa Wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kweli katika utekelezaji wa Miradi hii ya Vijiji Kumi, changamoto kubwa tulionayo ni wataalam. Wataalam siyo tu wale walioko ndani ya Halmashauri, pia wataalam ambao wanaweza kufanya kazi za uelekezi. Kwa hiyo, nchi nzima ilitangaza *tender* kwa wakati mmoja, sasa hao wataalam waliopo maana kila Wilaya watu wanachagua Wilaya wanazotaka kwenda, kwa hiyo, kuna baadhi ya Wilaya watu hawakwenda kabisa. Kulingana na Sheria ya Manunuzi ya *World Bank* ni lazima kuwe na *competition*, kuwe na angalau wataalam wawili au watatu walioomba kazi katika Wilaya ile.

Pili, kuna Wataalam wa Halmashauri ambao kuna vigezo vya kuweza kuangalia namna gani unachagua Mtaalam Mwelekezi, walikuwa hawana hiyo *capacity*. Sasa Programu imekuwa inaendelea kujenga *capacity* katika kila Wilaya. Sasa hivi kila Wilaya imeweza kufanya kazi hiyo na wameshaelewa na ndiyo maana kila Wilaya imeshakuwa na Mtaalam Mshauri. Sasa hiyo ni hatua moja. Hatua ya pili ni kwamba, Mheshimiwa Dkt. mwanzo uliambiwa utangaze Vijiji vinne, lakini baadaye tukakwambia viwe vitatu; hii imetokea baada ya kutangaza *tender* na baada ya kufungua, ikaonekana kwamba mahitaji ya kuweza kutekeleza Vijiji vinne, fedha zile hazipo na ndiyo maana tukasema toeni *tender* kwa Vijiji vitatu. Hii haina maana kwamba, hicho Kijiji kingine hatutafanya. Tunaendelea kutafuta uwezo wa fedha zaidi ili na Kijiji cha nne na vingine vilivyobaki tuweze kutekeleza katika Awamu ya Pili ya Programu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda umekuwa si rafiki kwetu, pamoja na kujitahidi bado maswali mawili yamebaki. Tatizo ni maswali marefu na majibu marefu na ukitaka kuwa na huruma huruma hapa kidogo, basi lazima utashindwa kumaliza maswali yote.

Ninayo matangazo ya shughuli mbalimbali na ya wageni. Tunao wageni waliopo kwa ajili ya mafunzo, nao ni wanafunzi 36 kutoka Chuo Kikuu cha Sebastian Kolowa – Tanga, pia ni Wanachama wa Chama cha Wanafunzi Wanaosoma Kiswahili Afrika Mashariki (CHAWAKAMA).

Wanafunzi 36 kutoka Tanga; kama mpo mnaweza kusimama. Bila shaka mmeona tunavyofanya kazi yetu. Karibuni sana.

Tunao pia wanafunzi watano kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM). Karibuni sana. (*Makofii*)

Tunao wageni 15 kutoka *Perfect Fighting Tanzania (PFT)*, wanaosimamia VICOBA Wilaya ya Temeke. Karibuni sana na sisi tunataka VICOBA vifike kwenye Majimbo yetu. Tunawakaribisha sana.

Tunao wanafunzi 31 kutoka Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijiini – Dodoma. Chuo cha Mipango, karibuni sana. Ninyi ndiyo wataalam wa kupanga mambo yetu ya vijijiini. Tunawakaribisheni sana.

Tunao wageni 56 kutoka Asasi ya Kiraia ya *Youth Empowerment and Support* ya Dodoma. Bila shaka watakuwa wapo *basement*. Karibuni.

Pia tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Wapo wageni tisa wa Mheshimiwa Angella Kairuki, amba ni Wajumbe wa UWT Mkoa wa Dar es Salaam. Karibuni sana kutoka Dar es Salaam.

Tunao wageni wa Mheshimiwa Shekifu, Mbunge wa Jimbo la Lushoto, nao ni wanafunzi 32 kutoka Chuo Kikuu cha SEKUCO – Lushoto. Aaah, ni wale wale; ndiyo SEKUCO huku mmesema ndiyo kifupi cha ile Sebastian. Karibuni sana.

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Abdul Rajab Mteketa, Mbunge wa Kilombero, kutoka Jimboni, akiwemo Diwani wa Kata ya Sanje na Mwenyekiti wa Kijiji cha Msolwa. Karibuni sana.

Sasa matangazo ya kazi; Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kuwa, leo tarehe 11, saa 7.00 mchana, kutakuwa na Kikao cha Kamati kitakachofanyika katika Ukumbi wa Pius Msekwa, saa saba kamili mchana.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa James Lembeli, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuwa, leo tarehe 11, mara baada ya Kipindi cha Maswali ya Bunge, kutakuwa na Kikao cha Kamati kitakachofanyika katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Wajumbe wote mnaombwa kuhuduria bila kukosa. Hawa wana kazi ya Muswada.

Mheshimiwa Pindi Chana, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuwa, kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo leo baada ya maswali katika Ukumbi Namba 231, uliopo Ghorofa ya Pili, Jengo la Utawala.

Kaimu DAP, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kwamba, Sekretarieti ya Maadili imeleta fomu za maadili ambazo Wabunge wanatakiwa kuzijaza kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya Mwaka 2003. Anaomba Waheshimiwa Wabunge, wazichukue fomu hizo kwa Sekretari wa Katibu wa Bunge ili wazijaze na kuzirejesha kabla ya kuondoka. Hizi ni fomu muhimu sana. Usipojaza, unaweza kupoteza nafasi yako ya Ubunge.

Mheshimiwa Jenista Mhagama, Katibu wa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, anaomba niwatangazie Wabunge wote wa CCM kuwa, leo kutakuwa na Kikao cha Chama, saa saba mchana, Ukumbi wa Pius Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo yalikuwa matangazo kwa siku ya leo.

### **MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

#### **Muswada wa Sheria ya Manunuzi ya Umma wa Mwaka 2011 (The Public Procurement Bill, 2011)**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Ninaomba nimtaje mchangiaji atakayeanza na atakayefuatia, baadaye nitataja orodha ndefu kidogo. Atakayeanza kuchangia atakuwa Mheshimiwa Rosweeter Kasikila, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed na baadaye nitawataja wengine watakaofuatia.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninataka kuomba mwongozo wako kuhusiana na jambo ambalo lilipita muda mfupi uliopita wakati wa kipindi cha maswali na majibu. Wakati Naibu Waziri...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, Kanuni gani?

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Naibu Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki anajibu swali namba 45 la Mheshimiwa Hussein Mzee, katika majibu yake kuhusiana na Miradi ambayo inaendelezwa na Afrika Mashariki kwa upande wa Zanzibar, alitaja suala la utafutaji ufadhili kwa ajili ya Uwanja wa Ndege Pemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia kwa Waziri wake wa Miundombinu, Mheshimiwa Hamad Masoud Hamad, Mwakilishi wa Jimbo la Ole, imetoe taarifa ya kwamba, sasa hivi Serikali ipo katika mchakato wa kusaini Mradi huu wa Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba na Uturuki. Taarifa ambayo imetolewa na Naibu Waziri hapa na mara nyingi amekuwa anairudia ni kwamba, wao wanautafutia ufadhili Uwanja wa Ndege wa Pemba. Tunachoju, Pemba kuna uwanja mmoja wa ndege wa Karume. Je, huu ambao unatafutiwa ufadhili na Jumuuya ya Afrika Mashariki kupitia Wizara hii ya Afrika Mashariki ni upi? Ninaomba mwongozo wako ili kusitokee mgongano wa kitaarifa baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Wizara ya Jumuuya ya Afrika Mashariki kupitia Serikali ya Muungano.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, sipati tabu sana katika kutoa mwongozo huu, pengine sioni kama ni vibaya kuwa na mipango miwili katika jambo moja; ni hatua nzuri tu na si vibaya. Kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Muungano wanafanya kazi kwa pamoja, ninadhani ni haja tu ya kuwatahadharisha kwamba wawasiliane, waweze kuona ni mpango upi ambao utakuwa *implemented* katika wakati husika. Sasa kama kuna mipango miwili, mimi sioni kama ni hatari. Ninadhani ni jambo la kawaida, hebu tuwaachie. Mwongozo wangu ningkuomba tuwaachie na kama utapata fursa wasiliane na Waziri aliyetoa jibu hilo ili muweze kuweka vizuri. Huo ndiyo mwongozo wangu; ni ufafanuzi tu.

Basi tunaendelea. Sasa ninamwita Mheshimiwa Rosweeter Kasikila, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamad Rashid.

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa nafasi uliyonipa, niweze kuchangia kidogo kuhusu Sheria ya Manunuzi ya Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninapenda kumpongeza Waziri mwenye dhamana, Watendaji na hata Kamati waliosaidiana kufanya maboresho kwenye hii Sheria ya Manunuzi ya Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitakuwa na mengi sana ya kuzungumza, isipokuwa nitaongelea kipengele cha 65, ukurasa wa 58. Ningombua uniruhusu nisome kidogo kipengele cha (2) kinachosema: *"For the purpose of subsection (1), emergency procurement shall meet one of the following criteria:-*

- (a) *Compelling urgency that creates threat to life, health, welfare or safety of the public by reason of major natural disaster ... et cetera et cetera.*
- (b) *Situation whereby, without the urgent procurement, the continued functioning of the Government or organization would suffer irreparable loss, the preservation or protection of irreplaceable public property, or the health or safety of public will be threatened."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kipengele hiki kimeweza kuonekana kwenye hii Sheria na kimefafanua mambo kinagaubaga hasa masuala kuhusu afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninaomba Sheria hii itakapokuwa imepitishwa, basi itumike, tusiwe watu wa kuitisha sheria, halafu tunaziweka kabatini tu au kwenye shelves bila kuzitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kuzungumzia kwamba, hii *emergency procurement* hapa imeonekana ni lazima iwe ni *emergency procurement in a real sense*. Kwa mfano, hospitali tunakuwa na makabati ya kutunzia dawa za dharura, kwa sababu bila dawa za dharura, wagonjwa wengi wanapoteza maisha yao. Mfano, mgonjwa anaweza akaja hospitali yuko kwenye comma, hamuwezi kujua anaumwa nini au apewe dawa gani mpaka apimwe kwanza. Utakuta dawa, labda kama vitendanishi hakuna au mama mjamzito anakuja ana *very high blood pressure* karibu anaingia kwenye kifafa cha mimba, lakini dawa za kupunguza ile *BP* hamna. Mtoto anakuja ana degedege, dawa hakuna na dawa nyngi za aina hiyo zinakuwa hazipo labda *cotton* na *gloves* kwa ajili ya kutumia labda kumzalisha mama. Vifaa hivi vinakuwa havipo, kwa sababu mara nyngi tumeagiza *MSD* na tumeambiwa kuwa hakuna (*out of stock*).

Sasa basi, vifaa vinapokuwa havipo *MSD*, kwa sababu moja au nyngine, hizi dawa na vifaa inapofika wakati sasa lazima viagizwe kwa dharura, taratibu za manunuzi zinazotumika, zinachukua muda mrefu sana. Maombi yanaweza yakapelekwa kwa Halmashauri, lakini mpaka *PMU* ikae, Bodii zikae na mara nyngine vikao havikai; mgonjwa amekuja hospitali anaumwa, lakini dawa hakuna. Huko ambako lazima zikanunuliwe, taratibu zinakuwa ndefu sana. Kwa hiyo, inakuwa inaleta *effect* sana. Vifo vingi vya watoto chini ya miaka mitano vinatokea kwa sababu pengine taratibu za manunuzi zinakwenda pole pole sana. Vifo vingi sana vya wajawazito vinatokea kwa sababu taratibu za manunuzi zinakwenda pole pole sana. Kwa hiyo, ninaomba hii *emergency procurement* ichukuliwe kwamba ni suala la dharura kweli kweli. Isije ikawa sheria imetoa nafasi ya kufanya manunuzi kwa dharura, lakini ile dharura inakuwa haitiliwi maanani, matokeo yake watu wanapoteza maisha.

Mara nyngi tumewashuhudia wauguzi hospitalini wanamwambia mama utakapokuwa unajifungua au umekaribia kujifungua, uje na dawa ya kukata damu, yaani kusitisha *bleeding*, uje na sindano, uzi wa kushonea na *gloves pair* kadhaa. Hii ni kwa sababu ya kutaka kumsaidia mgonjwa asipoteze maisha kwa sababu *MSD* dawa na vifaa vinakuwa ni *out of stock*. Pia vinakuwa vimeombwa kununuliwa kwenye maduka binafsi, zile taratibu za manunuzi zinakwenda pole pole sana na mgonjwa anapokuja hospitali hawezu kusubiri mpaka taratibu za manunuzi zitakapokamilika au dawa zitakaponunuliwa. Hakuna mgonjwa anayekuja na *very high blood pressure* akakaa mwezi mzima anasubiri dawa inunuliwe. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninatoa rai kwamba, tunaposema manunuzi ya dharura, yawe ni ya dharura kweli kweli. Tunaomba Halmashauri, wanapokuwa wamepelekewa

maombi au vifaa tiba kununuliwa, zitumike taratibu ambazo zitawezesha dawa hizi au vifaa hivi kupatikana ili wagonjwa wasiendelee kupata shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Sera nzuri ambayo imekuwa ikiongelewa asubuhi hapa ya wazee, wajawazito na watoto kusamehewa matibabu ni nzuri sana. Serikali imewasaidia watu hawa, lakini utakuta mara nyingi haifanyi kazi kwa sababu madawa hayapo MSD, lakini hata kwenye manunuzi inachukua muda mrefu sana, kwa hiyo, utaona mzee anaandikiwa akanunue dawa dukani. Mtoto mchanga amekuja anaumwa anaamibiwa nendeni mkanunue dawa. Kwa hiyo, utakuta hata hawa Wananchi hawafaidiki na hiyo *benefit* ambayo Serikali imewapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninaomba japo kuna huu utaratibu wa Sheria ya Manunuzi, *emergency procurement* ambazo siyo ngumu sana, dawa zinapokuwa zimekosekana zikienda kununuliwa zisichukue siku moja au mbili zipatikane ili hospitali zetu na vituo vya afya viweze kuhakikisha kwamba, makabati yana dawa hizi za dharura wakati wote, kusiwe hata na wakati fulani eti dawa hazipo kabatini. Tunawapa Wananchi shida, lakini pia tunawapa Wafanyakazi wa Hospitali shida maana hakuna anayewaelewa, sana sana watu wataamibiwa ni wazembe, lakini wanajitahidi hakuna kinachofanyika. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninatoa rai yangu hiyo kwamba, kama ni *emergency* basi iwe ni *emergency* kweli, isibaki tu kwenye sheria. Hayo yalikuwa ni masuala ya hospitali kwa ufupi, lakini jana wenzangu wamezungumzia sana kuhusu manunuzi ya mitambo au vifaa viliviyotumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *there is no way*, inapobidi kununua vifaa viliviyotumika vitanunuliwa tu. Kifaa kinapokuwa kimetumika siyo kibaya, inategemea kimetumika kwa muda gani. Ninamwomba Waziri atueleze kama wameweka vigezo kusema kifaa kilichotumika kinachotakiwa kununuliwa labda kiwe kimetumika miezi sita au mwaka baada ya *manufacturing date*. Kimetengenezwa lini na kiwe kimetumiwa kwa muda huu, uwe ni muda mfupi; *other wise*, tutatoa *loophole* ya watu kwenda kununua vifaa au mitambo ambayo imetumika lakini inakaribia kuchakaa kwa sababu tu hatukuweka *limitations*. Ingekuwa ni mahindi au maharagwe, tungenesema chukueni mzani mkapime kama kilo imetimia iwe kilo isiwe nusu kilo. Sasa tunawategemea wataalam watakoatumwa kwenda kununua vifaa hivi angalau watumie busara na wawe waaminifu, wanunue vifaa ambavyo wameelekeza kwamba vinahitajika viwe katika muda huu na kweli visiwe vile ambavyo vinaelekea kuchakaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema ni kwamba, watu tubadilike tabia tuweze kununua vitu ambavyo tumepanga wote, kwa sababu jana tulikuwa tunasema Mwenyekiti tu kusaini peke yake haitatosha, linaweza likakaa jopo hapo likasaini lakini anayetumwa kwenda kununua akaenda kununua vitu vingine ambavyo wala hakutumwa. Haya yote pamoja na sheria, lakini pia kitu cha kwanza ni uaminifu na uadilifu ndiyo tuuweke mbele, watu na sisi tuwe na mabadiliko ya tabia. Tumeona hata nchi inatuhinda akili, kila siku tunasema mabadiliko ya tabia nchi hata nchi inabadilika kwa nini wanadamu tusibadilike?

Mtu anapokuwa amepewa dhamana kwa niaba ya Wananchi, fanya kwa uaminifu ulete vyombo ambavyo vikija havitakuwa *hazard* kwa Wananchi; tusianze tena kushuhudia kichwa cha treni kinapandisha mlima kidogo kina-fail kinaanza kurudi nyuma, mkiuliza mnaamibiwa ni chombo kilichonunuliwa miezi miwili iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa rai yangu kwa ufupi kwamba, pamoja na mambo yote, manunuzi yote ya nje ya vyombo vikubwa na vidogo vya maofisini hata *stepplers* tununue zile ambazo zitawesaidia Wananchi na ambavyo havitaleta madhara kwa Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yangu machache ni hayo, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Rosweeter, kwa kutumia muda vizuri, sasa nitamwita Mhehsimiwa Hamad Rashid Mohamed na baadaye atafuatiwa na Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya pili kuzungumzia Muswada huu muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nieleze kwamba, kwa uzoefu wangu mdogo, huko tulikotoka magari *second hand* ndiyo tulikuwa tukipanda Mawaziri. Mwaka 1982, gari la kwanza nililopanda mimi ilikuwa *Peugeot 504*, tulinunua *State Motors Corporation*, ilikuwa la Balozi mmoja akalileta pale basi tukaambiwa tununue ndiyo Waziri apande. Kitu kikubwa kilichokuwepo ni uadilifu, uaminifu na kwamba, Serikali ilikuwa ina matatizo ya fedha za kigeni, kwa hiyo, ikahakikisha kwamba angalau kile kilichokuwepo kinatumika vizuri. Vilevile ninakumbuka *Air Tanzania* iliwahi kununua ndege mbovu kwa George Halack, ilimgharimu Waziri wake na Mkurugenzi wa ATC haraka sana; sasa tatizo liko wapi sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la kwanza ni kwamba, uadilifu umepungua, uzalendo haupo, kwa hiyo, kila tunachokifanya sasa tumekuwa na mashaka na ndiyo maana hata Kamati yetu ikawa na wasiwasi sana katika kifungu cha 65 juu ya kuiruhusu Serikali kununua mitambo ambayo tayari imeshatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalisema hili kwa sababu asilimia 55 ya manunuzi yanaharibika kutokana na watu kutosimamia sheria vizuri. Kwa mujibu wa *Auditors Report*, kati ya asilimia 55 ya manunuzi yetu, asilimia mia moja ni Miradi ya Maendeleo na asilimia sabini kwenye *Recurrent Budget*. Sasa kuwa na asilimia 55 ya kutokusimamia sheria katika *magnitude* ya triloni za pesa ni dhahiri kwamba, tuna tatizo la msingi na ndiyo maana wasiwasi ukawa mkubwa kwamba, tunapotoa mwanya wa kuruhusu manunuzi ambayo yanaweza yakaathiri usimamizi ...

(*Hapa kengele illilia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha*)

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Eeh! Nilidhani dakika kumi zimekwisha!

**MWENYEKITI:** Hapana, ninadhani atairekebisha vizuri.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Tatizo la msingi la kwanza ningetaka kujua kutoka Serikalini kwa nini hakuna matumizi mazuri na usimamizi wa sheria unakuwa mbovu siku hadi siku? Asilimia hamsini na tano ya Sheria ya Manunuzi haisimamiwi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na sheria nzuri tunayoitunga hivi sasa, kama utekelezaji wake na usimamizi wake una upungufu wa asilimia 55, bado hatujakidhi mahitaji halisi ya Sheria hii ya Manunuzi, tukitilia maanani kwamba, asilimia mia moja ya manunuzi ni maendeleo na asilimia sabini ni kwenye matumizi ya kawaida. Huo ndiyo wasiwasi wa kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, kazi yetu ya kwanza kwa Serikali ni kuhakikisha namna gani inasimamia kwa ukamilifu matumizi ya sheria hii. Dawa yake ni moja tu; inapotokea kosa wanaohusika wachukuliwe hatua mara moja. Nilielezea hapa manunuzi ya ndege ya Tanzania kwa George Halack, *immediately*, ndege imefika imekuwa mbovu Waziri na Mkurugenzi walipoteza kazi, leo watu wanavuruga mali za umma hakuna anyeshughulikiwa; huu ndiyo wasiwasi mkubwa! (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaeleweka kabisa kwamba, yapo mazingira ambapo Serikali inalazimika kununua vifaa viliviyotumika na nimetao mfano leo asubuhi. Tumeingia kwenye vita, ghafla vita vimetokea tumeishiwa silaha, ukienda kutengeneza silaha mpya haiwezekani ni lazima ukaangalie kwenye *shelves* kuna silaha kiasi gani zinaweza kukusaidia katika mapambano yako. Kwa hiyo, sheria ni lazima itoe *room* katika hilo. Sasa ni methali gani tunazitumia ili kulinda rushwa ndani yake na ili kulinda ufisadi ndani yake, ndiyo jambo la msingi; na ndiyo maana hata kwenye Kamati tuliangalia kwamba ni vizuri basi isije ikatokea kama Rais alivyotuambia, yeche hakujua mwuzaji wa Richmond ni nani!

Sasa tufike mahali ahusishwe katika kufanya maamuzi ya kusema hapa tunakubali tununue mtambo huu kutokana na matatizo halisi yaliyotokea, awe *accountable* yeche

mwenyewe. Bila ya hivyo, tutatoa mwanya wa watu kujirundikia mali kwa kununua vifaa dhaifu. Hilo ni jambo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni matumizi ya *electronic procurement*, ninashukuru sana kwamba, Serikali sasa imelisikia, tumelipigia kelele na tumelifanyia semina. Asilimia thelathini mpaka arobaini unaweza uka-save fedha kwa matumizi ya *electronic procurement* na limefanyiwa *study* kubwa sana miaka mingi. Ninachokiomba ili kupunguza rushwa, kupata ufani na kupunguza gharama za *tender*, *electronic procurement* ndiyo *solution* ya maneno haya tunayozungumza humu ndani. Kwa hiyo, hata unapotaka kununua kitu ambacho kimetumika, ukikiingiza katika utaratibu wa *electronic procurement* maana yake kila mtu ataona, atajua bei, atapata *specification* na ushindani utatokea wa wazi. Hii ni njia moja ya kupambana na hili tatizo ambalo lipo na stadi inasema imefanyika muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakumbuka wakati nikiwa Mwenyekiti wa *PAC*, tuli-conduct semina, *workshop*, tulialika wataalam kutoka Dubai na Mkurugenzi anafahamu sana jambo hilo, ninafikiri hili litasaidia kupunguza hili tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni suala la kuwaruhusu maafisa pale inapotokea amesahau kuweka kwenye *procurement plan*, basi aweze kuingiza. Katika eneo ambalo ni hatari ni hili. Anatakiwa *Procurement Manager* ye yote atengeneze bajeti ya *procurement*, tukimruhusu akisahau eti alete jambo kwa dharura, maana yake tayari tena unatoa mwanya mwingine wa mtu kusema aah tulisahau, akasahau jambo kubwa kwa makusudi akijua atapata mwanya kutokukiuka ule utaratibu. Pamoja na kwamba ile sheria imekuwa nzuri tu, lakini kwa sababu ya lile la kwanza nillolisema la *enforcement of the law*, ndiyo tatizo la msingi litakalotokea kusababisha watu wakapenyeza mambo yao ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo basi, ninashauri suala la kutengeneza *Procurement Plan* liwe *very thorough* na lipitiwe kiasi kwamba *room* ya kusahau humu ndani isionekane; hilo la kwanza.

Jambo la pili, hata kiwango kinachosahauliwa maana unaweza kusahau sindano ndogo lakini huwezi kusahau kununua ndege wala huwezi kusahau kununua kichwa cha treni na wala huwezi kusahau kununua meli. Unaweza kusahau kununua spea ya meli. Sasa *Procurement Plan* ndiyo msingi wa kuondoa tatizo tulilonalo sasa na bahati nzuri sheria tumeikubali na Waziri umeikubali kwamba miezi miwili kabla ya bajeti, *Procurement Plan* itengenezwe na wahusika. Sasa ninaomba mtile mkazo suala la elimu katika sehemu hii ili watu watengeneze *Procurement Plan* na ni vizuri sana Kamati za Bunge zinazohusika zioneshwe *Procurement Plan* zilivyo ili wajue Wizara fulani inakusudia kununua kitu gani wakati wa bajeti, kwa sababu kabla ya bajeti, miezi miwili Bunge linakaa angalau Wabunge wawe na picha ya hilo; tutapunguza hii mianya ya rushwa na watu kupenyeza mambo katikati. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema awali kwamba, dharura zinaweza kutokea, mimi ninalewa sana, bahati nzuri nimekaa Serikalini, lakini hizi dharura ni lazima zipimwe. Tumezi-generalize sana kwenye Sheria. Hivi ni kwa nini tunapata magari *second hand* kutoka Japani? Hii ni kwa sababu wao ikishafika miaka mitano, wanakuona mtu wa ajabu wewe raia kuendelea kulitumia gari hilo, sisi maskini wa Mungu tunakwenda kununua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia pekee ya kuondoa tatizo hili ni kupunguza kodi kwa vifaa vipyta. Ukienda Marekani, ukitaka kununua gari, unalipa kodi ya asilimia kumi tu basi imemalizika. Ukileta gari jipya hapa maana yake ni adhabu, kwa hiyo, tunaendelea kuwa *dumping place* hapa kwetu. Wenzetu gari likitumika kwa miaka mitano wanasema halifai liondowe, kwetu sisi ushuru wa magari mapya na vifaa vipyta ni mkubwa. Tupunguze ushuru kwenye vifaa vipyta na tuongeze ushuru kwenye vifaa vikongwe, tutapunguza haya matatizo ambayo tunayo hivi sasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa Serikali, kwanza ni kuondokana na utaratibu wa kununua vifaa vikongwe, haiwezekani nchi ikaangia kwenye matatizo, hatujaona watu wanakuja Tanzania kununua magari *second hand*. Tunakwenda Japani tunanunua magari *second hand*

kwa sababu wao kila miaka mitano ni lazima uliondoe gari au ulipeleke kwenye *scraper* tena kwa gharama zako. Vilevile tuweke mifumo ya kibenki ya kumwezesha Mtanzania kuweza kukopa kununua kitu kipyä, mifumo yetu ya fedha bado haijawawezesha Watanzania na hili ndijo tatizo ambalo ni lazima tuli-*address* tuondokane na matatizo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, nimeona Muswada umeruhusu na umetoa fursa kwa Wakandarasi wetu na wanao-*tender locally* waweze kupata fursa; ni jambo jema sana. Hapa kuna mambo mawili; jambo la kwanza kwa ndugu zetu tunapewa nafasi hii tunaitumiaje, maana tunaweza tukazungumza uzalendo lakini mtu akapewa *contract* akashindwa kuifanya, matatizo yako pale pale. Kwa hiyo, jambo la kwanza kwa Serikali ni kuyaziwezesha haya makampuni yetu ya ndani yaweze *ku-bid* hizi *tender* na wao ni lazima kwa upande wa pili wajitahidi kuona hii fursa waliyoipata wanaitumia vizuri. *It is two way traffic*, Serikali imetoa fursa na sisi tuitumie vizuri, usipewe Mradi halafu ukawa haumaliziki kwa sababu ni mzalendo, hiyo haiwezekani. Mradi umalizike, watu wapate huduma, ndijo lengo la Serikali. Kwa hiyo, ninasema ni *two way traffic*; pande zote mbili, Serikali imetoa nafasi hiyo na sisi wenywewe tunaopewa fursa hiyo ni lazima tutumie vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, ninaishauri Serikali ikiangalie sana kifungu hiki cha manunuvi ya vifaa vya *second hand*, lazima tukiangalie vizuri sana tusitoe mwanya mbaya sana. Ninafahamu katika mambo ya *Airline* haya, unaweza ukakuta ndege imetembea maili elfu moja, hiyo ndege ni mpya na ukawa na sheria inayokukataza kununua, lakini ukishaingia huko ni matatizo. Ninafikiri Serikali kama inataka kuingia katika hili, *ika-lease aircraft*, ijijengee uwezo waende wakakae na *manufacturers* waweze kupata ndege mpya. Ukinunua ndege *second hand*; maana yake nini? Maana yake kwenda kufanya *C-Check* na *D-Check* ni muda mfupi sana na hizo ni gharama kubwa, lakini ukinunua ndege mpya unachukua muda mrefu kufanya hizo cheki zinazotakiwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kidogo na mimi nimefanya mambo ya *Airline* ninafahamu, lakini inawezekana kabisa ukakuta kitu kimeshatengenezwa, hakikutengenezwa kwa *specification* zako, lakini ipo kwenye *plant* mtu kashindwa kununua, imetokea juzi hiyo. Tulikuwa tunatafuta meli tukakuta ipo moja mpya imeshatengenezwa, haipo kwenye *specification* zetu lakini ni mpya imekaa mtu kashindwa kununua, unachofanya pale ni kuangalia zile *specification* unazozitaka wewe, unaweza kuzirekebisha kiasi gani na hiyo meli ikakusaidia, bado hiyo angalau ina nafuu hajatembea. Tukienda kwa utaratibu huu tunaokwenda nao, tunaweza kupata matatizo, mimi ninashauri Serikali kama inataka kufufua *Air Tanzania, Lease Aircraft, for the time being*, kazungumzeni na *manufactures* ili mpate *line of credit* mtengeneze ndege mpya. Ukitaka kufufua *Air Tanzania, costwise* itapungua ukitumia chombo kipyä kuliko kikongwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, ninashukuru sana kwamba, sasa *Private Partnership* nayo imeingizwa katika Muswada huu; ni matumaini yangu kwamba, Serikali itaharakisha kanuni zake na kuweza kutekeleza. Ukifanya masahihisho hayo, mimi sina tatizo na Muswada huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofî*)

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninaomba nitumie muda wangu wa mwanzo kabisa, nimpongeze Waziri, Naibu Mawaziri na Watendaji wote, kwa kuuleta Muswada huu. Vilevile ninaunga mkono hoja za Kamati; ni za msingi, ninaamini Waziri atakuwa amezisikia na atazitekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, vile vile niungane na wachangiaji waliotangulia hasa kuishukuru Serikali kwa kuteremsha Sheria hii ya Ununuzi wa Umma kwenye ngazi ya Halmashauri kwa maana ya Madiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru wale wote walioshauri kwamba ni vyema basi mikataba yote iwe inaandikwa kwa Kiswahili na mimi ninaunga mkono. Vilevile ninapenda niongezee, lingine la msingi sana ni elimu. Waheshimiwa Madiwani, wapewe elimu namna ya kuitumia Sheria hii ya Ununuzi wa Umma, kwa sababu kila jambo linahitaji kuelimishwa na namna

ya kuangalia *tender* mara nyingi watu wanakuwa na mazoezi ya kuangalia yule aliye-*tender* chini bila kuangalia ufanisi na ubora wa jambo ambalo wanampa huyo mtu.

Kwa hiyo, ni vyema semina zikapelekwa kwa Waheshimiwa Madiwani, wakaelewa ni nini watakifanya katika kuangalia *tender* mbalimbali katika ngazi yao kama tulivyofanya kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati mbalimbali za Fedha, wamepewa semina mbalimbali na kila mara Bunge jipya linapoanza, semina hutolewa na hata ikifika mahali wanapewa tena. Kwa hiyo, wenzetu vilevile wapewe semina ili kuwaongeza uelewa wa kazi ambayo wanatarajia kuifanya. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya ushauri huo, ninapenda niungane na wenzangu kwamba, bado tuna kila sababu kung'ang'ania sheria ya kununua vifaa vipyta; kwa mfano, magari, mafriji, majenereta na vifaa mbalimbali. Hatuna sababu zozote wala visingizio vyovytote kulainisha sheria hii kuwaruhusu watendaji kununua vifaa vilivyochochaka kwa vitu vidogo vidogo ambavyo vipo chini ya uwezo wetu; kufanya hivyo ni kuchezea fedha za umma. Kwa kuwa kifaa kipyta kina-*guarantee*, umekinunua leo, utakitumia kwa kipindi Fulani; je, kifaa kikukuu kitakuwa na *guarantee* ya namna hiyo? (Makof)

Kwa hiyo, ninasisitiza kwamba, kwa vitu vya namna hiyo ambavyo bado vipo chini ya uwezo wa Serikali, tunang'ang'ania na sheria ya kununua vifaa, tutakuwa tumesaidia sana kulinda mali za nchi hii; bila kufanya hivyo ni kweli tutatoa mwanya wa watendaji kuendekeza kuweka cha juu. Mtu anakwenda kununua kitu ambacho hakina hata bei maalum anaweka na cha kwake hapo kwa sababu utamdhhibitili wakati vitu vilivyotumika havina bei maalum inayojulikana; bei ni makubaliano. Kwa hiyo, tutakachofanya ni njia mojawapo ya kuisaidia Serikali kulinda mali yake na kulinda uchumi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nizungumzie ununuzi wa vifaa vingine ambavyo bado viko juu ya uwezo wa Serikali. Ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, twende mbele, turudi nyuma, tukae tutafakari kazi iliyotuleta hapa ni kuisaidia Serikali kufanya yale yatakayoisaidia nchi hii kufanya yale yatakayowasaidia Watanzania. Ndugu zangu uchumi wa nchi hii bado haujaturuhusu kununua mambo makubwa; kitu kama ndege na vifaa vya kijeshi; hivi kweli nchi hii bado sasa hivi ina uwezo wa kununua meli ya kijeshi?

Ninawaomba sana, endapo tutaendelea kuibana Serikali kila kitu tununue kipyta, ninataka niwahakikishie Wabunge wenzangu watakaoweza kununua vifaa kama hivyo vipyta ni kizazi cha tatu kutokea hapa nilipo. Maana yake mimi nimzae mtoto na mtoto huyu azae mtoto na huyo mtoto azae ndiyo watakaoweza kununua hata hizo meli za kivita.

Angalieni vitu vingine vina umuhimu wake. Tunazidiwa hata na wenzetu wa nchi jirani wa Kenya na Uganda. Ninawahakikishia kama tutaendelea kuibana Serikali kwa kiwango hicho, tunaleta hatari ndani ya nchi hii. Tutapungukiwa hata na ulinzi. Siombi vita wala siombi matatizo, lakini likizuka kwa utaratibu huu watanywea chai Mwanza, siku ya pili wameshafika Singida. Kwa sababu tutakuwa hatuna vifaa vinavyoweza kupambana na matukio makubwa makubwa. Duniani hatuombi matatizo lakini yapo. Sasa kama matatizo haya yapo na kugombana kupo, lazima tuwe na tahadhari. (Makof)

Ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tuiruhusu Serikali iweze kununua vitu ambavyo bado haina uwezo wa kuvinunua vikiwa vipyta kama ndege. Mmesema meli za kivita na vichwa vya treli, Watanzania bado wanahangaika na usafiri; tutawanusuru vipi kama bado tunaibana Serikali wakati tayari imeshakiri kwamba uchumi haujaruhusu? Kinachotakiwa hapa ni kuibana Serikali kuinua uchumi na uzalishaji. Huku ni kuwabana watendaji kurudisha uzalendo kwa maana ya kulinda vite vitakavyoletwa. Kwa maana kuhakikisha wanunuwa bei ambayo ni ya uhakika waachane na tabia ya kuongeza kuweka chao hapo. Watanzania tatizo letu bado tumetanguliza maslahi binafsi badala ya kutanguliza maslahi ya nchi hii. Tufike mahali uzalendo urudi, tutangulize utaifa, tutangulize maslahi ya nchi, nina hakika kila mmoja kwa nafasi yake akiguswa kufanya hivyo, tutaisaidia nchi hii kufanikisha masuala yake. (Makof)

Ninawaomba sana Waheshimiwa Wabunge wengi wameongea wanakataa kabisa kununua vifaa *used* kwa maana viliviyotumika, lakini ujanja huo hatuna. Mganga hajigangi, lazima tukubaliane na wenzetu, wamekaa wametafakari, hawa watendaji wetu wana vichwa vizuri kabisa, wana uchungu na nchi yao, wametafakari wamefika mahali wameona hawana namna. Sasa kama hawana namna *what is next?* Lazima tukubali ilimradi tuhakikishe kwamba wawe makini katika kuangalia hivyo vitu viliviyotumika vimetumika kwa kiwango gani au vimechakaa kwa kiwango gani. Siyo tu kwa kuwa tunesema basi tununue hata kama hakina umuhimu kinunuliwe aghali. Lazima waangalie vitu vyenye maslahi, vyenye umuhimu na nchi hii.

Tuwe waaminifu na wazalendo, nina hakika tukifanya hivyo, Taifa letu litaingia kwenye historia kama nchi zingine. Nchi inakuwa haina ndege, nchi haina hata meli za kivita, nchi haina vitu vingi muhimu vyenye umuhimu wa pekee katika nchi yetu tunasema tununue kipywa kwa hela ipi? Tuwasubiri wakati wa bajeti tuwabane wanazalishaje, lazima wazalishe, watakapozalisha hapo tutakuwa na uwezo hata wa kubadilisha sheria yetu, kwa sababu kazi ya Bunge ndiyo hiyo hiyo ya kutunga na kurekebisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sikuwa na mengi ya kuzungumza, nilitaka nitoe mchango wangu huu, ninakushukuru sana na Mungu awatangulie watendaji; uaminifu mbele na utaifa mbele. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, kwa kuniachia na muda. Miongozo inaanza kuniharibia *patterns* sasa.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba mwongozo wako, kwa mujibu wa Kanuni ya 68 (7) kuhusu jambo ambalo limetokea mapema hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni muhimu kwa maslahi ya mjadala unaoendelea. Kwa muda sasa kumekuwa na *reference* inayoipongeza Serikali kwa kuingiza katika Muswada kifungu ambacho kinatoa mamlaka kwa Madiwani kuweza kusimamia taratibu za manunuzi kupitia Kamati za Fedha za Uongozi. Kauli hizi zimekuwa zikitoka jana na leo, kwa sababu ya maelezo ambayo Waziri aliyatoa wakati wa kuwasilishwa Muswada, maelezo ambayo kimsingi yalipotosha Bunge. Ukurasa wa tatu wa maelezo ya Waziri ambayo tumegawiwa inazungumzia mambo muhimu katika Muswada na ukurasa wa tano, nitanukuu kwa kifupi tu kipengele (p) kinasem, kuweka mfumo katika Kanuni za Sheria ya Ununuzi wa Umma wa Serikali za Mitaa.

**MWENYEKITI:** Hebu subiri twende kwa pamoja; kwenye hotuba gani?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Kipengele (p) kwenye Hotuba ya Waziri, ukurasa wa tano. Kuweka mfumo katika Kanuni za Sheria ya Ununuzi wa Umma wa Serikali za Mitaa, utakaowezesha Madiwani kusimamia masuala ya ununuzi katika Halmashauri kupitia Kamati ya Fedha na Mipango ili kudhibiti wizi wa fedha za umma katika Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Muswada tuliopewa, mahali pekee ambapo Serikali za Mitaa na mamlaka husika inatajwa ni kwenye ukurasa wa 35, kifungu cha 31 cha Sheria kuhusu *Tender Boards*. Ninanukuu kipengele cha tatu kinasema: *"The composition of local government authority tender board and the method of appointment of the members, and the procedures to be followed by such a tender board, shall be prescribed in Regulations made pursuant to the provisions of the Local Government Finances Act."*

Sasa ukirudi kwenye *Local Government Finances Act*, hakuna kifungu hicho ambacho kinatoa hayo mamlaka kwa Madiwani na Kamati za Fedha za Uongozi; na kwa bahati mbaya Muswada huu ulioko mbele una kifungu cha 105 ambacho kinatamka yafuatayo, ninaomba ninukuu nisipoteze muda, ukurasa 85, kifungu cha 107, kipengele cha tatu.

**MWENYEKITI:** Hebu rudia hapo umesemajé?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 85, kifungu cha 107, kipengele cha tatu; *upon the coming into operation of this Act, save for section 31(3)*, ambayo ndio ile niliyoisema awali *all laws, regulations or rules* na inaendelea kwamba kanuni/taratibu zingine zote zitaendelea.

Sasa kwa manufaa ya huu mjadala unaoendelea; ni vizuri ukatoa mwongozo ambao utawezesha Waziri kufanua maelezo aliyoatoa, ambayo yamepotosha mjadala unaoendelea kwa sababu hakuna mahali popote katika sheria hii ambapo kumetaja neno madiwani wala hakuna mahali popote kumetaja neno Kamati ya Fedha na Uongozi ila imesemwa tu kutatengenezwa kanuni kuhusiana na *tender board* na kwa *status iliyopo* sasa ya *tender board*, Kamati ya Fedha na Uongozi siyo sehemu ya *tender board*. Kwa hiyo, labda Waziri atoe ufanuzi au aseme kwamba anakusudia kuleta *schedule of amendment* kwenye eneo hilo ili mjadala wa Bunge usiendelee kupotoshwa na maelezo ambayo yalitolewa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, *concern* ya Mheshimiwa Mnyika ni dhahiri ipo wazi hapa, ukiwianisha *provision* ya hii 31(3) ambayo inasema kwa mujibu wa *Local Government Finances Act* na kule kwenye *Local Government* hajasema Sheria hairuhusu Kamati yoyote ya Madiwani kushiriki, lakini imekuwa *referred* kule. Mwongozo wangu hapa ni kwamba; ama Mheshimiwa Waziri atoe ufanuzi muda wake ukifika au tunaweza kumpa muda aka-clarify sasa; lakini ili uwe na uhakika na mwongozo wangu Mheshimiwa John Mnyika na wewe pia uandae *schedule of amendment* ili wakati wa Kamati ya Bunge Zima, tuweze kuona namna tunavyoweza kuingiza kuliko tukikaa tu hivi hivi tunaweza tukajikuta tumetunga sheria mbaya; kwa sababu ni kweli katika hotuba amesema kwa uwazi sana. Alichokisema Mheshimiwa Waziri kipo kwenye maandishi, ninadhani tutampa muda atakisema vizuri.

Ninataka Mheshimiwa Waziri useme baadaye kwa sababu kipo kwenye hotuba au unataka kufanua kwa sasa? Haya basi Mheshimiwa Waziri fanya hivyo kwa dakika chache.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Kwanza, kama alivyozungumza Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, suala hili lilipendekezwa na Kamati ya Fedha na Uchumi na Serikali ikalikubali. Kwa hiyo, wakati hizi sheria zimeandikwa, pendekezo hili lilikuwa halijakubalika na Serikali, *schedule of amendments*. Ninasikitika kwamba, limechelewa kutolewa, lakini *schedule of amendments* imetolewa na hilo tayari limeshachukuliwa na Waziri wa TAMISEMI ataaeleza jinsi gani Sheria ya *Local Government* itakavyobadilisha ili kuhakikisha kwamba, haya niliyoyasema mimi yanachukuliwa *into account*. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, pamoja na maelezo hayo bado maelezo yangu ninadhani yako *valid* kwamba tuko kwenye *process* ya kutunga sheria na tunaitunga baadaye jioni tutakapoingia kwenye Kamati ya Bunge Zima; kwa hiyo, nilikuwa ninadhani hilo linalotaka kufanyika nalo lifanyike na Mheshimiwa Mnyika na wewe unaweza uka-move *schedule of amendment* ili fursa yako ya hoja isipotee. Endapo maelezo yatakayokuja na *schedule* hiyo itakayokuja itatosheleza hoja hii ya Mheshimiwa Mnyika, basi hakuna tatizo maana dhamira yetu ni moja, kutunga sheria. (*Makof*)

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipatia fursa nami niweze kuchangia kwenye hoja iliyoko mbele yetu ya Sheria ya Manunuzi ya Umma. Nitakuwa na *point* mbili au tatu za kuzungumzia katika kutoa mchango wangu kwenye Muswada wa Sheria hii. Kwanza kabisa, nitazungumzia kuhusu mamlaka aliopewa Mtendaji, *Accounting Officer*. Kwa maoni yangu, kuna baadhi ya vipengele ambavyo ninahisi havistahili apewe huyo *Accounting Officer*.

Ninaomba kwa ruhusa yako nivisome ambavyo vipo kwenye kipengele cha 36(1)(b), kimeandikwa kwamba: *The Accounting Officer shall have the overall responsibility for the execution of the procurement process in the procuring entity, and in particular, shall be responsible for: sasa ninapendekeza hii part (b) ambayo inasema appointing the members of the tender board specified in the Second Schedule; ninaona kama ni kubwa sana kwa kupewa huyu Accounting Officer, kunaweza kukawa na kutokuwepo kwa uwajibikaji au kwa upendeleo fulani wa kibinadamu. Nilikuwa ninapendekeza, kwa sababu nimekuwa nikishuhudia katika manunuzi ya*

umma kupitia kwenye Kamati yetu ya *POAC*, tunashuhudia matatizo mengi sana ambayo yanatokana na utendaji wa hawa *Accounting Officers*. Kwa nini tusifikirie basi kama utoaji wa zabuni unatokea katika maeneo yetu labda ya uwajibikaji wa Wabunge labda kwenye Majimbo na unakuta kuna Mbunge wa Jimbo na Wabunge wengine wa Viti Maalum; kwa nini tusipendekeze hawa *member* wa *tender board at least* waweze kushirikishwa na Wabunge; kwa sababu ninaamini Wabunge tuna *integrity* ya kutosha hatuwezi kuwaangusha wapiga kura wetu? (*Makofii*)

Kitu kingine ambacho ninaona cha kuondolewa kwa *Accounting Officer* ni kipengele cha (e), ambacho pia kinampa mamlaka ya *ku-appoint the evaluation committee and negotiation team*. Sasa huyu *Accounting Officer* achague *tender board*, *Accounting Officer* anapewa mamlaka pia ya kuchagua watu wa *ku-evaluate* Kamati na Timu ya *negotiation*, ninahisi hii siyo sawa. Kwa hiyo, ninaomba Waheshimiwa Wabunge tuweze kufanya hii *amendment*, tupeleke pia kwa pendekero langu la kwanza kwamba *Members of Parliament* nao waweze kuhusishwa katika hili ambao kwa mtazamo wangu ninaamini kwamba, tutakuwa waadilifu zaidi hatutawenza kuliangusha Taifa letu na Wananchi wetu.

Kipengele cha (i) pia ambacho kinaonesha kwamba *Accounting Officer* pia *at-investigate complaints by suppliers, contractors or consultants*; ninaona kama kutakuwa na element za *biasness* hapa. Kwa hiyo, sioni kama hiyo inam-fit huyu *Accounting Officer*. Vilevile kipengele cha (l) ambacho kinasema; *the approving procurement not included in the annual procurement plan*, awe ana-approve all the procurements na hii pia ningependa aondolewe. Hapo pia ninaona kama mmerudia kipengele (m) na (l), kwa hiyo, ninafikiri inatakiwa kiondolewe kipengele (m).

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nirudi kwenye kitu ambacho ndiyo kimekuwa *debate* katika Bunge hili ndani ya hii nyumba ni kuhusiana na ununuzi wa bidhaa zilizotumika. Historia inatueleza kabisa kwamba, kwa bahati mbaya sana, watendaji waliopo katika Mashirika ya Umma na kwenye Serikali, hawana uadilifu; *integrity* ni zero au ina *percent* ndogo sana na kwa sababu uadilifu wao ni *questionable*, yaani hawana kabisa uadilifu, inapelekea sisi kupata wasiwasi wa kusema kwamba tuwaruhusu au turuhusu hii sheria ya...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, kwa lugha nzuri ya Kibunge, ukisema baadhi yao unaafanya jambo linakuwa zuri zaidi, ukisema wote uadilifu ni zero, yapo mengi makubwa na mazuri wamefanya katika nchi hii. (*Makofii*)

Kwa hiyo, ninadhani kwa Lugha ya Kibunge, unajua Mbunge una hadhi, ukitoka tu nje hapo unaanza kukutana nao, lakini nimewaambia wote siyo waadilifu; hebu weka baadhi yao, inakuwa lugha nzuri zaidi. (*Makofii*)

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru. Asilimia zaidi ya 70 uadilifu ni wa mashaka na ninasema hivyo kwa sababu ninawaona wanapokuja kwenye Kamati zetu. Inawezekana wapo lakini ni wachache sana, sasa kama zaidi ya asilimia 50 uadilifu wao ni wa mashaka *then* hii inatupa utata wa kusema kwamba turuhusu manunuzi ya vifaa viliviyotumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma, kwanza ninapata utata, ukitaka kufafanua hili katika vipengele viwili kwa maana ya uadilifu na pia katika zana ya kiuchumi, *from the economic point of view*, wamefanya *cost benefit analysis* ya kununua kitu kipyra hata kama Serikali haina hela za kutosha na kununua kitu kilichotumika ni kipi bora? Kwa sababu ukinunua kitu kilichotumika, kuacha *risk* ambayo Wabunge wengi walionesha *concern* ya kwamba itauwa Watanzania, lakini pia *life span* yake kwa maana muda wa kutumika utakuwa ni mfupi. Vilevile gharama za kuki-maintain hicho kitu ipo juu sana. Sasa ukiangalia *in the long run*, ni bora hata kama tunajua tutakuwa na uhitaji wa kununua kwa mfano ndege, basi *tu-budget ahead*, tuseme tutenye hela kiasi fulani baada ya muda fulani tununue ndege ambayo ni mpya; lakini ukisema leo unanunua ndege ambayo kwa mfano ndege mpya inauzwa shilingi trillioni nne na ndege ya zamani ambayo ni *used* ipo katika *good condition* inauzwa labda shilingi trillioni mbili unasema twende kwa hii ya trillioni mbili ni rahisi. Kwa mtazamo wa haraka haraka utaona ni rahisi, lakini katika muda ujao, *in*

*the long run, itakuwa ni ghamama sana kwa sababu maintenance cost, life span yake ni ndogo na risk zingine ambazo zinaweza kupelekea kwa Watanzania wetu. (Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma kipengele cha 65(1) kinasema kwamba; *emergency procurement may be made where the accounting officer determines that it is in the public interest that the goods, works or services be procured as a matter of urgency*. Sasa *the accounting officer* ata-determine kwamba kwa mahitaji ya Watanzania au Umma tunahitaji kununua hivi vitu. Kinachonitia wasiwasni kipengele cha tatu ambacho kinasema, *for implementation of subsection (1) and (2), the procuring entity may undertake procurement of used heavy plants or machinery upon satisfying the following criteria*. Kwamba, kama imejulikana kwamba kitu wanachokihitaji hakitawenza kupatikana kwa muda huo, lazima kipewe muda wa kutengenezwa, kwa hiyo, watalazimika kununua kitu ambacho ni *used*.

Pili, wanakwambia kwamba tukiwa na *lack of budget*. Sasa mimi ninajuliza katika Serikali yetu hatuna *emergency funds?* Kama kuna *disaster imetoka for example*, unasema una bajeti haitoshi hadi tunapelekea kununua kitu ambacho ni *used*, ambacho kina mashaka, ambacho kimetumika ili kuweza ku-rescue matatizo yaliyojiteza na hapa kuna utata labda Waziri akija afafanue zaidi kwamba hii *emergency* au udharura wanamaanisha nini? Udharura ambao unatokana *na the act of God* kwamba tumepata majanga ambayo hatukutarajia au ni udharura ambao unatokana na *poor planning* ya watendaji wetu? (Makof)

Kama ni udharura ambao unatokana na *poor planning* ya watendaji wetu, *then hii kitu kwa kweli hairuhusiwi kwa sababu kama ni poor planning au ni plan mbaya za watendaji wetu, huwezi ukaja ukaita kwamba ni ununuzi wa dharura; na ndiyo maana tunasema kwamba, inabidi watendaji wawajibike vilivyo*. Kama ni *the act of God* pia Serikali itenye fedha, kuna fedha zinakuwa zinatengwa kwa ajili ya maafa na vitu vingine, sasa kama kuna fedha za aina hiyo, kwa nini tununue vitu vilivytumika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninapingana vilivyo na hiyo dhana, hauwezi ukunanua vitu vilivytumika kama mashine za hospitalini. Kipengele namba 65(3) na kipengele chake cha (a) na (b) *emergency* na kipengele cha 65(2) pia kimeelezea.

Kwa hiyo, dhana yote inayoelezea kuhusu ununuzi wa vifaa vilivytumika na kama nilivyoeleza mwanzoni kwamba, watendaji kwa asilimia kubwa siyo waadilifu, leo hii watasema kwamba ni kweli sikatai unaweza ukapata vitu vilivytumika ambavyo ni vizuri, lakini kwa sababu tuna historia ya Watanzania, asilimia kubwa ya watendaji wana masilahi binafsi; yaani akitaka kununua kitu anajitengea kwanza yeche kati kuna hiki kitu kama ni billioni moja lazima atajenga nyumba ya milioni 500 kutohana na hii kitu. Kwa hiyo, ndiyo maana tunapinda hii dhana yote, siku ikija kujulikana kwamba ni waadilifu kwa asilimia 100 kwamba wakiambiwa wanunue kitu ambacho kimetumika kweli watakenda kununua ambacho kimetumika, lakini kwa asilimia ndogo. Kuna kitu ambacho kimetumika kwa muda mchache, lakini bado kina *condition* nzuri, lakini uadilifu kwa Watanzania bado una utata na hiki kinapelekea tununue kitu kipy, ambacho kitakuwa kinaelezeka na lazima tueleze kabisa kitu kipy siyo feki maana siku hizi kuna vipy feki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma namba nne ya *section* ya 65 inakwambia mwendelezo wake *upon satisfying the provisions of subsections (3), the procuring entity shall seek approval of the Cabinet before proceeding on with the procurement*; yaani kila ikitokea dharura ya manunu, lazima wapeleke kwa Mawaziri. Kwa mtazamo wangu, ninahisi kwamba, Baraza la Mawaziri tunalitwisha mambo mengi mengi zaidi, ikitokea *emergency* sehemu yeyote ile Tanzania wakitaka kuitisha *approval* wapeleke kwenye Baraza la Mawaziri. Mimi ninaichukulia kwa mtazamo hasi na sidhani kama hii inafaa, wana mambo mengi ya kufanya na mengine hata bado hawajayakamilisha. Kwa hiyo, ninaomba hiki kipengele pia kifanyiwe marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia na kwa msisitizo zaidi niwaombe Waheshimiwa Wabunge chonde chonde, bila kujali itikadi yako ya chama, kuwa mzalendo, usome Muswada huu kwa uhalali wote, tafakari, tusichukulie mtazamo hasi, tuangalie hali halisi ya Tanzania watendaji wetu wanafanyaje. Hivi ukiruhusu leo kufanya ununuzi wa dharura au ununuzi wa vitu vilivytumika; jamani tutafakari mara mbili, tatu; je, kuna umuhimu wa kununua vitu vilivytumika?

Jana watu walikuwa wanasema aah, mbona mnanunua magari yaliyokuwa used? Tofautisha *individual procurement*, *Private Sector Procurement* na *Public Sector Procurement*. (*Makofii*)

Mimi kama mtu binafsi niki-*procure* gari nitakuwa committed. (*Kengele*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, muda wako umekwisha, sasa nitamwita Mheshimiwa Murtaza Ali Mangungu na baadaye atafuatiwa na Mheshimiwa Asumpta Mshana.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi adimu na mimi niweze kutoa maoni yangu katika Muswada huu ulioko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwneyekiti, mimi binafsi, nikueleze tu kwamba, ninakubaliana na Muswada huu na Muswada huu ni mzuri kwa asilimia 99.9. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwneyekiti, nikifuatilia majadiliano yaliyokuwepo hapa, ipo haja ya Wabunge kuisoma vizuri Miswada hii kabla ya kuja kuchangia hapa maana inaweza ikafika wakati tukawianisha vitu, mathalani unaweza ukawianisha matunda, lakini huwezi kuiwanisha machungwa na maembe. Ipo dhana moja; mamba anapokikamata kiumbe chochote kile huwa anatoa machozi mengi sana na kama wewe ukiwa mbali unaweza kufikiria mamba yule anamwonea huruma yule aliyemkamata kumbe yale machozi ni ya furaha kwa lile tendo ambalo analifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ninafuatilia mjadala huu ukiendelea, nimesikitika sana kwa maana kwamba, wapo wengine wametumia mpaka mifano ya hotuba za kibaguzi ambazo zilikuwa zinatolewa na Wazungu kuukandamiza utu wa mtu mweusi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana nydingine iliyoukupopo hapa kwamba, Serikali hii imeshindwa kupanga, lakini Serikali hii ndiyo ambayo inatengeneza barabara na ndiyo ambayo imetengeneza hata hili Jengo la Bunge. Serikali hii baada ya kuchukua kutoka kwa Wakoloni, tumeweza kujitengeneza mfumo wa umeme na kila kitu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiendelea tutawapotosha Wananchi na ndiyo tunasema kwamba tumekosa uelekeo. Imani yangu ni kwamba, Serikali hii haijakosa uelekeo, ipo makini na ndiyo maana tumeifikia hatua hii tuliyokuwa nayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi kwenye Muswada, dhana ya Muswada huu, kwanza kabisa ukiangalia *Section (8)* imesema kwamba, yenyewe inatoa sasa mamlaka kwa PPRA kuwa na uwezo wa kufanya kazi zake kiufanisi. Wameanzia kwenye (a) mpaka (e), lakini katika kipengele hiki mimi nina ulakini kidogo kwenye (c), kwa sababu nitanukuu kama ifutavyo: *The objective of the Authority shall be to set standards for the public procurement systems in the United Republic of Tanzania; standards hizi tunazipata vipi?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye *section 54(1)*, yenyewe imesema hivi: *Tenderers are allowed to participate in procurement proceedings without regarding to their nationality*. Ipo haja ya msingi kabisa kulinda viwanda vyetu vya ndani, kulinda wakandarasi wetu wa ndani, hii dhana ya kusema kwamba kampuni iwe imesajiliwa Tanzania peke yake huku tukijua kabisa sheria yetu inaruhusu watu wa nje kufungua makampuni ndani ya hii nchi, tunawaumiza Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba Waziri atakapokuja kuleta majibu, atueleze kinagaubaga ni jinsi gani na ni kwa namna gani Watanzania watalindwa kwenye kushiriki. Lazima tuweke *ceiling* kwamba, ikifikia kiwango hiki hapa haruhuswi mtu mwininge yeoyote kutoka nje kuingia kufanya kazi hii. Hapa ndiyo tunapokuta kwamba kuna Mataifa ya kigeni yanaleta watu wao hapa kufanya kazi za tender hata za milioni kumi. (*Makofii*)

Makampuni haya ya Watanzania ambayo tumeyasajili na yanafanya kazi hapa; wanapataje kazi na hawawezi ku-compete? Wenzetu wapo connected na suppliers kutoka katika nchi zao na vilevile wanapewa facility za aina tofauti. Sasa tukija hapa na sisi tunawapokea wao kama Watanzania, hali ya kuwa siyo Mtanzania tu kwa kigezo cha kusajili kampuni, hapa hatuko sahihi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipo kipengele ambacho kimeleta mjadala mrefu sana, lakini kwa mimi labda iwe mwalimu wangu hakunifundisha vizuri, lakini ninachoona hapa, kipengele cha 66 kimezungumza vizuri sana kimesema; *where the public interests demands that railway machinery, civilian or military ship, civilian or military aircraft has been used be procured, the procuring entity may, upon approval by the Cabinet and the Authority, proceed with normal or emergency procurement.* Hivi jamani kweli Wabunge humu ndani hatuelewi maana ya Cabinet?

Cabinet ni Baraza zima la Mawaziri ambapo Mwenyekiti wake ni Rais; kweli Rais anaweza akakubali kupitisha kitu ambacho hakina maslahi kwa Wananchi wa Tanzania? Imefikia hatua hiyo? Tuisome hii Miswada vizuri jamani, tuisiwapotoshe Wananchi, Wananchi wote wamekaa wanatutazama na wanasikiliza tunachokizungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakupa mfano wa jambo moja; leo hii tukizungumzia kununua ndege moja ya abiria ni zaidi ya dola milioni 65, lakini tunao Wananchi ambaao wana shida ya kupanda ndege. Kila siku tukiwa humu ndani tunaihimiza Serikali ijitegemee itumie fedha zake, Serikali haina uwezo wa kufanya hayo yote na ninyi mnafahamu; sasa hii dhana ya kujitegemea tunaipata viyi kama hatuwezi kuweka mipango inayowiana na uwezo tulionao? Vifaa hivi viliviyotamkwa hapa vyote vina kitu kinachoitwa *life span*, ambayo Mheshimiwa Matiko amezungumza. Kama ndege imetumika miaka mitano, *life span* yake ni miaka mia; sisi tutakuwa tuna makosa gani kununua ndege hiyo na ikaweza kutusaidia? (*Makof*)

Vilevile hivi vifaa vinavyonunuliwa siyo lazima kitu kipyta ndiyo kipewe *warranty*, siyo kweli; kitu chochote mnaweza mkakinunua kwa mkataba na kikafanya kazi kikapewa *warranty* na kikaendelea kuhudumia Wananchi. Leo hii wale wajukuu zetu wa Mikoa ya Ziwa, Wanyamwezi kule, wana matatizo ya reli, kama kipo kichwa cha treni ambacho kimetumika labda kwa miaka mitano, kumi au ishirini; kwa nini tusikinunue kikatuendeshea tena miaka 50 inayokuja? Hapo dhambi iko wapi? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hii ndipo ambapo kila siku tutakuwa tunailaumu Serikali na tutakuwa tunalaumu utendaji wa Serikali. Kwa sababu tunapokataa Serikali isiyafanye haya, tunatoa *room* kwa makampuni binafsi kuja kuvekeza hapa na wao wanapowekeza, wanunuva vifaa hivyo hivyo ambavyo vimetumika, wanakuja na mitambo hiyo hiyo ambayo imekwishatumika na wakishawekeza Serikali inapungukiwa na mtaji kwa sababu wale watakuwa wamewekeza zaidi kuliko sisi. Sasa kama hii inawezekana kwa nini tusikubali Serikali yetu leo ikashiriki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye dhana hii binafsi sioni kama kuna tatizo la kipengele hiki. Maoni ya Wabunge karibu wote ni kuwa, kipengele hiki kiangaliwe kwa makini kwenye utekelezaji wake na katika ufanyaji wake kazi. Pamoja na Cabinet kushirikishwa, iangaliwe namna bora, ikiwezekana, Kamati za Bunge zipo ambazo zinafanya kwa niaba yetu sisi, basi nazo zishirikishwe katika mfumo huu wa ununuzi wa hivi vifaa. Jambo la aibu na la ajabu sana leo hii hapa tunazungumza kwa nini Serikali inunue ndege iliyotumika ya kijeshi; hii itawezekana viyi?

Dokta Mahenge alikuwa anazungumza hapa kwa mfumo huo huo wa kununuva vitu vipyta, hakuna kitu ambacho kitaingia Tanzania kikiwa kipyta, kwa sababu kimeshatengenezwa ni lazima kifanyiwe *testing* na kikifanyiwa *testing* hata ya kilomita moja au ya nusu inchi, imetembea nusu inchi tayari imetumika; sasa tutapata wapi vitu vya aina hiyo? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaomba kuwasihni sana Wabunge wenzangu, tuupitie vizuri Muswada huu, tuisaidie Serikali itekeleze majukumu yake na tuwasaidie Wananchi wenzetu ambaao wanateseka katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa, kwenye suala la kushirikishwa Halmashauri Mheshimiwa Mnyika na wewe Mwenyekiti na Mheshimiwa Waziri hapa, mmetoa ufanuzi na michango ya aina tofauti. Hilo nilikuwa nimeshaliona, lakini niliona labda nije kulizungumza kwenye mchango wangu. Kwa hiyo, tungeomba kabla Mheshimiwa Waziri hajafanya majumuisho, Waziri wa TAMISEMI atuletee sasa hizo *amendments* ambazo amezifanya au anakusudia kuzifanya ili kuweza ku-accommodate na hii sheria ikawa *more effective* na ikasaidia utendaji wa shughuli zetu za kila siku. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, ninaomba niunge mkono hoja na ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mangungu, ninakushukuru sana kwa mchango wako. Sasa ninamwita Mheshimiwa Assumpter Mshama na kama tutajaliwa basi atafuatia Mheshimiwa Shekifu. Acha niende kidogo kidogo hivyo, nina hali ngumu kweli hapa, maana *note* ninazoandikiwa hapa sina la kufanya. Mheshimiwa Assumpter Mshama.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Kwanza kabisa, ninamshukuru Mungu, kwa kunipatia nafasi kusimama mbele yake na mbele za Waheshimiwa Wabunge na mbele yako Mwenyekiti.

Nianze kwa kusema kwamba, jambo hili limepotoshwa, hasa jana liliptoshwa sana kwa Wananchi. Katika habari ya vitu kuna aina nne; kuna kitu kipyaa, kitu kilichotumika, *re-condition* na *scraper*, yaani kitu ambacho hakifai, chakavu ni hatua ya nne kabisa. Sasa nipeende kusema kwamba, nimeletewa *message* nyingi sana hapa na wapiga kura wangu, wananshihi nisilunge mkono hoja ya vyombo chakavu. Hakuna hoja ya vyombo chakavu. Ninataka niwajulise kwamba, hakuna cha orodha ya vyombo chakavu, kuna kununua vifaa viliviyotumika kwa ajili ya *emergency* na kwa sababu ile Sheria ya kwanza ilikuwa imefunga, tunajaribu kufungua, kama kikitokea dharura tunakwenda kununua vitu viliviyotumika, siyo chakavu. (*Makofii*)

Mimi niseme hivi; hivi sasa nina miaka 50, tangu nimekuwepo nimeona tukitumia vitu viliviyotumika na vikiendelea kutumika na bado vimesaidia watu na tunavyo mpaka leo. Kwa hiyo, ninashauri Watanzania waelewe kwamba, Serikali yao makini waliyoiweka madarakani, ina mawazo yaliyo mema na itahakikisha inachagua vitu vilivyo bora kwa ajili ya Taifa na wala siyo vitu chakavu. Hatuwezi kukaa hapa watu wazima tukaongelea kununua ndege chakavu, hebu tuongelee ndege, ndege inakwenda kwa saa; labda tuishauri Serikali itakapokuja itueleze inapoongelea kitu kilichotumika ina maana kilichotumika kwa muda gani kwa sababu ndege inatumia saa. Kwa hiyo, itakapokuwa imetimiza saa fulani, labda hiyo haitufai, lakini kama ndege ina saa zinazokubalika hiyo kwetu ni sawa. (*Makofii*)

Ngoja niwaambie Watanzania; sasa hivi kuna wenzetu wana ndege 777, *Air Bus* na *Concord*. Hivi sisi tumeingia kwenye *rank* hiyo? Lazima tuangalie uwezo wetu na uwezo ndiyo unaoturuhusu kununua kitu. Labda cha kushauri, kwa ndugu zetu ambao watakuwa wamepewa mamlaka hiyo, tunachoomba sasa ni wakati wa kurudisha uzalendo na ni wakati wa kurudia nyakati za Nyerere na Sokoine; watu ambao walikuwa tayari kufa kwa ajili ya nchi yao; hicho ndiyo kitu tunachopungukiwa. Siyo matumbo yetu kwanza na nina uhakika kwa mtindo huu tunaokwenda nao, juzi tu hapa Wananchi mnaosikiliza tumemsimamisha hata Katibu Mkuu Wizara ya Nishani kutaka maelezo. Hivyo, hata hawa watu watakaokuwa wamepewa mamlaka, tuna haki ya kuwaambia tunataka vitu na vikifika vitu ambavyo siyo sahihi, tutawasimamisha na hata kuwafukuza kwenye nafasi hizo. Hatuna haja ya kubabaishwa. Mimi nilichokiona jana nilitamani hata kulia, kwa sababu tangu tumejitawala mtu analeta mfano wa Botha hapa kutuambia sisi, kwanza mimi sisemi ni Botha, ni yeche ametukana. (*Makofii*)

Huwezi ukaleta mfano wa kutukana, mtu anakuja nyumbani kwenu anasema baba yako na mama yako nimewaona; mmoja kichaa na mwagine mshenzi. Halafu unamwambia baba ndiyo maana fulani siku moja alisema wewe ni mshenzi. Utakuwa wewe ndiyo umemwambia baba yako mshenzi. Kuna mifano ya kuiga na kuna maneno ya kutamka, lakini huwezi kutoa mfano wa Botha. Hivi South Africa leo haiko huru; anayetawala si Mwfrika? Mimi katika hilo nimeona ni udhalilishaji. (*Makofii*)

Huwezi ukatoa mfano wa matusi ukauleta hapa Bungeni na Watanzania wengine walikuwa hawajui kama Botha alikosea kiwango hicho. Leo kuna Mwfrika South Africa na wanaendelea na uchumi wao kama kawaida, sijaona kilichopunguka South Afrrica. Nimesoma pale zaidi ya mara nne, ninaona maisha yanaendelea na Waafrika wanaunganishwa wanaishi maisha mazuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Watanzania kokote mlipo hili neno la uchakavu halipo na Waziri huyu hawezi kuleta kitu chakavu. Tunataka kuangalia mfuko wetu una uwezo gani. Hivi ndege mpya unajua bei yake? Tukisema tulete mpya wakati *competitor* wetu analeta vitu vilivytumika na bado wanajaa kule na sasa ninataka niseme hata hivi sasa ndege zikja, Wafanyakazi wa Serikali tumieni ndege za *Air Tanzania* kuliko kila siku mnapanda ndege za watu wengine, tumieni ndege zetu ili ziweze kuendelea. (*Makofi*)

Mimi ninauliza treni gani unaweza kuikuta dukani; leo tukitaka kichwa cha treni twende dukani hodi tunataka kichwa tunaweza kukikuta dukani? Lazima utoe *order* na tukianza kuagiza leo *train* itachukua miaka mitatu au minne, wakati kichwa kimepinduka pale Sekenke; kwa nini tusichukue kichwa kilichotumika?

Ndege iliyotumika kwa miaka mitano au kumi kwa Afrika ni mpya. Hakuna katika Bara la Afrika nchi ambayo inanunua ndege mpya kama ipo ni Ethiopia nayo ni kwa sababu imeamua kufanya usafiri wa anga kama kitega uchumi klikubwa kama tulivyo na madini Tanzania. Kwa hiyo, tangu zamani uchumi wao ni ndege tu na sisi tukiamua kufika hatua hiyo, tutanunua ndege mpya. Nenda Kenya kaangalle, hata hivyo tulivyoongelea hapa ni mambo ya kivita. (*Makofi*)

Juzi juzi tulikuwa na vita, ndege moja ilianguka, tunahitaji ndege ya kuendeleza vita; tuanze kwenda kutafuta mpya au tunatafuta hata iliyotumika tunaendelea kupigana? Mimi ninadhani kitu cha msingi ni wale watu wanaokwenda kukaa kwenye hizo nafasi, wanaokwenda kununua hivyo vitu. Tuking'ang'ania vipyta kuna vitu vya Mchina pale, utaleta kitu cha Mchina, mtu mwingine ataleta kitu cha Japani chenyé miaka kumi na cha Mchina cha jana kinakufa wakati cha Mjapani bado kipo kwa sababu kina muda uliotengenezwa. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Watanzania popote mlipo, hili Bunge lina tofauti na hatutaruhusu vitu visivyofaa, tunakwenda kuwatendea haki lakini acheni kusikiliza propaganda. Maana ninasema *oxygen* ya Upinzani ni kupinga, ili aweze ku-survive kwenye Upinzani lazima apinge hata akiambiwa mama yako mzuri, atasema mama yangu ni mbaya kwa sababu aliyesema siyo Mpinzani. Mimi nilikuwa ninafikiri ...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge?

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Sawa sawa, vipengele vimesomwa sana kama hujanisikia mimi ninaendelea ooh!

**MWENYEKITI:** Tusikilizane, Waheshimiwa Wabunge ni haki ya kila Mbunge kuchangia; ni kwa mujibu wa utaratibu. Sasa hata kama unakerwa, nillsema hapa jana ndiyo siasa; sasa tuvumiliane, nikienda upande mwingine msije mkakilalamikia Kiti, lakini nikirudi huku, Mheshimiwa Msingwa jana alijiachia kweli kweli hapa. *It was a fare play.* Sasa ninasema tujaribu kuwa wastahimilivu. Mheshimiwa endelea.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Labda niendelee, ninarudia tena, kwa mfano, kusema ukweli hakuna chombo chakavu kitakacholetwa Tanzania. Kitaletwa kitu kilichotumika na kwa kuzingatia ubora wa kile kitu na muda uliyotumika kule. Labda niseme tu kwa *Accounting Officer* na utaratibu mzuri ambao tunaweza kuufanya ili tupate vitu vilivyo vizuri. Maana hapa tulisema ufanisi na vitu madhubuti pamoja na kuuboresha huu Muswada. Kwa hiyo, nilikuwa ninashauri mamlaka aliopewa huyu *Accounting Officer* ni makubwa sana, kwa ujumla wake sina haja ya kuyataja. (*Makofi*)

Mheshimiwa alishavitaja vitu vyote pale. Kwa nini isiwepo Kamati ya Fedha ya Halmashauri ipewe *mandate* kubwa ya kuwaidhinisha na kukataa au kukubali hata kama kuna uharaka wa namna gani; hiyo Kamati ikae na iweze kuitisha kuliko mtu mmoja kumpatia majukumu makubwa? (*Makofi*)

Katika *tender* tuna tatizo lingine ambalo linasumbua sana; kwa mfano, inatolewa *tender* ndani yake kuna watu wana tabia ya umimi wana-leak information na vitu gani ambavyo vingetakiwa kuwepo pale. Matokeo yake anakuja kupata mtu asiye na uwemo. Sasa kuna vigezo ambavyo vinachukuliwa, ninataka tuangalie ubora, uzoefu wa yule mtu na ujuzi wa kutenda kile kitu. Anaweza akaweka bei kubwa lakini kumbe ndipo atamaliza kazi kwa ukweli. Akaweka bei ndogo baada ya siku mbili barabara imetoboka na wewe alipokukabidhi ilikuwa ina-shine. Ameweka lami ya juu inaendelea miezi miwili inatoboka. Kwa hiyo, ninashauri tuangalie ubora, uzoefu, pamoja na ujuzi wa kitu ambacho mtu amepewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninaendelea kusema kwamba, ikitokea sasa habari zimepatikana, mtu ame-*tender* amepata, malalamiko yametokea na inaonekana kweli huyu alipata habari na kuna mtu yuko pamoja naye; *tender* hiyo ifutwe na wala ile Kamati yote iondolewe kwenye hiyo shughuli ili watu wapate kujifunza na pale tutapata nidhamu nzuri. Kwa hiyo, ninafikiri ni vyema Watanzania wote tukarudisha moyo wetu nyuma; ni wakati mzuri wa kulitumikia Taifa letu kwa uaminifu kuliko mtu unaamua wewe na tumbo lako na familia yako na ni kweli kwamba watu wamefanya hivyo. Tuseme ukweli, siyo percent kubwa kihivyo, ingekuwa percent kubwa hizi barabara zingekuwa hazipitiki. (*Makofi*)

Kwa hiyo, kitu ambacho tunakwenda kufanya, tunaomba Waziri aje na *lifespan* labda tunasema kama ni meli iwe imetumika miaka kumi, kama ni ndege tujue saa ilifanya kwa saa ngapi. Ndege yoyote iwe mpya, iwe ya zamani, lazima kila mwaka iende *check* na ikifanya *check* inakuwa kama mpya, kwa sababu wanatoa vifaa vyote vile ambavyo havifai wanaweka vipyta, inaanza kufanya kazi. Kwa hiyo, suala la ndege kwa kweli ninalifahamu na nimefanya kwenye ndege na kwa maana nytingine hata ndege hii unayoiona tunayo, *Forker 28*, leo kiwandani haipo. Kila tukitaka kuipeleka mafundi wake wapo na vifaa vyake viro. Kwa hiyo, ndege ikiwa haipo sokoni, haina maana kwamba kifaa hakiwezi kupatikana, maadam yule aliiteitengeneza ame-guarantee kwamba ataifanyia service. (*Makofi*)

Vyombo vya kivita; hivi kweli tunaweza kwenda kununua *missile* mpya kwa hela gani na kwa vita ipi? Sisi ukituletea kifaa ambacho tunajua risasi zitatoka, kwanza, hata mipaka yetu ikishajua tuna vifaa tu ni amani, wana jua kwamba hawa watu wapo tayari kupigana. Kwa hiyo, hatuna haja ya kuchukua mamillioni kulundika kwenye vitu ambavyo haviwezi kutumika na hatuna haja ya kufanya hivyo.

Hakuna meli iliyopo dukani ambayo tutakwenda asubuhi tutasema hodi tunataka meli tukanunua kama tunavyonunu gari. Hapana, unatoa *order* itachukua miaka mitatu. Leo hatuna meli katika sehemu zingine.

Kwa nini walio mbele na ukishaitwa *Third World* kubali kwamba wewe ni *Third World*, huwezi kupambana na *First World*. Lazima tukubali kwamba, tutavitumia lakini umakini uwe kwa wale ambao watakuwa wamepewa mamlaka. (*Makofi*)

Kwa hayo, machache ninaamini kabisa tumeelewana. Ahsanteni kwa kunisikiliza. Ninaunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Assumpter Mshama. Sasa nitamwita Mheshimiwa  
...

Mheshimiwa Taarifa.

## TAARIFA

**MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 68(8), ninapenda nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge aliyemaliza kuzungumza kwamba, Wabunge wanashindwa kutofautisha maana au tofauti ya kitu kilichotumika na chakavu. Ninapenda nimpe taarifa kwamba, chakavu na kitu kipyä ni tumbo moja; ni pacha, huwezi kuwatenganisha. Ndiyo sababu unaponunua kitu kipyä dukani wale wenzetu Wahasibu kwenye mahesabu wanaanza sasa kila mwaka ku-*establish* uchakavu, kiwango cha uchakavu kila mwaka cha mali iliyanunuliwa mpaka mwisho wa siku wanapata *zero book value*. Kwa hiyo, unaponunua kifaa leo kinapoanza kutumika ndipo na uchakavu wa hicho kifaa unaanza kuhesabika. Kwa hiyo, ningependa ajue kwamba, hatuelewi maana ya uchakavu au maana ya kifaa kilichotumika. Nilitaka nimpe tu hiyo taarifa. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lugola, kama nimemsikiliza vizuri Mheshimiwa Assumpter na wenzangu mmesikia amesema, kuna makundi manne katika vitu; *kwanza*, kipyä (*new*); cha pili ni *used* kwa maana *kilichotumikal*; cha tatu *kilichokarabatiwa* kwa maana kitu *kilikuwepo* *kikarabatiwa* *kinaitwa recondition*; na cha mwisho kabisa ni *scrapper*; ndiyo *mnasema* chakavu. Chakavu ni kitu *kilichokufa* *kinapaswa* kutupwa. Sasa ndiyo nilikuwa *ninasema*, *ukisema* hapa kwamba chakavu na *new vinaishi* katika tumbo moja, aah, mimi ninadhani siyo tumbo moja. Kwa hiyo, nimpe tu taarifa sijui unaipokea hiyo taarifa, mimi nilikuwa *ninafanua* tu.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Ninadhani siipokei, hata yeye anaona kwamba haijapokelewa.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea, ninamwita Mheshimiwa Henry Daffa Shekifu.

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninakushukuru sana. Baada ya wazungumzaji wawili wa mwisho; Mama Assumpter na Mheshimiwa Mangungu, kwa maelezo waliyoyatoa ninaamini Umma wa Watanzania wameelewa. (*Makof!*)

Ninaomba sana, tunapoingia katika kujadili Miswada ya Sheria, basi ni vizuri tuisome kwanza na tusome *between the lines* katika Luga ya Kizungu na uelewe maudhui ya Muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya Muswada huu kwa kifupi, madhumuni ya mapendekezo haya ni kwanza, kurekebisha mapungufu yaliyojiteza katika utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2004, tangu kutungwa kwa Sheria hiyo mwaka 2004. Pili, kuzipa nguvu zaidi Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma na Mamlaka ya Rufani ya Zabuni kutekeleza majukumu yao ya udhibiti na kushughulikia malalamiko ya zabuni kwa uhuru na ufanisi. Tatoo, kuboresha utaratibu wa ununuzi wa umma ili kuongeza ufanisi, nidhamu na uwajibikaji katika sekta ya ununuzi wa umma. Ukihasoma hilo, Sheria inapaswa kujielekeza huko; sasa tuulize, Sheria haikujielekeza huko? Sheria hii imejielekeza huko na mimi ninaiunga mkono 100%. Yalikuwepo na yapo mawazo potofu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama nilivyosema huko nyuma, mimi ninaamini upinzani kazi yake kubwa, hata jua lingetokea Mashariki, watasema linatoka Magharibi, ni kanuni; sasa wewe utakayesombwa wakati unajua rasmi kwamba jua linatoka Mashariki ukaenda Magharibi, utaumia wewe.

Mimi niwaombe Wabunge walio na dhamira nzuri ya kuisaidia Serikali yetu, niipongeze Kamati ya Fedha na Uchumi, imechambua vizuri Muswada huu kwa niaba yetu na ndiyo taratibu za kutunga sheria; pengine inawezekana Wabunge wengine hawaelewi, unaweza ukazungumza hapa saa 24, lakini hapa Muswada ulipofika utapita. Ukitaka uende kwenye Kamati, ndiyo mabadiliko yote yatatoka huko, yakishafika hapa tukijadili katika ngazi hizi, hapa ndiyo tunatunga Sheria, wewe kama utazungumza maneno usikike huko kwa wananchi, utasikika lakini sheria itasimama palepale na madhumuni yake yatakuwa ni yaleyale. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nitamke tu kwamba vifungu ambavyo vimetukorofisha ambavyo kwa kweli vimepotoshwa sana, ni hicho kifungu cha 65 na 66. Lakini

vifungu hivi na ukiangalia ile *amendment* ambayo inakuja, inajieleza vizuri. Sasa labda upungufu wa kuielewa lugha iliyotumika; na ndio maana kuna umuhimu pengine kubadilisha, Kiswahili nacho kiletwe katika kujadili Miswada. Hapa imesemwa hivi, ili tuweze kufikia uamuzi wa *emergency procurement*, masharti yafuatayo mawili ni lazima yazingatiwe; sharti la kwanza, *compelling urgency that creates threats to life, health, welfare or safety of the public by reason of major natural disaster, epidemic, riot, war, fire or such other reasons of similar nature.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima katika kununua *emergency* itokee hivyo. Sasa unahitaji kwenda kweli ukajilize maswali? Hivi ikitokea vita, kweli hapo sio *emergency*? Utakwenda tena muda ukaanze kutafuta meli mpya, ndege mpya, ukapigane! Utapata muda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mifano mizuri, tulipigana hapa mwaka 1979 na Uganda, Mzee Mrema hapa alikuwa Usalama wa Taifa; asimame kama tuliwahi kwenda kuagiza ndege ili tukapigane Uganda! Tulikwenda na zana tulizokuwa nazo. Na mniamini msiniamini, nyingine zilikuwa ni *second hand* zana kutoka Urusi zimekwenda kutuokoa Uganda. Kwa nini mifano hii ya kweli tusiillesabu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii mifano na Sheria inatungwa kwa sababu sheria iliyokuwepo huko mwanzoni ilikuwa inakataza. Kulikuwa na tatizo juzi la umeme katika nchi yetu, humu humu ndani tulibanana, lakini Bunge hili hili huko nyuma lilitakataa kununua *reconditioned generator* kwa misingi hii hii kwamba ni *second hand*, Taifa likaingia kwenye giza la ajabu! (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi kwenye Bunge hili liliopita, tukaanza kutamka hiyo Sheria ya *Procurement*, ifutwe tukanunue mahali popote, humu humu ndani ndio tulitamka. Lakini baada ya kuona madhara ya nchi yetu kiuchumi na kiusalama. Leo tunakuja hapa tunakataa! Ooh, kije kipy! Hivi juzi sisi tungeagiza majenereta bila kutumia utaratibu ambaa ulizungusha kisheria, leo tungekuwa wapi? Hata haya tunayozungumza leo kungekuwa giza nchini, leo nchi nzima inawaka kwa gherama kubwa sana. Lakini makosa mengine tumeyafanya wenyewe huko nyuma! Kwa nini hatusomi? Na waliokuwa wanalamika ndio hao wa kwanza kusema kwamba sasa nchi iko katika...! Ndiyo waliokataa kununua yale majenereta. Kinyume chake yale majenereta Wamarekani wakaja wakayanunua, wakapitia mlango wa nyuma, umeme tunautumia hamuandamani, kwa nini? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii inakwenda zaidi inasema hivi, katika hicho kitu kinachoitwa *procurement* kwa ajili ya vitu vya *second hand*, inasema hivi; "Where the public interest demands that railway machinery, civilian or military ship and civilian or military aircraft that has been used be procured, halafu ikasema kama itabidi zinunuliwe ifuate sheria na kanuni zilizotajwa katika vifungu hivi vya huku nyuma. Kuwe na *emergency*, tumetishwa na vita na nini na nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi niulize na ninarudia; hivi hii reli ya kati hii iliyojengwa mwaka 2005, leo ukitafuta behewa lake ukaombe utengezewe jipya utalipata wapi? Utachukua miaka mitano, sita kulitengeneza behewa, wananchi wetu wanateseka; hivi kama wenzetu wa Singapore au India wanayo mabehewa, tukayanunua tukayatengeneza kwa *standard* zinazokubalika, ubaya wake ni nini? Mbona Wahindi hawa tulioalaeta walileta mabehewa yakatumika! Sasa hivi tumewakatalia, wameyarudisha kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninasema nia ni nzuri kwa Muswada huu. Na nia yake ni kurekebisha mapungufu yaliyokuwepo katika Muswada uliopita wa Manunuzi. Kwa hiyo, mimi ninaomba Waheshimiwa Wabunge, tukubaliane. Dhamira ya Serikali ni nzuri na dhamira hii tuiunge mkono. Wabunge wote wa CCM ninawaomba, msisombwe. Mimi nasema hivi tusije tukafanya makosa, tukacheza mchezo usio wetu! Maana mdundiko ni mchezo wa ajabu, unaweza kuingia unafika mwisho, unajigundua kumbe kwenu sio huko! Sasa tusije tukacheza mchezo wa mdundiko! (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ndugu zangu, wenzangu wengi wamesema, kuna kijana wangu upande ule wa pili alisema wafanyakazi wa Serikali 70% ni wabaya! Tunawaonea, ni dhambi kwa Mungu. Maana kwa kweli wafanyakazi 70% au asilimia yote ni wabaya, tunafanya

makosa. Mimi nasema wapo wachache, kama wachache hawa wapo basi sisi tuisihi Serikali yetu, katika maeneo haya nyeti ya ununuzi tafuteni wale waliopitia Seminari au waliopitia Misikitini, watakaotusaidia wakae huko. Na mimi naamini wapo Watanzania hao. Sasa kuwaambia wafanyakazi wote ni wabaya, jamani, umekaa kwenye jengo zuri hili, wafanyakazi hao ndio walioleta hayo! Chama chenyewe hicho, barabara ndiyo ukitoka hapa unakwenda kwenu unatamba, unaandika nne kwa kuringa, bado huamini kwamba ni hao! Akina Magufuli wanahangaika, jamani! Mimi nafikiri, Waswahili wanasema, mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi ninaomba tukubaliane katika hili, Muswada ni mzuri. Mimi nafikiri tutakapopata zile *amendments*, zitaongeza uzuri wa Muswada na niipongeze sana Serikali kwa Muswada huu. Naomba tugeuke wote tuisaidie Serikali yetu ifanye kazi vizuri, huo ndiyo wajibu wetu; mama Assumpter Mshama amezungumza vizuri sana kueleza vipengele vya taratibu za vitu hivi vinavyoitwa vifaa viliviyotumika. Mimi nasema, pengine tuombe sisi kama Wabunge, kwamba tusiruhusu labda miaka 30 tusema basi! Tuwaombe wenzetu wa Serikali, tu-set *limit* kwamba kifaa chochote chenyeye kununuliwa kisivuke miaka 10 au miaka mitano. Hapo tutakuwa angalau tumewapa uhuru wa kufanya kazi, lakini kuwakatalia tu ati kwa sababu hatuwaamini, hatuwatendei haki. Tositunge sheria kwa ajili ya watu, tutunge sheria kwa maslahi ya nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi hii. Mungu aibariki nchi hii na wenzangu ninawaomba tuiunge Serikali mkono. Ahsanteni sana. (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nichukue nafasi hii kukushukuru sana kuniruhusu na mimi niweze kushiriki katika mjadala huu. Na kabla sijaingia *speed*, niombe kabisa nitamke waziwazi kwamba mimi Muswada huu ninaunga mkono. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo ambayo yameletwa hapa ambayo yamezungumzwa. Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ameweka wazi kwamba wakati Muswada huu unajadiliwa, *in the course of discussion*, likatokea sasa suala hili ambalo ameliweka vizuri Mheshimiwa Mnyika na wenzake wamezungumza hapa kwamba je, ni wapi ambapo inatamkwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge wenzangu, sisi tulipo katika Serikali za Mitaa tunapomsikia Mheshimiwa Mkulo anasema haya anayoyasema kuhusu utaratibu ambao utawekwa katika kanuni wa namna sasa ya kupitisha hizi zabuni, nataka niwaambie tunafurahi na tunashangilia sana. Hapa kinachozungumzwa, ukiangalia huu ukurasa wa 35, ambao ninafikiri Mheshimiwa Mnyika, amezungumza hapa; anasema kipengele kile, *Part IV: Institutional Arrangements*, kile kipengele cha (3), "*The composition of local government authority tender board and the method of appointment of the members, and the procedures to be followed by such a tender board, shall be prescribed in Regulations made pursuant to the provisions of the Local Government Finances Act.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa maana yake ni nini? Najua anachosema ni kwamba, sheria *i-command* pale iseme kwamba huyu atakwenda kufanya hivyo na ndivyo tunavyotegemea. Sisi tutuwa sasa na kanuni ambazo zitatamka mle ndani kwamba sasa na labda nieleze kidogo kwamba ilikuwaje; Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, alikuwa anamteuwa mmoja wa wakuu wa idara anakuwa Mwenyekiti wa Bodi. Na Katibu wake anakuwa ni yule anayeshughulika na mambo haya ya manunu, ambaye ni Ofisa huyu wa manunu ndiyo Katibu wake, wanakaa pale wanapitia pamoja na injinia na zile *engineer adjustments* na kila kitu kimefanyika. Wakikaa mle ndani wakimaliza, wanatoa wanakabidhi; wakati huu na ma-*BoQs* yote yameshatengenezwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenyekiti wa Halmashauri ambaye ndiye anatamkwa na Sheria, angalia Ibara ya 145, 146, ambayo inatoa madaraka kwenye *Local Government*, anakwenda katika kijiji au katika Kata anakuta vijiko viro kule vinazunguka namna hii, yeye mkataba ule hajasaini wala hajafanya kitu chochote! Wanaofanya maamuzi katika Halmashauri ni Baraza la Madiwani. Wale wengine wote Wakuu wa Idara na watumishi wengine, kazi yao ni

kushauri Baraza la Madiwani ili lifikie maamuzi sahihi. Wenye *mandate* na *power* ya kufanya maamuzi katika Halmashauri, sio Wakuu wa Idara. Wakuu wa Idara wanakutana katika kitu kinachoitwa *Council Management Team*. Mle ndani ndipo wanaposema kila kitu, wanaangalia masuala ya sheria, wanaangalia taratibu, wanaangalia kila kitu, wakimaliza hao kwa maana hii niyozungumza hapa, hii inakwenda katika *Tender Board*; mle ndani hakuna Diwani! Mle ndani hakuna Diwani yejote anayeingia mle ndani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenyekiti wa Halmashauri anatamkwa katika Sheria namba 7 na Sheria namba 8 kwamba, mkataba wowote utakaingiliwa katika Halmashauri, hata kama Mwenyekiti hakuwepo, atakayesaini mkataba ule sio Mkuu wa Idara ni Mwenyekiti wa Halmashauri ambayo ni mmoja wa Madiwani katika Halmashauri inayohusika. *That is the bottom line, otherwise huna kitu kinachoitwa Local Government. We are talking about decision making* hapa; wanaofanya maamuzi ni Baraza la Madiwani, lakini kinachotokea ni nini? Atakwenda kukutana na Mwenyekiti wa Halmashauri katika Kamati ya Fedha, Uchumi na Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kama iliyovoleza hapa *already* maamuzi yameshafanyika, wamekwenda, wamesha-*award* na kila mtu yuko kule! Ndiyo maana unatuona tunapotoka hapa tukienda sisi katika vijiji, tukienda katika Halmashauri, tunadai *BoQ*; *BoQ* itakuambia kama hapa watatumia mabati *gauge* ya 28, itasema mle ndani. Lakini *by that time it is too late*, mkataba umeshaingiwa! Mwenyekiti wa Halmashauri anakwenda pale anasaini pale, habari imekwisha. Huu Muswada unaokuja hapa leo, unataka kuondoa hiyo; unasema hivi, hata kama mmekutana kwenye *Tender Board*, hamtaweza kuitisha maamuzi haya kwa maana ya mabadiliko haya yatakayofanyika mpaka Kamati ya Fedha, Uchumi na Mipango, ambayo Mwenyekiti wake ni Meya au Mwenyekiti wa Halmashauri wakae waseme tunakubali. Hataweza tena, hatapita mahali popote! Na sisi tunamuomba Mheshimiwa Mkulo, haraka haraka kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, tuleteeni hizi kanuni sisi tutakwenda kuzibadilisha na taratibu zetu zitabadilika na kama zinakinzana na sheria ya nchi, tutaleta hiyo sheria hapa na wenye mamlaka na madaraka ya kuitisha hiyo Sheria ni Bunge hili lilloko hapa. Hilo ni la kwanza hilo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, imezungumzwa hapa habari ya *the lowest bidder*; ukitoa kazi hapa nitoe mahesabu ya chini tu nikasema kazi hii "A" amesema atafanya kwa shilingi 50,000/=, "B" atafanya kwa shilingi 30,000/=, "C" atafanya kwa shilingi 20,000/=, *the lowest bidder* pale ni shilingi 20,000=/. Hatuishii hapo, tunapekenya huyu aliyesema shilingi 20,000/= atanunua vifaa hiyo kwa bei gani? *Gauge* ya 28 ya bati imefika shilingi 20,000/=, *the lowest bidder* hapa akisema kwamba nitatengeneza mimi hapa nitaweka bati la shilingi 15,000/= hapa Dodoma tutamuuliza hili bati unalipata wapi? Ndiyo maana kimewekwa kipengele kinasema *the lowest evaluated bidder*; kwa maneno mengine yule wa shilingi 30,000/= aktiuambia bati nitanunua kwa shilingi 20,000/= na sisi tunajua ndivyo yanavyopatikana, *the lowest evaluated bidder*, sio shilingi 20,000/= ni shilingi 30,000=/. Huyu wa shilingi 20,000/= unataka ku-exit aingie pale apate ile baadaye atuchakachue aende sasa akanunue *gauge* ya 30!

Mheshimiwa Mwenyekiti, *gauge* ya 30 inauzwa shilingi 12,000=/. Kama yule ame-*quote* kule shilingi 20,000/= maana yake shilingi 8,000/= zimeondoka, zidisha mara mabati 10,000 yanayowekwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Bahi, natoa mfano tu, hilo jambo haliwezi kupita tena hapo! *The lowest evaluated bidder* hapa ni yule ambaye tumechunguza tukaona kwamba huyu sio kwamba anafanya ujanja tu hapa unataka kuingia ili apate, maamuzi yafanyike hapa hapa.

Kwa hiyo, tukikuta kwamba anasema atanunua mabati kwa shilingi 15,000/= *gauge* ya 28, tunajua huyu ni muongo! Huyu atakuja kutuchakachua tu. Kwa hiyo, *the lowest evaluated bidder*, maana yake ni lazima twende tupitie kipengele kwa kipengele tumekipitisha pale tuseme palepale. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka niseme kwamba sisi tumejiandaa vizuri. Nchi hii haiwezi kuchezewa, Halmashauri haziwezi kuchezewa hapa, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mliopo hapa tunawaombeni fanyeni haraka haraka pitisheni huu Muswada, sisi tutakwenda kufanya kazi hiyo na hatutawaangusha. Hatutawangusha, nataka niseme hilo ili tuliweke vizuri kabisa; haiwezi kuchezewa chezewa tu hivi hivi, watu wanapita pale. Suala la *language*, hili ni

suala linalohusu watu wanaita *solicitor*, *solicitor* ni Mwanasheria. Mwenyekiti hakusoma habari hiyo na wale wenzake wote hawakusoma habari hiyo, lakini hawesi kusaini mkataba ule mpaka Wanasheria wa kwake wa Halmashauri, waketi chini waangalie *implications* zake! Sasa unakutana na Mwenyekiti pale, Mwenyekiti, Mbunge au Diwani, hakuna mahali alipodaiwa kwamba asome awe na *Masters* na *Ph.D*, kama anazo ni *advantage* kwa Halmashauri. Lakini *it is not a prerequisite, it was not a requirement*, ni ajue kusoma na kuandika kwa Kiingereza au kwa Kiswahili. Sasa inapokuja pale mimi mambo ya mkataba nayafahamu hapo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunachosema hapa wale Wanasheria wa Halmashauri wao ndio wanaotakiwa waupitie huu mkataba, wauangalie. Waangalie unasema nini, wacheki mle ndani, kama kuna mahali ambapo tunaitumbukiza Halmashauri, *wana-refrain*, wanaacha kuingia katika mpango huo. Kwa hiyo, sisi tunachosema hapa, Wanasheria wetu watumike katika Halmashauri kuhakikisha kwamba, mikataba ile ambayo inaingiwa katika Halmashauri, mikataba hii haichezewichezewi kama tulivyoeleza hapa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia *Controller and Auditor General Report*, na Mheshimiwa Dokta Augustino Mrema anajua Mwenyekiti wa *Local Authorities Accounts Committee* najua ananisikiliza hapa. Mambo ya ajabu ajabu haya yanafanyika katika eneo hili tunaloofanya; *for your information 70% ya mapato yote ya Halmashauri, yanapitia kwenye Procurement Unit, Kitengo kile cha Manunuzi*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia hakuna ugomvi hapa ni msisitizo tu hapa kusema kwamba Waheshimiwa Madiwani tusaidieni. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusaidieni hapa twende tukanyooshe hii habari, sisi tukitoka hapa tukitumia hiki kipengele tukienda kule Mheshimiwa Mkulo na sisi tukabadihisha hizi taratibu hapa hatoki mtu hapa, halafu akatuambia kwamba alipitisha tu hivi hivi, wanafanya nini wakati mwingine siri zinakatwa kule wanajua mle ndani nini kimeandikwa mle ndani wakiangia mle ndani wakati mwingine unakuta wengine wanaochukua kazi ni wale wale wanaofanya kazi pale na vitu vingine, na hili nalipeleka katika mada yangu ya mwisho. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuseme kitu chochote tunachotaka kuzungumza humu ndani kama nchi hii ya Tanzania haitakuwa na wenyewe wa kufikia tunga sheria mahali popote ni kazi bure. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno yaliyosemwa hapa ya uadilifu, maneno ya uzalendo, nchi yetu ya Tanzania haiwezi ikatafunwa tafunwa tu hivi na sisi tumekaa hapa, tumepewaa madaraka na mamlaka ya kuja kukaa hapa kuhakikisha kwamba tunadhibiti hela za Serikali na wananchi zisiliwe. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila jambo *engineer* wetu aliyepo kwenye kitengo cha manunuzi, Mwenyekiti wetu, Madiwani wetu kwanza wataweka mbele moyo wa kizalendo nchi hii kama haina Madiwani, haina Wakuu wa Idara, haina Wakurugenzi, Mawaziri, Wabunge amba wako tayari kuifikia Tanzania ni kazi bure. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanafunzi wa Sheria aliulizwa *what is law*, akajibu *law in simple common sense* akajibu hivyo. Maana yake nini hapa na akina Mnyika nyie mnafahamu kwa sababu mmesoma, mimi ni *political science* na *public administration, common sense* inatupeleka kwamba lazima tuenze kuzuia kila mianya iliyopo pale baada ya hapo tutaweka moyo wetu pale, *engineer* anayetufaa ni *engineer* anayejua kwamba hapa zege likorogwe kiasi hiki, lakini *engineer* huyo huyo lazima tupime moyo wake wa kizalendo katika kujenga nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa nasema kwa niaba ya Serikali tunawaomba Waheshimiwa Wabunge, tusaidieni kupitisha jambo hili halafu baada ya hapo kama tutawaangusha mje mtuulize sisi, sisi tunaona tu mambo yanafanyika kwenye Halmashauri kule yanafanyika anakuja kijana anakwambia mzee soma sheria imeniambia, nimemteue mtu, Mwenyekiti wangu ni huyu, Afisa Ushirika nimeweka pale wamepitisha, unanyamaza kimya wewe ni mtu mzima unakwenda pale unapewa pale, unanyamaza kimya, unatoka kimyaa, sana sana

zile zingine ni fujo tu tunafanya pale fujo, mtu anakuambia mimi nililetta kitasa hapa kinaitwa *yaya* mbona hakikuandikwa hela, kilikuwa kimeandikwa kwenye *box* majibu ya namna hii tuyakatae kwenye sheria hizi, mambo ya kujenga hapa majengo watu wanatuwekea hapa mambo ya ajabu ajabu tukatae tupitishe hii sheria ili tuende. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu la Siha, mimi naunga mkono hoja hii nawaomba Wabunge tupitishe jambo hili.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango huo Mheshimiwa Mwanri, umezungumza leo *ki-back bencher*, safi sana. Sasa nimuite Mheshimiwa Nundu...

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Sina muda rafiki kabisa, sina muda kabisa unisamehe ndugu yangu Mheshimiwa Nundu, Waziri wa Uchukuzi huyu ni bingwa wa masuala ya usafiri wa anga, tunaomba mchango wako. (*Makofi*)

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili nami kama walivyofanya Wabunge wengine nichangie katika Muswada huu. (*Makofi*)

Kabla sijaingia kwenye mada yenyeWE rasmi naomba pia nimshukuru ndugu yangu Waziri wa Fedha, wasaidizi wake wote Naibu Mawaziri na wafanyakazi kwa kutuletea Muswada huu ambaao ni muhimu sana, ambaao kiini chake hasa ni kuleta jinsi ya kudhibiti manunuzi ya Serikali pamoja na taasisi zake zote, huu udhibiti ndiyo kiini cha Muswada huu. Na mimi ninavyoupitia pamoja na hoja nyingine ambazo zimetolewa, pamoja na ushauri mwiningi ambaao Wabunge wengine wametoa naona sheria hii ikikubalika sasa udhibiti huo utafanyika. Nyezo ya kufanya udhibiti tunayo, kilichobaki sasa ni kama walivyosema Wabunge wengi moyo wa kizalendo, utendaji kazi na kuiangalia nchi yetu inakwenda wapi, hilo ndiyo linalotakiwa ili kile ambacho kiko katika sheria hii sasa kifaniwe kazi. Vyombo vinavyoongelewa hapa katika kununua ni vyombo vipyta na vyombo viliviyotumika, siyo vyombo viliviyotumika tu peke yake sasa udhibiti huu ni wa vyombo vipyta na vyombo ambavyo vimetumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea pia niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ambaao imeupitia na ikauboresha mpaka ukafikia hapa ulipo. Nami kama Wabunge wengine nawaomba tuwe waangalifu na weledi ili tufanye maamuzi ya kupeleka mbele Taifa letu siyo maamuzi ya kuduwa maendeleo yetu. Leo tuna nafasi hapa ya kufanya kitu ambacho tukikipitisha tutakuwa tuna nyezo ya kuifanya Serikali ifanye kazi vizuri katika kupeleka mbele nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na tufanye hivyo kufanya maamuzi bila woga kwa sababu ambazo hazipo, tufanye maamuzi ya kina ili twende mbele. Kuna masuala ya udhibiti utafanyikaje udhibiti huo tumelezwa hapa kwenye Muswada sehemu mbalimbali ambazo zimepewa madaraka ya kufanya udhibiti. Sasa niangalie katika ile ngazi ya Halmashauri ambapo Madiwani sasa wanapewa meno ya kuweza kusimamia maamuzi ya ununuzi kule. Lakini pia katika taasisi nyingine hilo limeelezw, sasa mimi sitaki kuliongolea hilo zaidi, nataka niende kwenye kile kipengele cha 66 na hasa kile cha 65 ambacho kinahusu ununuzi wa vyombo maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzuri wa Muswada huu, ukiachia kule nyuma tulipokuwa tunafanya shughuli hizi hakukuwa na *definition* ya vitu gani ambavyo tunatakiwa tufanye maamuzi maalum.

Sasa Muswada huu unatupa sasa badala ya kuyumba yumba unanunua *refrigerator* ununue la zamani au jipya, unanunua magari ununue ya zamani au mapya, ununue mitambo ya umeme ya zamani au mipya na tumeona tulivuosua sua katika mitambo ya *DOWANS* na mwisho

hatukuweza kununua. Ununue hata vichwa vya treni, vya gari moshi vya zamani au vipyta vilikuwepo hapa vya *RITES* vimetumika dakika za mwisho tuvinunue au tusivinunue hatukuvinunua. Badala ya kusuasua, hapa tunaelezwa kinaga ubaga ni vitu gani ambavyo vinatakiwa viangaliwe tunapoangalia kununua vifaa ili Taifa liende mbele, zimetajwa ndege hapa, zimetajwa gari moshi, vichwa vyake pamoja na mabehewa na zimetajwa meli, wazi kabisa. (*Makofi*)

Sasa vitu hivi vinakuwaje, ukiangalia meli na ndege na kwa sisi Tanzania hata gari moshi kwa sababu reli ya *TAZARA* inatumia Tanzania na Zambia, hivi vitu katika matumizi yake vipo katika mantiki ya Kimataifa. Ndege zinatumiwa na Mataifa kwa pamoja, ndege inayotoka Ufaransa kuja hapa na inayotoka hapa kwenda Ufaransa inahitaji kanuni zile zile, *whether inatumiya Ufaransa ama inatumiya Tanzania, meli vivyo vivyo*. Sasa mimi kwa kulieleza kwa undani nataka njikite kwenye mambo ya ndege, ndege ubora wake kwa sababu *Wabunge* wengine nimeona wasiwasi wao ni kuwa hivi vitu vikinunuliwa basi vinaweza vikatuleta majanga, nataka niliweke wazi, ndege ubora wake ni kwa sababu zinaangaliwa na kutunzwa siyo tu katika ngazi ya Kitaifa lakini pia ngazi ya Kimataifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kila nchi kuna kitengo ambacho kinahakikisha kuwa ndege ni salama na katika ngazi ya Kimataifa, kuna kitengo ambacho kinahakikisha kuwa siyo ndege tu kama ndege lakini usafiri wa anga kwa ujumla wake ni salama. Kule katika Shirika la Kimataifa *ICAO* wana vitengo tunaita *Annex 18* na sasa hivi wanaanzisha cha 19; kila kitengo kimoja ni ma-book makubwa yanakueleza kile ambacho unatakiwa ufanye katika usafiri wa anga katika kutengeneza ndege hata jinsi ya kuongea wewe *pilot* ukiwa kule mbele unaongea. (*Makofi*)

Sasa niache hilo la jumla nije kwenye hizi ndege, ndege kila inapotua inafanyiwa *check* tunaita *turn round check*. Kila ikilala asubuhi ianze tena usiku ule inafanyiwa *check*, tunaita *night check* kila baada ya miezi au saa kadhaa nyingine ni 345 ndiyo inafanya *check* ambayo ameisema ndugu yangu Mheshimiwa Serukamba jana. *Certificate of maintenance* lazima ifanyiwe hiyo na kila mwaka inafanyiwa tena *check* kubwa inayoitwa *certificate of air worthiness*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kila kipindi cha miaka labda minne inafanyiwa *C check*, na ikifika miaka 24 inafanyiwa *D check* kubwa inatolewa kila kitu inarudishwa upya, sisi wataalam, mimi ni *Electrical Engineer* kwa hiyo huku ndiko nilikokulia miaka 38 nafanya shughuli hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndege haina umri wa mwisho, kitaalam ndege haina umri wa mwisho, ukiona ndege inatolewa inaambiwa isiendoolee ni kwa kuwa tumebadilisha mfumo tumeweka kompyuta ma-*pilot* waangalie, *engine* tulizokuja nazo sasa ni bora zaidi ndiyo 707 yanatoka hayo lakini ndege kama ndege haina umri wa mwisho, unaweza kuitumia na kuitumia kinachotakiwa hizi kanuni za utaratibu za utengenezaji wake uwe unazitekeleza, ukitekeleza hilo ndege haina umri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo wenzetu Msumbiji kule wakati tuna *Boeing 737* hapa mwaka 1978, walikuwa wameshazinunua mpaka leo zinatembea zina miaka karibu 40. Hata mashirika haya makubwa unayoyasikia *Air France*, wastani wa ndege walizonazo zina umri wa miaka 20 ndiyo kusema zingine zina miaka 30, nyingine zina miaka 10, lakini wanatengeneza vile inavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuwa inatengenezwa hivyo unakuta ndege ambayo ipo Ufaransa inatumika kama ingekuwa ipo Tanzania inatakiwa kwa umri wowote iliyo miaka 20, miaka 25 iwe ni sawasawa ndiyo maana katika usafiri wa anga unakuta Mashirika ya Ndege yote dunia nzima wanakodishana ndege na wanauziana na ndege hakuna hata nchi moja ambayo haiuziani na mwenzake ndege hizi ambazo zimetumika, dunia nzima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nitoe mifano ambayo ni michache tu hii maana yake ipo mingi, *British Airways* ndege zao umri wao *average* ni miaka 20, Lufthansa ndege zao za 737 umri wao ni miaka 21, Kampuni nyingine ambayo ipo Uingereza ilinunua ndege tarehe 25 Machi, 1994, na tarehe 1 Oktoba, 2006 ikauzia *Star Peru, Virginia Atlantic* ilikuwa na *air bus 340* iliyonunuliwa

tarehe 21 Januari, 1994, tarehe 25 Januari, 2004 ikauzia *British West Indian Airways*, Virginia hiyo, ndege hii ya 340 nyingine ya tarehe 24 Oktoba, 1994 waliiiza wakauzia *Fin Air* tarehe 19 Juni, 206, 747 ya ndege hiyo hiyo iliyonunuliwa tarehe 12 Juni, 1993 walipomaliza kuitumia kwa miezi michache wengine wakainunua *Air Newzland* tarehe 1 Novemba, 1993, hata *Kenya Airways* hapa walikuwa na *Boeing 767* walionunua tarehe 24 Desemba, 2001, tarehe 10 Juni, 2005 wakawauzia *Air Canada* ni nyingi *list*. Kwa hiyo, ninachotaka kusema hili siyo suala jipy, sisi tukisema Mashirika yetu hapa ya Serikali yasinunue ndege ambazo zimetumika, ni kuwa tunakuwa tuko peke yetu katika hilo, siyo mfumo wa dunia. (*Makof*)

Sasa athari zake ni nini, athari zake tuingalie *Air Tanzania* hapa mwanzo nilifarjika sana, kila mtu akisimama tunataka *Air Tanzania* mimi nilikuwa nakaa hapa siyo kuwa nilikuwa na wasiwasi yaani nafurahi tunataka *Air Tanzania* yetu, kwa sababu bila *Air Tanzania* hapa hakuna usafiri wa anga ambaao utachanganya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaosema leo kuwa usafiri wa anga ni *luxury*, usafiri wa meli ni *luxury*, usafiri wa reli ni *luxury*, mimi ninawashangaa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafiri wa *luxury* ni wa gari moja moja ambazo upo wewe peke yako unaendesha hapa siyo usafiri huo, safari hizi zinatakiwa zichanganye nauli ikirudi chini utakuta kuwa usafiri wa anga ni muhimu sana wa kumtoa mtu Kigoma akafika Dar es Salaam kwa saa tatu badala ya kuchukua muda mrefu nyumbani. Na ni nani ataufanya usafiri huu uwe siyo *luxury* ni *Air Tanzania*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hatuwezi hapa tukamwambia *Air Tanzania* akiona kuna ndege ambayo inafaa imetumika, imetumiwa na wenzao ambaao wangeweza kuitumia zaidi tumwambie wewe huwezi kununua, lakini shirika lingine la mtu binafsi hapa linaweza kununua ndege hizo na kuzitumia hapa hapa, tunaifanya nini *Air Tanzania*? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnaniambia tunataka *Air Tanzania* ifaulu iende mbele ndiyo hivyo, angalia *Air Tanzania* inavyoweza kukufanya sasa hivi ndege wanazotumia *Air Tanzania* siyo mpya, zile *dash eight* zimenunuliwa ndege ambazo zilikuwa zimeshatumika, lakini kule tulikuwa hatujui sasa sheria inatuambia wazi wafanye hivyo. Na hizi ndege ndiyo juzi ya Tanzania imeanza kwenda Kigoma hapa, mmelalamika hapa nakumbuka ndugu zangu wengine wakasema Dar es Salaam mpaka Kigoma wanalipa shilingi milioni moja nauli, *Air Tanzania* imeingia nauli sasa hivi ni shilingi 342,000/. Kwa sababu hiyo wengine pia wamepunguza bei, *Precision Air* yuko kwenye shilingi laki nne na kitu, wengine wako shilingi laki tano wanapunguza bei na ni *Air Tanzania* ndiyo anaweza kuwafanya hawa watu wakapunguza bei. (*Makof*)

Ndugu zangu haya mambo tuyaaingalia kwa ufanisi wa nchi yetu, ndege ambazo ni za kukodisha sheria hii hamzui *Air Tanzania* kufanya kinachomzuia ni kununua ndege siyo kukodisha ndege, mifano mingi imetolewa ya matatizo yaliyotokea huko katika mifano hiyo yote *Air Tanzania* haikununua ndege, ndege ya *George Hillac Boeing 707* na *Boeing 27* zilikodishwa, ndege ya *Air Bus 320* ambayo imekaa huko imekodishwa na unapokodisha utakutana na wakodishaji ambaao wanawenza kukutia kwenye matatizo. Sasa ile sheria nilyosema ambayo sisi tunaifuata kinchi na inaangaliwa na Kimataifa ndiyo illitufanya sisi 707 tukazi-ground baada ya kuruka kwa miezi kadhaa. Kwa hiyo, ule usimamizi upo, mnajua wenywewe hapa mwaka 2008... ilikuja hapa katika kuangalia tunafanyaje, *Air Tanzania* ikaonekana karatasi tu hazikukaa vizuri wakanyang'anywa *Air Operator Certificate* tangu mwaka 2008 juzi ndiyo tunawarudishia, wasimamiaji wa kuhakikisha kuwa hivi vyombo vinaruka kwa usalama wanaifanya kazi nataka kuipongeza *TCAA* kwa hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuwapongeza pia *SUMATRA* kwa hilo kwa kuangalia mambo ya meli na reli. Sasa baada ya kurudishiwa *Air Operator Certificate*, mnajua tangu mwezi wa pili mpaka leo juzi tu tarehe 1 Novemba, *Air Tanzania* ndiyo imeanza kuruka, zile ndege siyo kuwa ni mbou, zile ndege walikuwa hawawezi kuzitumia kwa sababu hazikukidhi zile taratibu za kuziangalia za kuzitunza, siyo kuwa mbou. (*Makof*)

Kwa hiyo, hakuna ndege itakuja hapa iwe ni ndege chakavu hapa tutaleta ndege ambazo zimetumika vizuri, vimetunzwa vizuri kama kianzio cha kuhakikisha kuwa usafiri wa anga ukichochewa na Air Tanzania unaenda mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungkuwa tunazo pesa watu wanasema matajiri, nchi yetu ni tajiri ndiyo hatujafika bado wakati wa kuweza ku-exploit utajiri wetu kikamilifu, wakati utafika tutajigamba na sisi tutaweza kufanya makubwa, na katika kufikia huko na kuanzia hivi vyombo vyta kuchochea usafiri sasa hivi vifanye kazi. Leo hii mabehewa ya mizigo yamekaa, reli yetu hii mabehewa yanayohitajika *local motive* zinazohitajika ni *local motive* zinazotumia *gauge* hii iliyopo, utatoa wapi duniani sasa hivi hizo *gauge*.

Kuna mahindi yamejaa kule Mpanda, ndugu zetu wanakufa njaa, tunahangaika kutafuta *local motive* itoe mahindi, watu wakale mtu anasema usiende ukachukua *local motive* ambazo zimeshatumika, kuna *local motive* hapa hapa wametumia *RITE*, mtu binafsi akija anatumia tunaangalia tunakubali, *RITE* ametumia hapa, 15 yapo tunasuasua tufanyaje, watu binafsi wanataka wayanunue hao wanaweza kuruhusiwa kununua, tukiingia nao ubia kutumia reli, wanayatia kwenye reli hiyo halafu mnasema haya yataleta vifo, vifo vinakuja tu wakati Air Tanzania imenunuua ndege iliyotumika? Au wakati tu *TRL* imetumia *local motive* na mabehewa yaliyotumika au kampuni yetu ya meli imenunuua meli zilizotumika, vifo havitokei wakati watu binafsi wamenunuua vitu hivyo hapa ni nani anawatumika? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nani anawatuma hapa kuja kubabaisha watu hapa, nani anawatuma msjidai hapa kusema hawa wamekaa hivi ninyi wengine mnatumwa. Baadhi yenu hapa tukiwasikia lugha tunawasiliza tu lakini mnatumwa, kwa sababu wale wataokuja watu wataleta ndege mpya kutaka kubabaisha... (*Makofi*)

(*Hapa kengele illilia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja, tungeangalia mambo ya magari, tungeangalia kwa ukubwa wetu, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umekwisha. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, mtaamini kwamba leo tumemuona Mheshimiwa Omar Nundu *original*, ye ye ni mtaalam, hakuna nchi hii anayeweza kumbishia kuhusu masuala ya anga na amefanya kazi kwa vitendo, uzoefu wake umejaribu kuweka mchango ambao unaweza ukatusaidia wakati tunapoendelea kwenye mchakato wa mwisho wa kwenda kumalizia kutunga sheria yetu.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Nichukue nafasi hii muda umekwisha, nichukue nafasi hii kuwajulisha tu kwamba jioni tutakaporudi basi tutaanza na watoa hoja kwa namna ambavyo wamejipanga na baadaye tutaendelea na hatua zinazofuata. Baada ya haya naomba kusitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja jioni.

(*Saa 7.00 mchana Bunge lilsitishwa mpaka saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilitrudia*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kwamba mchana wakati tukahirisha Bunge, tulisema tukifika jioni tutaendelea na hatua za mwisho za kumaliza Muswada huu. Lakini kwa mamlaka ya Spika ameniomba niwatangazie kwamba kwa sababu mjadala ni mzuri, michango inayotolewa ni ya afya kwa maslahi yetu, ili Sheria yetu tunayoitunga iweze kuwa nzuri, basi wachangiaji waliokuwa wamebaki na wenyewe tumalize kabisa ili tuweze kupata michango

mingi ya kutosha ili pamoja na mambo mengine itusaidie katika kutengeneza Sheria nzuri zaidi na kwa hiyo, *winding up* ya Muswada huu itafanyika siku ya Jumatatu baada ya maswali na majibu.

Kwa sababu hiyo basi, naomba niruhusu kwa wachangiaji waliokuwa wamebaki tuendelee kuchangia kwa nguvu zote ili tupate michango mizuri zaidi na tutengeneze Sheria nzuri kwa maslahi ya Taifa na Watanzania wote kwa ujumla. (*Makofi*)

Basi tuendelee na mchangiaji wetu wa kwanza kwa jioni hii atakuwa ni Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Sanya, karibu!

#### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 68(7). Wakati unaahirisha Bunge mzungumzaji wa mwisho ambaye alikuwa ni Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi alipokuwa anahitimisha hotuba yake ama hoja zake alisema wanaopinga Muswada huu ni kwamba wametumwa. Mimi nakiri wazi kabisa kwamba ni kweli tumetumwa na wananchi sasa tunataka tutambue na atueleze ni nani aliyetutuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Mwongozo nitautoa baadaye, tuendelee Mheshimiwa Sanya!

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie mawili au matatu niliyokuwa nayo kuhusu Muswada ambao tunakwenda nao sasa hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatozo kubwa ambalo tunalo nchini mwetu Tanzania tumefikia mahali tunaviogopa vivuli vyetu wenye, namna gani? Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere alisema kwamba unapoanza kula nyama ya mtu hutaishia hapo utaendelea kula nyama ya binadamu. Kwa nini nikasema hivyo? Kwa sababu kitu chochote kinachohusiana na fedha katika nchi hii kitakapoletwa au kinapoletwa katika Bunge letu kinatia wasiwasi kwa Wabunge na raia wa nchi hii. Sasa tujulize nani aliyetufikisha hapo? Aliyetufikisha hapo ni ulafi, uzembe na wizi unaofanywa na baadhi ya viongozi wasiokuwa na imani na wananchi wa nchi hii. (*Makofi*)

Hii nchi ni maskini lakini nchi ni tajiri, utajiri wake uko wapi? Utajiri wa nchi zetu kama hizi za ulimwengu wa tatu hasa Afrika ni kuthamini tulichokuwa nacho tukakitumia vizuri na madaraka yetu tukayatumia kwa ajili ya manufaa ya walio wengi ambao ni wananchi walalahoi waliokuwa hawajui, wanalala vipi na wanaamka namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema hakuna kitu kitakachotukomboa sisi Watanzania kama uaminifu, tukishakuwa waaminifu tukajenga imani kwa wananchi wetu basi moja kwa moja tutaaminiwa na hata hakuna mambo mengine yatakayokuwa na haja ya kuyaleta katika Bunge hili. Leo tunasema kwamba huu ni Muswada wa *Procurement*, ni mzuri tu hata huu ambao ulipitishwa huko nyuma ulikuwa ni mzuri tu, wabaya ni sisi viongozi tunaosimamia matumizi ya nchi hii. Kama sote kuanzia Wabunge, Wakurugenzi, Makatibu, Mawaziri na viongozi wote tukadetermine kweli kweli kwamba sasa tuwe kitu kimoja, tukomboe uchumi wa nchi basi nchi hii itakomboka wala si muda mrefu, ni determination tu kama tukiamua. Lakini juu ya yote hayo, bado tutatunga sheria na watu watavunja sheria na hawatachukuliwa sheria na watu watakula uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu cha *Public Procurement*, ukurasa wa 38 functions and powers of the accounting officer, mimi naona hili kidogo linanitia wasiwasi kwenye vipengele vya (b) na (e).

Kipengele (b) inasema; "appointing the members of the tender board specified in the Second Schedule" yaani iwe chini ya Accounting Officer, na (e) inasema; "appointing the

*evaluation committee and negotiation team*", mimi naona hapa kuna kasoro kidogo. Lazima hizi nafasi ziwe zinakwenda kwa mujibu wa namna tutakavyokuwa tunaamua kutenda namna gani katika hii *procurement*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka nilizungumzie ni *PPRA*. *PPRA* waongezewe Bajeti kwani wanafanya kazi vizuri tu. Kwa hiyo, waongezewe Bajeti ili wafanye kazi vizuri na manunuzi yote ya ndani na ya nje ambayo yanawezekana kufanyika mikoani basi tuyapeleke mikoani, tukiyaacha yote yawe Dar es Salaam yanazidisha gharama na yanazidisha njia yene harufu ya manunuzi ambayo hayaendani sambamba na uhalali wa manunuzi hayo. Hapa ndiyo ndiyo ile *D by D* itakapofanya kazi, ni sera nzuri lakini iwe *implemented* ili ifanye kazi huko mikoani.

Sasa watu wana wasiwasi na lazima tuwe na wasiwasi, kwenye *emergency procurement*, mimi nasema tusiwe na wasiwasi kiasi hicho lakini lazima iwe ni *emergency* kwa maana ya *emergency*. *Emergency* iliyokusudiwa hapa iwe ni kweli *emergency* isije ikachukuliwa hii *emergency procurement* ikawa ni *emergency* ya kutafuta njia watu kula mapema. Kila Mtanzania anataka kula mapema lakini tunachokitafuta sasa ni upatikane uhalali wa kununua bidhaa kwa fedha halali na fedha ambazo zinakwenda sambamba na manunuzi hayo ambayo yamefanya.

Leo tunasema kwamba Madiwani washirikishwe kwenye Halmashauri, *well and good* wala hakuna tatizo, lakini je, tumejipanga kuwapa elimu Madiwani hao? Madiwani hao tutakuja kuwatwika mzigo hawauelewi, matokeo yake watakuja kuwa *over powered* na viongozi wengine katika hizo Halmashauri, waboronge na wakishakuboronga waje wakamatwe Madiwani. Madiwani lazima wasomeshwe, wapewe elimu na waelewe nini *procurement* katika Halmashauri zao, na zipo Hazina ndogo mikoani, haya madaraka yapelekwe katika hizo Hazina mikoani kuliko kusema kwamba kila kitu kinafanyika Dar es Salaam, kila kitu Makao Makuu na kila kitu *accounting officer*, hapana!

Mimi ninavyoolewa hili suala la kwamba tunanunua vitu chakavu kila mmoja ana tafsiri zake, lakini tafsiri za kisayansi unapokwenda kwenye chakavu haina maana kwamba unakwenda kununua kitu kilichoza au ambacho hakifanyi kazi. Dunia nzima na Mashirika ya Ndege yote hayanunu ndege mpya, *it is too expensive*, lakini dunia huwa wanafanya *leasing* kwenye ndege na ndege zina taratibu zake usifikiri zinanunuliwa kama gari la *Toyota* au *Land Cruiser*.

Ndege zina viwango vinavyosimamiwa na *IATA* yaani *International Air Traffic Association*, lazima kwanza ujunge na hiyo *International Air Traffic Association* halafu wao ndiyo watakaota specification za ndege gani umenunua, kama zinaruhuswa kuruka, zimetumia muda gani kuruka, ziliikuwa *grounded* wapi, zinahitaji vipuri gani ili ziweze kuruka tena la sivyo na wao pamoja na *ICAO* hawakuruhusu ndege yao kuruka. (*Makof*)

Kwa hiyo, sisi kwa kuanzia, mimi sikatai *Air Tanzania* sasa hivi wanajikurupua kurupua na Serikali ya Canada imeonyesha namna gani inaweza kutusaidia baada ya kuona mwamko wa *Air Tanzania* kwamba *they are serious in this business*. Kwa hiyo, tunaweza tukakodi ndege lakini je, wasimamizi au *management*, suala ni *management*. Unaweza ukununua ndege mpya ikakutia hasara na ukununua ndege kuukuu ukawa na *management* nzuri ndege ikakuletea faida. Tanzania tatizo tulilokuwa nalo kwamba unamchukua daktari unampeleka kwenye *management* ya ndege na unamchukua *Engineer* wa ndege unakwenda kumuingiza kwenye Bodi ya kuagiza dawa, *it is nonsense!* Mchukue mtu ambaye analingana na pale mahali. Kwa hiyo, mimi nasema kuhusu uchakavu, Serikali haitanunua magari chakavu wala Serikali haitanunua *motorbikes* mbovu lakini Serikali itakuwa *committed* kununua vitu ambavyo gharama zake ni kubwa kwamba ni vipywa wakakodi vikuukuu...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sanya!

**MHE. MUHAMMED IBRAHIM SANYA:** Yes sir!

**MWENYEKITI:** Umaanisha iliyotumika au chakavu? Maana chakavu na iliyotumika ni tofauti.

**MHE. MUHAMMED IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua Kiswahili kina upana wake. Hata kitu kichakavu nacho huwa kinatumika kwa baadhi ya wakati, inategemea uchakavu wake, wewe unaweza ukakiona kimechakaa kumbe kwa mwenzako ni kipyga na ndyo maana utaona Kariakoo kuna viatu vilivyokuwa vizuri zaidi, chakavu kuliko hata viatu vipyga vinavyotoka Thailand. Kwa hiyo, mimi ninapokusudia chakavu nakusudia uchakavu ambao kwa sisi kwa *grade* yetu tunaweze tukatumia. Kuna watu wanapiga suti humu ukimuuiliza ulipata nafasi ya kwenda Ulaya? Anakwambia *no, just Kariakoo!* Kwa hiyo, ni uchakavu. Ahsante sana. (*Kicheko*)

Sasa ninachotaka kusema mimi hapa ni kwamba Serikali makini kama yetu vilevile izingatie kununua vitu vipyga, nitatoa mfano na nitawapa njia ya kupata vitu vipyga kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti iliopita mimi nilichangia hapa Wizara ya Ulinzi. Wizara ya Ulinzi ilipata dhamana ya Benki Kuu kupitia kwa Wizara ya Fedha na Mheshimiwa Waziri wetu wa Fedha na fikirini ndiye aliye kienda kutia saini mkataba huu tukapata matrekta na vipyga vyake vya mkopo wa dola milioni 20, kama mwongo mnisute hapa! Na tukaambiya tulipe mkopo huo kwa muda wa miaka 25 na miaka 25, miaka mitano ni *grace period* yaani bure hulipi chochote, *the coming 20 years* ambapo tutakuwa awamu ya sita ya uchaguzi wa Tanzania ndiyo tunamaliza deni hilo.

Sasa kama India wameweza kutukopessa vifaa vya kilimo kwa sababu ya *ku-boost Kilimo Kwanza* matrekta na vipyga vyake kwa nini Mheshimiwa Waziri huendi India ukaenda ukakopa vichwa vya treni ili treni yetu ya Kati ikaanza kufunguka? Kweli, *If somebody is ready to give you a socks he can be ready to give you shoes* kwa sababu anajua kwamba akishakupa soksi unahita viatu. Kwa hiyo, kama kakupa trekta rejea mwambie trekta nimeshalimia nina mazao nataka niyasafirisha treni zangu hazifanyi kazi nipe vichwa vitano vya treni. Sijui Waziri wa Uchukuzi atatuambia nini lakini nakumbuka *last five years* kichwa cha treni kilikuwa shilingi 1,000,000 dollars kama kitakuwa kimepanda 1.5 or 2 million dollars, tukipata vichwa 10 sisi reli ya katika mpaka Mpanda, Kigoma na Mwanza itafanya kazi tutakuwa tumejikomboa kiuchumi au tutakuwa hatujajikomboa? (*Makofii*)

#### **MBUNGE FULANI:** Tumekomboka!

**MHE. MUHAMMED IBRAHIM SANYA:** Kwa hiyo, siyo lazima kununua vitu chakavu, muende mkakope na ninarejea tena kauli yangu kwamba Tanzania tuwe na sifa ya kukopa, tusiogope kukopa lakini tuwe na nidhamu ya kulipa. Tukishakuwa na nidhamu ya kulipa Wachina wana fedha hawajui wazifanyi nini, Wahindi wana fedha hawajui wazifanyi nini, hatakupa fedha lakini akikupa *production* yake ina maana *percent* yake inaingia katika mfuko wake wa maendeleo katika nchi yake. Hilo la kwanza.

La pili, hivi sasa mkiangalia televisheni angalieni *Europe inavyo-shake* kiuchumi, tazameni *World Trade Organisation* wanavyofanya kazi za ziada hata kubadilisha muundo wa Serikali zilizopo ili mradi nchi zao zije juu. Sasa nchi za *Europe* zikishakuwa zimepata mtikisiko mjue sisi huku ndiyo tuna *earthquake* kwa sababu sisi tunawategemea wao, Bajeti yetu kwa kiasi fulani tunawategemea wao, misaada yetu tunawategemea wao, bidhaa zetu kwa kuanzia ni wao, kwa hiyo, sisi tuwe makini sana katika matumizi ya manunuzi ili tuweze kuhodhi fedha yetu vizuri tusije tukaipoteza, tukaja tukaingia katika njaa. Kuna hatari hiyo kwani nchi zetu bado ni maskini, hizi *crisis* za *North Africa* za hao Waarabu zimesababisha *petrol* kupanda huku kumetokea *floods* Thailand na *last year* imetokea Pakistan, Vietnam, Indonesia ikapandisha vyakula bei lakini leo Thailand chakula chao hawatauza kwani wao wenye we wanatafuta chakula, tutakuja kununua wapi? Sisi tuna Kilimo Kwanza, tuna pembejeeo, tuna chakula, maghala tunayo, soko lipo lakini hatuuzi kwa sababu gani? Kwa sababu na sisi tunahitaji chakula. Kwa hiyo, sisi lazima tujikite na tuwe waaminifu, tuwapende wananchi wetu na tufanye kazi la sivyo wananchi wataamua kututoa sisi Wabunge na Serikali iliopo ikaja Serikali nyingine mpya *whatever* kwa sababu hatujasimamia maendeleo yao na hicho ndicho kilio cha wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nasema sina tatizo na hii Sheria lakini tuwe waaminifu kwani tukijenga imani za uaminifu tukanunua kilichokusudiwa kununuliwa kwa bei ya soko tutaweza kuhodhi uchumi wa nchi na tutainua hali za watu wetu. Haiwezekani *stationeries*

kwenda kununua kalamu kwa shilingi 1,000/=, haiwezekani *stationeries* kwenda kununua kitu cha shilingi 500/= ukaongeza zero kikawa shilingi 5,000/=, kwa kweli tunawaumiza walio wengi. *Inflation* ndiyo hii tunayoiona namna gani ya ku-control hatujui, Serikali ina mipango gani ya muda mfupi ya ku-control *inflation* sasa hivi haijajulikana, hali ya chakula imepanda, hali ya kipato imeshuka, biashara hakuna, usafirishaji mdogo. Ulaya kuna mtikisiko, Waarabu hawajatengemaa kwa hiyo, tunakwenda kushika wapi?

Tushikamane sisi wenyewe kwa wenyewe yaani sisi kwa sisi tupendane, kama maskini sisi si maskini kuliko maskini waliotuleta hapa, kuna watu wanazaliwa mpaka wanakufa nchi hii hawajui nini kiatu, wewe walau una *pair* tatu, wewe una kigari, wewe unapata mafuta yanatokana na jasho la mwananchi, mwananchi wa kawaida. Tujengeni mipango ambayo itatuletea faida, tuwapende raia wetu, tusiwe tayari kupitisha Miswada halafu Miswada isitekelezwe. Miswada haitakuwa na maana yoyote wala si busara kuja kumfunga Mkurugenzi wa Halmashauri, kumfunga Diwani wala kumfunga Waziri, hiyo bado haijawa heshima ya nchi, lazima tujenge himaya ya kwamba wananchi wanawenza wakajenga imani juu ya watu wao, juu ya Halmashauri yao, juu ya Wizara zao, Makatibu Watendaji, Mawaziri pamoja na sisi Wabunge tuwe kitu kimoja kunyaanya uchumi wa nchi hii. Tuwe kitu kimoja ku-save *single cent, if you have a penny save pound, pound will save themselves.* Lazima tuwe na umoja, imani na ushirikiano na tuondoe rushwa katika nchi yetu tupendane na wananchi wetu wawe na imani na Serikali yao ambayo inatunga Sheria kwa mujibu wa Sheria na kwa maslahi na matakwa ya wananchi waliotuleta hapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Sanya kwa mchango mzuri, sasa nitamuita Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina na baadae Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza atafuata na baadae Mheshimiwa Lucy Mayenga.

Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina!

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwanza nianze kwa ku-declare kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi kwa Bunge hili, lakini vilevile ni Mjumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi wa Bunge la Afrika. Vilevile nataka nilifahamishe Bunge lako kuwa ni miongoni mwa Wabunge ambaao walioanzia uongozi chini kabisa nilikuwa Mtendaji wa Kata. Kwa hiyo Watendaji wa Kata kote Tanzania wajue kwamba wana Mtendaji mwenzao hapa akiyawakilisha, kama ni Serikali za Mitaa nazifahamu kweli kweli, kwa sababu baada ya kutoka kwenye Utendaji wa Kata nikawa Mhasibu wa Halmashauri najua kweli kweli, Halmashauri zilivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo sasa nije kwenye Muswada wenyewe, tunajadili huu Muswada wa Manunuzi ambapo Afrika na Tanzania zikiwa kwenye tatizo kubwa la ufujaji wa fedha, rushwa na ujisadi mkubwa sana. Taarifa ya Mkaguzi zinaonyesha hata kikao kile cha *Fraud and Corruption African Summit 2010* wote walibaini kwamba Bara la Afrika lipo kwenye matatizo makubwa ya rushwa na ufujaji wa fedha.

Taarifa ya *Global Financial Integrity Report* ya mwaka 2008 inabainisha kuwa Tanzania katika kipindi cha miaka 39 kutoka mwaka 1977 mpaka mwaka 2008 imepoteza jumla ya shilingi trillioni 11.6 zikiwa zinaibiwa na Watendaji wa Serikali wanaenda kuficha kwenye mabenki nije ya nchi. Tanzania inabainishwa kuwa nchi ya 13 katika ya nchi 20 zinazofanya zoezi hilo la *illicit financial outflow* kwa kiasi kikubwa, kwa hiyo ni nchi ya 13 katika ya nchi 20 bora kwa ufujaji wa fedha za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunazungumza haya hatuko pahali pazuri pa kujisifu, nchi yetu fedha zimekuwa zikiibiwa, wananchi wanaachwa wanateseka. Kwa hiyo, tunatunga Sheria hii tukiwa na ufahamu wa kutosha kwamba tupo kwenye janga kubwa. Sasa leo sisi kama Wabunge tuhakikishe tunatoka na sheria nzuri ambayo itawapa matumaini Watanzania dhidi ya kulinda rasilimali zao na dunia ituelewe kuwa tumedhamiria kwa dhati kuhakikisha kwamba rushwa itakuwa ni historia tena hasa rushwa ya manunuzi hapa nchini. Nimejaribu kuzungumza sana hili

suala la Waheshimiwa Madiwani kushiriki katika zoezi zima la manunuvi. Katika Kamati ya Fedha tuliona kwamba kuna umuhimu wa kufanya hivyo kwa sababu hivi sasa Waheshimiwa Madiwani wetu wanajikuta wapo kwenye matatizo makubwa wanakuja kulisimia tatizo wakati hasara ni kubwa mno na huwezi kuirudisha, *that is the damage, is beyond repair.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Madiwani wetu wanaingia katika mgogoro huo na kazi kubwa tumewagawia kusimamia kuhakikisha kwamba rasilimali zinasimamia kikamilifu, lakini zoezi zima la manunuvi linafanyika bila wao kushirikishwa. Sasa tukasema kuna suala la *Annual Procurement Plan*, hii *Annual Procurement Plan* sio kwamba haikuwepo, lakini tunataka katika sheria hii, hii *Annual Procurement Plan* itumike kikamilifu kama inavyotakiwa kutumika. Waheshimiwa Madiwani wajiridhishe jinsi manunuvi yao kwa mwaka yanakuwaje. *Procurement Plan* lazima iwasilishwe kwa Waheshimiwa Madiwani katika kipindi cha Bajeti ikiwa na ratiba nzima ya utekelezaji, ikiwa imezungumzia njia gani zitakazotumika katika manunuvi kwa kila awamu kama ni *quarterly* maana yake kila awamu *unit* iliyoengwa lazima njia ya manunuvi itakayotumika ijulikane na mwanzo kabisa kabla ya hapa, lakini vile vile lazima *Bill of Quantity (BoQ)* zionekane mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano katika shughuli za ujenzi lazima uonyeshe kama ni barabara inajengwa, lazima Waheshimiwa Madiwani wafahamu mwanzo kabisa kwamba barabara ya kutoka Ng'oboko ikaenda mpaka Kisesa ina *ma-drift* mangapi yanayojengwa, yatakayogharimu shilingi ngapi, wafahamu kuanzia kwenye *Annual Procurement Plan* na wala sio kuja kuletewa hesabu tu. Lakini vilevile gharama wazijue *from the beginning* na michoro ijulikane *from the beginning*.

Lakini vilevile *tender* ikishakuwa *awarded* na kila kitu, utaratibu umefuatwa Waheshimiwa Madiwani sasa wao kazi yao wanapitia ule utaratibu uliotumika wa kumpata Mkandarasi, mwanzo mpaka mwisho halafu wanatoa baraka za Mwenyekiti wao kusaini na Mkurugenzi kusaini kuliko ilivyokuwa sasa Wenyevitwanatumika kusaini wakati kikao cha kujadili na kumuelekeza Mwenyekiti kusaini ni Kamati ya Fedha na Uchumi ya Halmashauri. Lakini Wenyevitwi wetu walivyokuwa wakisaini na hana uwezo wa kufanya chochote kile, kwa sababu hata sheria hajiamsema kwamba je, yeye akikataa kusaini inakuwaje? Kwa hiyo, hilo tulilliona ni la msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninachotaka kusisitiza katika Muswada huu ambaa tunao hapa hili suala *schedule of amendment* limechelewa sana. Hata wakati nanyanyuka hapa kuchangia sikuweza kuona ninaanzia wapi sasa kusoma *schedule of amendment* ili nilijue hili suala limewekwaje. Lakini kwa sababu umetoa muda wa kutosha basi tutajifunza tuone hili suala limeingizwa vipi kwenye sheria ili kuwawezesha Waheshimiwa Madiwani kuwa na ufahamu wa kutosha katika utoaji wa *tender* katika Halmashauri na kuhakikisha kwamba wanasmamia rasilimali hizo za umma kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama walivyozungumza wenzangu tuna tatizo kubwa sana la usimamizi, tunatunga sheria hizi, *well and good*, sheria hii ni nzuri na Waheshimiwa Wabunge wameendelea kuiboresha, Kamati imeiboresha kikamilifu, lakini tatizo kubwa lipo kwenye usimamizi wa sheria yenye kwa sababu watumishi walio wengi wa Serikali wanabebana mno. Kesi tunazopeleka Mahakamani mara nyangi tunashindwa kwa sababu ya kushindwa kuwakilisha vielelezo na kwa sababu ya kushindwa kutoa ushahidi. Sasa kama tatizo lilitokea kwenye Idara au Wizara inawezekanaje siku ya mwisho ushahidi ukosekane. Kwa hiyo, tunalo tatizo kubwa ambalo haliwezi hata likamalizwa na kutunga hili Sheria ya Manunuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini labda tuamue kwamba katika Idara husika Mkuu wa Idara, Katibu Mkuu na wasaidizi wake kama kuna Mtendaji anaweza kumtolea siri bosí wake na baadae tuka-prove kwamba siri zilizotolewa ni za haki kwamba bosí wake amekula rushwa katika manunuvi au bosí wake amefuja fedha katika utaratibu fulani. Kwa sababu wasaidizi hawa wanakuwa na sifa ambazo zinalingana karibu na bosí wao iwepo *reward* kwamba huyu mtu anayeweza kumtaja boss wake aliyefuja fedha za umma au aliyefanya ubadhirifu basi tunam-promote yeye halafu huyu tunamtoa. Mimi nashangaa hata wale watu wa kuteua ambaa mmewa-appoint ninyi Makatibu Wakuu, Wakurugenzi mnashindwa kuwa-demote pale ambapo wanagundulika wana matatizo makubwa ya uufuaji wa fedha, kwa hiyo, tutawenza tukatafuta mfumo wa kuwazawadia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mzee Mrema wakati akiwa Waziri wa Mambo ya Ndani alikuwa na mfumo wake alikuwa anazungumza yupo Dar es Salaam watu wanatupa mikenge ya gongo, watu wanatupa bunduki wakiwa vijijini kule. Mzee Mrema anazungumza redioni alikuwa na mfumo wa kuwazawadia wale ambao wanatoa siri ambazo zinaiwezesha Serikali kuondokana na kero. Sasa na sisi lazima tuwe na utaratibu huo ndio tutawawezesha watendaji wa umma kwamba hata msaidizi huyu ambaye leo amechoka wapo watendaji Serikalini wamechoshwa kabisa na hujuma zinazofanywa na mabosi wao lakini hawajui wamwambie nani, akitoa taarifa anafukuzwa kazi. Tuwape reward accordingly wanaweza kutusaidia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza, kaka yangu hapa Mheshimiwa Mwanri anasema kwa nguvu zote akisema kwamba ana uwezo wa kushughulikia matatizo yaliyopo kwenye Halmashauri. Lakini nasema aliyokuwa anayasema Mheshimiwa Mwanri alikuwa anasema tu. Halmashauri ya Wilaya ya Meatu tayari sisi tumefanya uchunguzi pale, kulikuwa na Kamati Ndogo ilikuwa inachunguza Halmashauri ya Wilaya ya Meatu tukagundua kwamba jengo liliokuwa linaweza likajengwa kwa shilingi milioni 20 ipo nyumba ya kuhifadhiya maiti iliyo kuwa inaweza kujengwa kwa shilingi milioni 25 jengo hilo au shilingi milioni 20 limejengwa kwa shilingi milioni 61.5. Ukumbi mdogo wa kawaida bila ya samani umejengwa kwa shilingi milioni 291 na Baraza la Mawaziri limekuwa likiripotiwa katika taarifa zake inaripotiwa kwamba kufikia mwezi Desemba, 2011 fedha zilizokuwa zimetumika kama posho baada ya saa za kazi ni shilingi milioni sita, lakini uchunguzi uliofanyika fedha halisi zilizotumika kwa shughuli hiyo ni shilingi 44.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkuu wa Wilaya anajua, Mkuu wa Mkoa anajua, Waziri wa TAMISEMI anajua na hata wasaidizi wake nina imani wanajua na Waziri Mkuu anajua, lakini ni toka mwezi Aprili taarifa hizi tumewasilisha mwezi Aprili na kisha mwezi wa Agosti zote tumeziwasilisha lakini hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa.

Kwa hiyo, unaweza ukaona jinsi ambavyo inakuwaje sasa na kama tunawezaje sasa kuwasimamia katika mazingira ya namna hiyo. Makosa yapo wazi, chunguzeni basi kama Baraza la Madiwani lilirosea mtaona mkichunguza, lakini majibu hakuna wala taarifa hakuna. Adhabu za Kifungu cha 104 unapendekeza mtu aliyeba mabilioni ya fedha unasema katika sheria hii shilingi milioni 10 aliye, mtu ameiba bilioni nzima wewe unam-charge shilingi milioni 10 atatoa shilingi milioni 10 atampa zawadi na Hakimu shilingi milioni 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, adhabu tunazopendekeza hatujawa *serious* katika suala la rushwa nchini, wala hatujawa *serious* kutunga sheria ambayo kweli inaweza ikawashughulikia wala rushwa. Bunge hili liliwahi kutunga sheria ngumu kama ya kuteketeza mali, mtu analeta mali hapa nchini zinateteweza kwa kisingizio kwamba ni bandia na kadhalika na Bunge hili liliwahi kutunga sheria ya kupiga risasi mwananchi akiingia kwenye hifadhi ya wanyama akijaribu kukimbia hata kama hana silaha likapitisha. Leo mwizi anayeiba fedha za nchi anafungwa miaka mitano na kwa sababu inapendekezwa hivyo na tunesema sana kwenye Kamati kwamba iwekwe adhabu kubwa, haikuweza kuwekwa kwa sababu wanaopendekeza ndio hao wanaotegemea kwenda kutoa rushwa ikiwezekana baadee. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, haiwezekani mimi napendekeza hapa iwe watu wanaobainika wamekula rushwa, watu wanaobainika wametuibia fedha kuititia manunuzi kitu cha kwanza kabisa anafilishiwa, tunamfilishi mali zake zote halafu atumikie kifungo cha miaka 30. Tukifanya hivyo yapo makosa madogo muuza kuku akiiba akikamatwa anaenda kwa Hakimu anahukumiwa miaka mitano, leo huyu anahukumiwa miaka saba, leo huyu ameiba mali za umma anafungwa kwa kipindi kifupi cha miaka mitano halafu na faini ya shilingi milioni 10 na wakati mwagine anaweza akakutana na msamaha wa Mheshimiwa Rais akatumikia kifungo cha miaka miwili na akatoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba sana kwamba Bunge hili tuonyeshe nidhamu ya hali ya juu katika kuipitisha sheria hii. Tuipitishe sheria ambayo kwa kweli na wale tunaowatungia ambao wanatarajia kwenda kuiba mali ya umma itakuwa ni fundisho kwao.

Leo upo mfano wa watu ambao tuliwatuhumu kwa mabilioni ya fedha wanadunda tu Watanzania wamepata nini? Mtu akihukumiwa miaka miwili jela, Watanzania wameibiwa shilingi bilioni 100 wao wananaufaika nini, ye ye amefungwa miaka miwili, wewe unanufaika nini. Tumfilisi mali zake, tufilisi hata kwenye Makampuni tukauze *share* zake mpaka tuhakikishe kwamba fedha ya Watanzania imekuwa *compensated* na akimaliza miaka 30 hiyo jela basi atakaporudi tutaendelea kumtoza kile atakachofanya katika uchumi wake mpaka atakapokufa tunaendelea kumtoza. Wenzetu wa China ukikamatwa kwa rushwa unapigwa risasi unakufa na hiyo risasi unainunua wewe. Serikali ya China *have no money*, unainunua wewe wanakutwanga risasi.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa muda wako umekwisha. Sasa nitamwita Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza baadae atafuatiwa na Mheshimiwa Lucy Mayenga.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia kidogo katika Muswada ulio mbele yetu. Kabla ya kuchangia naomba Mwenyezi Mungu anipe uwezo wa kutokuwa na jazba ili niweze kuchangia angalau nimetulia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nianze kwa kifungu cha 31(3). Katika kifungu hiki hakikuweza kuwapa mamlaka vizuri Madiwani ili waweze kusimamia manunuzi katika Halmashauri. Ukioma katika kifungu hiki kinasema Madiwani watatengenezewa Kanuni kutokana na Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 1982, naishauri Serikali katika Muswada huu Mheshimiwa Waziri utamke wazi wazi Madiwani watashiriki vipi? Sheria inasema kanuni, mimi siamini kanuni hizi inategemea huyo atakayekwenda kutengeneza kanuni hizi anatengeneza katika *moodgani* na ana maslahi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria itamke waziwazi kiwekwe kifungu ambacho kitasema Madiwani hawa watashiriki namna hii na wakati mwingine tunaposema Kamati ya Fedha kama inavyosomwa katika kifungu nimekuja kugundua kwamba hata katika Halmashauri nyingine Kamati za Fedha zinaundwa kutokana na maslahi ya Mkurugenzi akishirikiana na Meya. Katika Halmashauri nyingine Meya ana-*pick* watu wake na wakija kuangalia kwa mfano katika Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba wamewekwa Madiwani wawili kwa maslahi ya Meya na Meya anatamka waziwazi kwamba mimi ndio nina uwezo wa kuteua watu. Kwa hiyo, unawenza kukuta hata hiki ambacho mnadhamiria kufanya Mheshimiwa Waziri hakitafanyika kwa sababu unawenza kutegemea huyu Meya na Mkurugenzi wana mahusiano gani. Kwa hiyo, nasema kiwekwe kifungu cha wazi, kwa sababu kuendelea kukiacha katika sheria zile za mwaka 1982 ni kama hakuna chochote ambacho kimewekwa, nafikiri Muswada huu urekebishwe kabisa utamke Madiwani watahusika vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia wawape mamlaka. Mimi nimeona kwamba mnaelekeza kama kutagunduliwa kwamba labda kuna upotevu au kuna mienendo isiyoeleweka katika manunuzi basi watoe taarifa kule juu kwa yule mtu ambaye anayehusika *Executive Officer* katika PPRA ni kwa nini Halmashauri zipewe *mandate* wameshagundua wizi, wameshagundua ukiukwaji ni kwa nini tena wao wasichukue hatua. Mimi nafikiri ili kusudi Muswada huu uende vizuri kuna haja ya Baraza la Madiwani kupewa uwezo wa kuchukua hatua za moja kwa moja bila kusubiri kwenda kupeleka mpaka Dar es Salaam mpaka wapi huko wakati mambo yanaendelea kuharibika. Kwa hiyo, kwa maoni yangu naona kwa kweli hiki kifungu msituache Madiwani na mimi ni Diwani, Wabunge wote hapa ni Madiwani, hiki kifungu kinatuacha solemba, tutashindwa namna ya kuwawajibisha watendaji. Kwa sababu baada ya kubadili ile Bodii iliyokuwepo ilikuwa inamweka angalau hata Meya anaingia mle au Mwenyekiti wa Halmashauri anaingia sasa hivi unakuta Mameya wetu wanasantini vitu ambavyo vimepitishwa na Wakurugenzi mimi nafikiri itaendelea kuwa hivyo hivyo kwa hiyo udhibiti hautakuwepo.

Nikimaliza hapa nije kwenye kifungu cha 65 na 66 ambacho kwa kweli kimezia mjadala mkubwa. Mjadala huu tunapopinga Muswada sio kwamba tumetumwa na mtu. Tumetumwa na wananchi hatujarubuniwa hapa. Tumetumwa na wananchi ambao wameshindwa kuamini watendaji wa Serikali kwa miongo kama miwili iliyopita katika nchi yetu. Kumekuwepo na mambo mengi machafu ambayo yanatendeka katika nchi yetu hatuoni uwajibishwaji. Naomba labda niongee kidogo, simsemi lakini ni-*comment* kidogo juu ya Waziri wa Uchukuzi amejaribu hata

kukasirika hapa, lakini nafikiri nikuonee huruma unataka mambo yako yaende, lakini ninachoku-alert ni kwamba wewe umefanya kazi miaka 11 ATC. Wewe ni mdau unaelewa vizuri Shirika hili limeharibika vipi, nani ameliua mbona hamtuambii, imekuwaje ndege zinanunuliwa katika msingi huu, ndege inaruka mara moja halafu inatua hairuki tena aliyefanya hivyo amewajibishwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, helkopta za Jeshi zimenunuliwa katika misingi hii zimeanguka, zimeua na Wanajeshi wetu nani amewajibishwa? Tuje kwenye reli unaelewa vizuri, leo mnatuambia kwamba mngetaka kununua vichwa vya treni vya RITES, lakini tunakataa kupitisha Muswada. Mnataka kutuambia mmesaini mkataba nao, kwa sababu kama watu hawa wamekuja wametuharibia reli namna hii, lakini Serikali imekaa kimya sijasikia mahali popote ambapo mmewawajibisha watu na kutowawajibisha watu, sasa watu wengi hawaamini kama kweli tunaweza kupitisha Muswada huu wa kununua bidhaa chakavu. Mimi naziita chakavu kwa mfano unaponuna gari ambalo limekuwa *used* miaka 10 sheria ya TRA wanakuambia ulipe 25 percent ya gharama uliyonunulia gari kama uchakavu.

Kwa hiyo, hata TRA ambayo ni Taasisi ya Serikali inaelewa. Kwa hiyo mtu anaposimama hapa anataka kutudanganya kati ya *used* na uchakavu, mimi simwelewi. Kitu ambacho kimetumika na nauliza katika Sheria mbona hamjatwambia ni nani ambaye atakwenda kutwambia uchakavu upo kwa kiwango gani? Mtueleze kwamba atakwenda Waziri au atakwenda nani kuangalia kiwango kama kigezo na atwambie mipaka ya uchakavu wenyewe. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisema neno *used* ni kitu kimetumika. Ni kitu ambacho ni chakavu. Kwa hiyo huwezi ukatofautisha uchakavu ndiyo maana unapimwa na mpaka unalipiwa ushuru TRA wa 25 percent, kama unanua gari milioni kumi unalipia milioni mbili na nusu kwa maana ya kwamba wewe umetuletea gari chakavu. Kwa hiyo, hiyo ndiyo maana yake. Watu tunang'ang'ana kwa sababu ya uadilifu na uzalendo kwisha katika nchi yetu. Kama kungelikuwa na uwajibishwaji, tukaona mtu amefungwa, amefilisiwa, nafikiri tusingekuwa na utata katika hili. Kinachogomba hapa ni jinsi gani hii Serikali iliyopo itaweza kusimamia hivi vitu. Tumelia ufisadi watu kimya na mnauna na wananchi pia wanauna, hamwezi kutwambia kwamba nchi hii ni maskini, miaka 50? Tunayo madini, tuna kila kitu na kila kitu mnakielewa. Tungejipanga vizuri tukawa na matumizi mazuri tusingewaambia Watanzania kwamba tunapitisha Miswada ambayo inasema tununue vitu ambavyo ni *used*. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajuliza, kama watu wanaweza kununua vyote vilivyosemwa hapa, nani sasa ambaye atasimamia jambo hili likawa jinsi mnavyofikria kwamba litatekelezwa. Kwa kweli, napata mashaka na watu wote wana mashaka. Namwomba Waziri wa Uchukuzi asiwe na hasira. Hata yeye angekuwa huku *back bencher*, asingekuwa Waziri, naye angekuwa analalamika hivi kwamba kulikoni. Watu wangefurahi kama ungewaambia Watanzania kwamba tuna uwezo wa kununua ndege yetu mpya na najiuliza ni kweli yapo Mashirika kama *Precision Air*, nani aliua ATC aka-boost *Precision*? Tunajuliza. Kwa sababu *Precision Air* imeanza tunaona, wakati ATC inakufa nani aliweza ku-boost hiki kitu kikawepo. Waziri wa Uchukuzi alikuwa mdau atuamble kusudi Watanzania tuelewe ili tukupe *mandate* ya kununua vitu chakavu. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna sababu ya kugombana tu-discuss hapa kwa niaba ya watu wote na najiuliza kama unanunua ndege mpya *Precision Air* watafurahi? Inawezekana kuna mlango wa nyuma kwa watu wengine huku, maana najiuliza kama wewe unawenza kununua ndege mpya Precision watafurahia wewe kununua ndege mpya si utawanyang'anya wateja? Labda ndiyo maana mnakataa kununua ndege mpya. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kwa mawazo yangu napenda tuamue hiki kitu kwa makini. Si kwamba tunagomba kwa ajili ya Muswada, tunagomba kwa ajili ya uadilifu na mambo ambayo yamekuwa yakinendeka katika nchi yetu. Hatuaminiki tena, viongozi hawaaminiki, Serikali haiaminiki, katika haya tuseme ukweli. Ndiyo maana na sisi tunapingga, tunasema tunavyopitisha hapa tunawapa watu uwezo wa kwenda kutenda mambo ambayo sivyo ndivyo, ndiyo maana tunabisha, tunasema sisi hatutaki mambo chakavu na nasema siungi mkono hoja mpaka kile

kifungu cha 31, 65, 15, 16 na 20 viwe vimerekebishwa, ndipo nitaunga mkono vinginevyo napinga moja kwa moja. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. (*Makof*)

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii angalau nami niweze kutoa mawazo yangu. Nianze kwanza kabisa kwa kusema kwamba, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Binadamu yejote yule anapenda kuwa na vitu vizuri, binadamu yejote yule akiambiwa leo hii kwamba kuna ugali na wali asilimia kubwa watakwenda kwenye wali na wengine watakwenda kwenye ugali. Lakini cha msingi ambacho mtu anatakiwa kujuliza ni je, hata kama napenda wali uwezo ninao? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu, nimeduwa nikisikiliza huu mjadala tangu jana kwa umakini mkubwa sana na kwa kawaida yangu huwa napenda sana kwenda kunywa chai lakini leo kwa mara ya kwanza nilibaki humu ndani. Ili nisikilize na nilikuwa najaribu kupima nione hivi Waheshimiwa Wabunge wenzangu mawazo yao yana-base kwenye kitu gani? Suala ni uchakavu, suala ni ndege, treni na nini, suala ni siasa au suala ni kwamba tuone labda Serikali haijali watu, nilikuwa najaribu kujuliza maswali yote haya. Lakini naheshimu maoni waliyoyatoa watu wote. Lakini napenda sana sisi kama wanasiasa tujaribu kwa kiwango kikubwa sana kuangalia ni kwa jinsi gani, licha ya kwamba tunapenda maendeleo, tunapenda vitu vizuri kwa ajili ya watu wetu, tutumie muda wetu mwangi kuona ni vipi tunaichangia Serikali katika kupata pesa na haya mapato ili iweze kufanya yale ambayo tunayataka. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu, nagusia hoja hii ya ununuzi wa vifaa viliviyotumika. Kila mtu angependa Tanzania iwe na ndege mpya, kila mtu angependa Serikali inunue treni mpya na kila mtu angependa zinunuliwe meli mpya, lakini uwezo wetu hauruhusu. Wakati mwangi sisi wanasiasa tunatumia muda mwangi kuwahimiza hawa Watanzania na tunachangia kwa kiwango kikubwa kuwaambia wasilipe kodi. Sisi wanasiasa tunatumia muda mwangi wa wananchi kufanya vitu ambavyo si vya kuwaleta maendeleo na vitu vya kuweza kuisaidia Serikali ili hatimaye Serikali ipate pesa tuweze kufanya yale tunayoyataka. Nachanganyikiwa inapofikia wakati tunasema kwamba, inunuliwe ndege mpya, Serikali haina uwezo, pesa zitatoka wapi? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujitahidi sana tukiwa kama wanasiasa *tu-spent* muda wetu mwangi kuangalia vitu ambavyo vitamfanya mtu aondoke kwenye umaskini wake ili hatimaye na Serikali iweze kufaidika kwa kipato kile ambacho kinapatikana kwa mwananchi. Nimeshangaa sana, Waziri wangu wa Uchukuzi ameongea vizuri sana kuhusu hili suala la ununuzi wa vifaa viliviyotumika. Nisingependa kurudia lakini *KQ, Kenya Airways* mwaka 2004 ndege yao ilikuwa ni mpya, iliua watu wote Cameron. Kwa hiyo, leo hii mtu anaposema kwamba inunuliwe, haina maana hiyo ndiyo *hundred percent guarantee*. Lakini vilevile hivi tujulize kwa wale ambao ni wakazi wa Zanzibar na sisi Wabara ambao tunakwenda Zanzibar hivi zile *boat*, kuna *boat* hata moja mpya ambayo imewahi kununuliwa? Nyingi au zote maana nina uhakika zote ni *used*. Lakini hata hawa wanaofanya biashara kama hiyo au niseme kwa ufupi kwenye ndege mashirika mnayajua, wanunua vitu *used* lakini hakuna mfanyakishara ambaye hataki faida kwa hiyo, lazima atanunua kitu ambacho ana uhakika nacho lakini vilevile hakuna Mtanzania au kiongozi ambaye pengine atakuwa katika *mandate* ya kuweza kuingia kwenye hayo manunzia akanunua kitu huku akijua kabisa kwamba ananunua kitu kwa ajili ya kuwaua Watanzania wenzetu, hakuna kitu kama hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusijenge taswira kwamba hii nchi ina watendaji wabovu kupita kiasi, ina viongozi wabovu kupita kiasi, ina watu ambao hawaaminiki. Hiyo kwa kweli tunakosea sana. kwa sababu unapokaa na watu au wafanyakazi, watendaji Serikalini huko watu wengine hawalali, wanafanya kazi usiku na mchana, wanaumiza vichwa vyao, mtu anakaa anasema hivi mimi nitafanyaje niweze kuhakikisha kwamba nchi yangu inapata manufaa. Sasa mtu unaposimama unasema watendaji wote hawafai, ni wezi, hii nchi haina watu wazalendo, sisi wenyeve tunajua jinsi ambavyo tunawategemea hawa watendaji. Sisi wenyeve tunajua jinsi ambavyo tumekuwa tukikaa na hawa watendaji na wanaweza kutusaidia katika masuala mbalimbali. Ningependa sana tena bahati mbaya sana unakuta mtu anayeongea hivyo

amenizidi umri, unamwangalia unasema dah! Jamani! Kwa kweli huyu mama yangu au baba yangu hebu angejitätahidi basi kidogo awaonee hawa watu huruma. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwa na *mentality* maana hili ni Bunge, tukiona watendaji wote hawafai hatimaye watu watakata tamaa kwamba hata nikifanya nini mimi kama mimi nitaonekana ni mwizi. Lakini vilevile tujue na hawa watendaji jamani kuna viongozi. Wananchi wa Tanzania wamekipa ridhaa Chama cha Mapinduzi kiongoze Serikali, wanajua kwamba hiki ndicho chama kitakachowafikisha kule wanakotarajia kufika. Kwa hiyo, tukisema kwamba, mtendaji leo hii unaweza ukala pesa unavyotaka, ukaamua ujinga unaoutaka kuufanya, halafu viongozi wakuangalie, hakuna kitu kama hicho. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kuhusu suala zima la kipengele cha kuhusisha Baraza la Mawaziri, kwanza hilo sikubaliani nalo, kuhusisha Bunge au *PPRA*, hizi zote sio *procuring entities*. Ushauri wangu mkubwa ni kwamba tuwe na *Ad hoc Committee*, Kamati ambayo itakuwa ni Kamati maalum pale ambapo inapotokea udharura wa kufanya manunuzi inaundwa Kamati. Kama nilivyo sema wapo watu ambao wana uwezo mkubwa sana na wanajulikana wana uzalendo na ni watendaji wazuri. Waweze kuteuliwa fulani, fulani na fulani na hawa wanateuliwa pale ambapo kuna hiyo kazi tu. Inakuwa si kazi ya kudumu, ni kazi ya dharura na hii kazi baada ya ule ununuzi ukishakamilika na hiyo kazi na Kamati inakuwa imekwisha. Hii itasaidia kwanza, kuepusha wasiwasi wa watu kwamba labda mtu anaweza akazoeleka akaingiliwa na watu wakaanza kutaka kumhonga, kumrubuni na vitu kama hivyo. Kwa hiyo, inakuwa ni Kamati au Tume maalum ambayo itakuwa imeteuliwa, ikishateuliwa inafanya hiyo kazi, ikimaliza na biashara inakwisha. Ikitokea dharura nytingine hawa watu wapo, Kamati nytingine itaundwa, itafanya hiyo kazi na itakamilika. Badala ya kutumia sijui *Cabinet*, badala ya kutumia Bunge, sijui *PPRA*, tutasimamiaje? Hizi ni mamlaka kwa kweli ambazo haziendani kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu mwengine kuwe na *time framing* kwenye haya manunuzi. Tukae tujipangie na wenzangu wengi sana wamesema tukae tujipangie kwamba kama ni ndege ambayo imetumika iwe imekwenda masaa mangapi, kama ni meli ambayo imetumika iwe imekwenda masaa mangapi na kwa miaka mingapi, kama ni treni iwe imekaa kwa kipindi gani ili tuweze kuwa na vitu ambavyo kwa kweli viwe ndani ya ubora na ule wasiwasi ambao watu wanao labda unaweza kwisha. Lakini wasiwasi wa Wabunge wengi ambao nimeuona ni kwa sababu katika sekta hii ya manunuzi inatumia asilimia 15 ya pato ya Taifa yaani pesa zote ambazo zinaingia kwenye manunuzi nchi hii ni asilimia 15 ya pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile kwa kipindi cha miaka mitatu ya fedha iliyopita, Serikali peke yake ilitumia shilingi triliioni 7.6 kwa ajili ya manunuzi na hii ni bila kushirikisha Mashirika ya Umma. Lakini vile vile kwa mujibu wa Ripoti ya *CAG*, mwaka 2009/2010, jumla ya triliioni 2.4 zilipotea hazijulikani zilipo kwa matumizi mabaya. Kwa hiyo, wasiwasi huu upo lakini vilevile naishauri Serikali ijitätahidi sana kujaribu kutafuta mbinu mbalimbali ambazo zitaondoa hii mianya ya kuwafanya watu ambao wapo katika sekta hii wasiweze kuwa nazo. Nasema hivyo kwa sababu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mji mmoja wa Gujarat, India, wao waliamua kupambana na suala la rushwa, kupambana na suala zima la ucheleweshwaji wa miradi mbalimbali ya Serikali kwa kufanya jambo moja. Ameteuliwa Gavana mpya katika mji huo. Huyo Gavana alichokifanya ni kwamba watu mnaingia kwenye *tender* kama ni kampuni au watu binafsi, mkishaingia mnaanza kuchujwa, wanatoka, 20 wanaingia 15, wanaingia watano mpaka wanapatikana labda *the best three*. Wakishapatikana wale *the best three* ile Tume ya kushughulika na hiyo *tender* wanachofanya ni kwamba, yule ambaye anakuwa mshindi namba moja anapewa nusu ya kazi lakini wale wengine wawili ambao vigezo vinafanana wanapewa nusu iliyobaki. Kwa maana hiyo unaondoa ule mwanya wa rushwa. Badala ya mtu kukaa yeye akawa ana-fight mimi niwe wa kwanza inakuwa haiwezekani, lakini hata kipindi cha kazi kufanyika *let say* ni barabara, barabara inafanywa na watu watatu badala ya kufanywa na mtu mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, badala ya haya mambo ya kila siku tunakaa hapa, mradi kapewa mkandarasi mmoja, barabara haijawkwisha, pesa labda alishapewa, pengine ameshakula nusu au robo tatu. Lazima tujaribu kufikiria vitu kama hivi. Hebu twendeni tukajifunze, Serikalini huko watu wanasafiri wanafanya nini, hebu jitahidi kwenda Gujarat India kwa sababu gazeti la

*Economist* la wiki iliyopita ni moja kati ya *State* ambayo imekuwa ni mfano na watu dunia nzima; Marekani na Uingereza wanajuliza huyu Gavana amewezaji kufanikiwa kwa kiwango hiki. Sasa hivi ni *state* ambayo ni gumzo. Twendeni maeneo kama hayo tukajifunze. Watu watakanwanatulaamu kwamba hawa watu wanakula rushwa kumbe wakati mwiningine ni kutokana na mfumo mzima wa manunuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho. Napenda kuiomba Serikali na Mheshimiwa Waziri Mkuu yupo hapa kuwe na utaratibu wa tuzo. Kama alivyosema Mheshimiwa Mpina, kaka yangu, mtu akifanya vizuri apongezwe, aitwe atambulike, lakini vilevile ukifanya vibaya wala usicheleweshwe. Ukifanya vibaya uadhibiwe. Juzi Mheshimiwa Hawa Ghasia alikuwa anajibu swali hapa, nilikuwa nataka nimuulize kuhusu hilo suala badala ya haya mambo ya kusema labda tumchukue huyu mtu tumhamishe, unajua Mtanzania mwenzetu jamani, mzaledo, bado miaka miwili anastaaifu, tuachane na hayo mambo. Mtu acae ajue kwamba hapa nikichemsha Jumamosi, Jumatatu sipo. Tusikae na haya mambo ya kusema labda pengine jamani unajua ilikuwa bahati mbaya, ni kosa la fulani, tuache huruma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuwe na utaratibu wa tuzo kama mtu akifanya vizuri, kwa sababu hata wale ambao wanajitolea kwa ajili ya nchi yao wataona kwamba hata nchi imetutambua kwamba kumbe na sisi tupo na imegundua mchango wetu. Lakini hivi, mtu anafanya kazi usiku na mchana, matokeo yake mtu akija hapa anasema watendaji wote bomu, hawafai kwa sababu hajawa *recognise*. Lakini kukiwa na utaratibu wa tuzo hapa itakuwa hata mtu akisimama akisema kwamba kuna watendaji wabovu tunamwambia *ahaa bwana!!* Juzi bwana fulani amepongezwa kwa utendaji mzuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho, nataka kuzungumzia kipengele cha *successive tender*, kipengele cha kwanza. Huu utaratibu ambao anaye-*bid lowest* ndiyo anapewa, tuuache kwa sababu hii ndiyo ambayo imetusababishia miradi mingi ya Serikali kukwama na wengine wajanja, ana-*bid the lowest* baadaye anaanza kusema nimekwama hapa na hapa anaongezewa pesa. Kwa hiyo, pesa za Watanzania zinatumika bila mpangilio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofî*)

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada huu. Kwanza kabisa, naomba niipongeze Serikali pamoja na Kamati kwa marekebisho ya huu Muswada mzuri. Mimi ni mdau ambaye nimekuwa nikitumia Muswada huu, kwa hiyo nilikuwa nauelewa vizuri na upungufu wake mwingu ambao ulikuwepo. Kwa mantiki hiyo, naomba niseme kabisa kwamba, naunga mkono hoja. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema imerekebishwa kwa sababu kulikuwa na *issue* ya muda wa zabuni, kulikuwa na *issue* kama hii ya kuwaongeza Madiwani ambao wanaingia, sitaki kwenda huko kwa sababu wenzangu wengi wameshazungumza. Lakini Sheria hii inanunua tokea pini mpaka kifaru cha jeshi. Sheria hii inanunua bidhaa ambazo ni *perishable* mpaka *non-perishable*. Sasa, ndiyo maana naona kidogo inatuwia matatizo. Lakini naomba niwaambie ndugu zangu hii Sheria ilikuwepo ila ilikuwa na matatizo au upungufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niende kwenye hiki kipengele cha bidhaa ambazo zimetumika. Kwa lugha ya kitalaam ya *ki-medical*, nasema kwamba ndugu zangu wengi wanaoona kwamba Muswada huu una walakini, wanajaribu kutibu kwa kutumia *symptoms*, badala ya kwenda kwenye *root cause*. Kwa nini nasema hivyo, kwa sababu kila aliyesimama hapa anazungumzia uadilifu na uaminifu, lakini hasemi kwamba, Tanzania ina uwezo wa kununua hivi. Wote hapa tumesimama, tunataka barabara, maji na huduma mbalimbali ambazo mpaka sasa hivi Serikali bado haijaweza kumaliza kuwashudumia Watanzania. Sasa hii hela ya kununua ndege mpya, meli mpya na kadhalika, inatoka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunajua kwamba hatuwezi, lakini sasa badala ya kwenda kwenye lile tatizo na kusema kwamba tunaiomba Serikali itatue tatizo hilo. Tatizo hapa ni uadilifu, lakini tatizo siyo mali ambayo imetumika. Ulimwengu mzima hapa, wachache sana, labda Mataifa makubwa ya duniani ndiyo yanaweza kununua ndege mpya au kununua meli mpya. Hivi sisi

tumepatwa na janga juzi, Mwenyezi Mungu aendelee kutunusuru, tusubiri miaka mitano ndege itengenezwe, ndio wananchi wapate kupona? Naomba ndugu zangu, wananchi tuwaeleze waelewe vizuri kwamba tunachozungumza hapa wala siyo mali chakavu. Mali chakavu ni kitu ambacho hakitumiki. Lakini, tunazungumzia mali iliyotumika au bidhaa zilizotumika ambazo bado zinafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Nundu alivyozungumza. Amelzungumza vizuri sana na namuunga mkono sana kwamba tuipe nafasi Serikali ili iweze kuwahudumia wananchi wake. Isije ikawa tunaiambia Serikali inunue mali mpya, tukijua kwamba itashindwa ili kutoa mwanya kwa wale ambao wanaruhusiwa kununua mali *used*, waendelee na biashara wakati Serikali imechacha. Hilo tuliangalie. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye sheria hii kuhusu manunuzi hasa bidhaa zinazotengenezwa kwenye viwanda vya ndani pamoja na *service* za ndani (*contractor*). Naomba ku-*declare* hapa kwamba mimi ni mjasiriamali ambaye nina kakiwanda kadogodogo. Kufanya biashara hapa Tanzania, kuwa mjasiriamali ni moto! Ni moto! Jehanamu unaipata hapa hapa. Hakuna *order*, tenda zote, zinakwenda huko huko nje. Hata zile ambazo tunaambiwa sijui za hapa Tanzania, unakuta kuna makampuni yako huko, hapa yameweka tu *representative* na yeye anasema ni *local*. Matokeo yake viwanda na wakandarasi wa hapa wanashindwa kupata kazi kwenye Serikali, wakati ulimwengu mzima, kila nchi inatetea viwanda vyake, wafanyabiashara wake, na wakandarasi wake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Ununuzi, huu Muswada umezungumza. Lakini nataka kukubaliana na mchangaji mmoja kwamba wanasema *schedule* zitatengenezwa baadaye ili kusudi kuweka sasa kiwango gani hawa *local contractors* au *tenderers* wanaweza kupewa. Hilo ndilo linaloua viwanda vya nchini na linua *contractors* wa hapa nchini kwa sababu gani? Kitu gani utakachopata, inategemea nani yuko kwenye meza wakati huo. Unakwenda kwa huruma ya mtu aliyeko kwenye meza. Kwa nini basi sheria hii isitamke hilo. Nakumbuka nilikwenda Marekani, wakati huo wanasema katika Sheria yao ya Ununuzi, asilimia 30 ni lazima itoke katika viwanda vidogo vidogo vya nchini, hapo ndipo tutakapokuza viwanda vyetu. Hivi kesho na kesho kutwa, Mungu atupishie mbali, panatokea matatizo hapa, tunawekewa *embargo*, tunakwenda kununua wapi? Mnakuilia mbali!

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini viwanda vyetu haviendelei, tunapiga *mark time* hapo hapo, *day in day out*, tuko hapo hapo hatuendi. Sasa hii sheria ilipaswa iseme kwamba asilimia kadhaa iende kwenye viwanda vya nchini, asilimia kadhaa iende kwa *contractors* wa nchini. Lakini, tukisema tuachie huko ambako watakwenda kutengeneza... Nafahamu kulikuwa na hii iliyopita, *regulations* zake zinasema kwa mwaka mzima, *local industry* ambayo nilikuwa naifanya, katika mauzo ya bilioni zaidi ya 30, *local industries* zilikuwa zimevekewa milioni 800 tu, hata siyo bilioni moja. Zingine zote hizo, hata kitu kidogo ambacho kinaweza kutengenezwa hapa pia kiende kikatoke nje!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kufanya hivyo, hatuwezi kwenda mbele. Haya masuala sijui ya *technology* sisi tutakuwa tunayaskia tu. Gharama ya uendeshaji inakuwa kubwa, kwa hiyo, kunakuwa hakuna tija katika uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii inahitaji elimu kwa watumiaji, tena elimu kubwa kweli kweli na siyo elimu tu hivi hivi, lakini kuwe basi na *interaction* kati ya PPRA na watumiaji wa sheria hii. Kuwe na *dialogue* pia katika *regulations* kwamba ni lazima hizo *regulations* hawa *stakeholders* na wenyewe waziangalie, siyo wazitengeneze halafu zinakuwa *imposed*, zinapelekwa tu kwamba ninyi mztumie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshukuru kwamba kuna vipengele humu ndani vimerekebishwa. Kwa sababu kulikuwa na kipengele wanasema, ukitaka ku-*appeal*...

(*Hapa kengele illia*)

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Hiyo ni kengele ya kwanza?

**MWENYEKITI:** Ndiyo Mheshimiwa Endelea.

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Ukitaka ku-*appeal*, kama wewe umeonewa, una-*appeal* lakini tenda inaendelea. Sasa na-*appeal* kwa sababu gani kama tenda inaendelea? Halafu kama kuwa *compensated* labda pengine ndiyo umepata, unalipwa ilikuwa sijui *five percent*, sijui *percent* ngapi! Ni ndogo sana na kwa hiyo, ilikuwa inalinda rushwa, ilikuwa inalinda ujisadi. Lakini napongeza kwamba, hayo nimeyaona humu ndani, sasa hayapo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na suala la *Chief Executives*, hawa Watendaji Wakuu; kila kitu kinazungumzwa huko, kuna *tender board* na nini, kimemalizika. Lakini kuki tokea kitu kimebumbuluka, *Chief Executive* ndiye *answerable*. Inakuwaje mbona kule haruhusiwi kuingia? Sasa hili nilivyolielewa, nalionna hilo limerekebishwa. Kama halikurekebishwa, naomba lirekebishwe ili kusudi kuweza kulifuatilia na kulifanyia kazi pale pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba niwaombe ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, tuisaidie Serikali ili iweze kufanya kazi ya kuwatumikia wananchi. Tusijidanganye na tuisiadanganye wananchi kwamba Serikali inaweza kununua sijui ndege mpya, nini mpya, haiwezekani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Nundu, kama kweli tunaifanya kazi Serikali, kama kweli tunawafanya kazi wananchi, kama kweli tunataka kuwasaidia wananchi, tuitishe sheria hii ili kusudi tuisaidie Serikali iweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. (*Makof*)

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kutoa mchango wangu katika Muswada huu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijasahau, naomba kwanza nimshukuru Mheshimiwa Lucy Mayenga kwa kunukuu vipengele vilivyokuwa katika hotuba ya Upinzani wakati anatoa mchango wake, japokuwa hakutaka kusema hivyo. Lakini, mambo aliyoyasema kwa mfano; "asilimia 15 ya Pato la Taifa inakwenda katika Sekta ya Manunuzi ya Umma" na "takribani shilingi triloni 7.6 zilitumiwa na Serikali katika manunuzi". Hayo ni mambo ambayo hotuba ya Kambi ya Upinzani iliyasema. Vile vile shilingi triloni 2.4 katika mwaka wa fedha 2009/2010, zilitumika vibaya katika manunuzi ya umma ambayo ilikuwa ni sawa na asilimia 21 ya bajeti yote ya mwaka huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mheshimiwa Lucy angekwenda mbele zaidi, angegundua kwamba hotuba yetu ilisema *compliance level* ya manunuzi ya umma haikufuatwa kwa kiwango cha asilimia 55.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna udhaifu mkubwa sana katika sekta ya manunuzi ya umma. Nashangaa hapa tunapoambiwa kwamba Serikali haina fedha za kununua vifaa vipyta, lakini hapo hapo tunaambiwa kwamba asilimia 21 ya bajeti nzima ya mwaka inatumika vibaya katika manunuzi ya umma na hakuna mtu aliyetwambia kwamba walioituwezesha kuingia katika matumizi hayo mabaya walichukuliwa hatua gani. Ni fedha kiasi gani zingeweza kuokolewa na zikaweza kufanya kazi zingine ambazo zina manufaa. Kuna matatizo makubwa katika sekta ya manunuzi ya umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijikite sasa katika hoja yangu na nitaongelea mambo mawili hivi. Nirejee mchango wa Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Nundu. Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi alituambia kwamba, kununua vifaa vilivyotumika ni jambo la kawaida, nami nakubali. Kununua vifaa vilivyotumika ni jambo la kawaida katika nchi za wenzetu ambazo wana uadilifu katika manunuzi ya umma na wana taratibu na sheria ambazo zinafuatwa, ndiyo maana wanafanikiwa katika sekta ya ununuzi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika Muswada huu tunaoletewa, Mheshimiwa Nundu ataathirika na sheria hii itakayopitishwa kwa sababu ye ye ndiye Waziri, anieleze Muswada unaeleza wapi kwamba vifaa vilivyotumika vitakuwa na viwango gani vya ubora. Muswada huu

uko kimya, umeacha wazi bila kueleza vifaa vilivytumika vitakuwa na kiwango gani cha ubora. Kama hakuna kiwango cha ubora kilichotajwa, basi hata *scraper* zinaweza zikanunuliwa kwa sababu *scraper* nazo ni *used*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watendaji wetu ambavyo wamekuwa daima siyo waadilifu katika manunuzi ya umma, wataachaje kutununulia *scraper* kwa sababu na zenyewe ni *used* na sheria haitamki kwamba kiwango cha matumizi kiwe kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, ni mtalaam katika sekta ya usafiri wa anga. Anataka kutuhakikisha kwamba leo hii tukipitisha sheria hii tutafanikiwa, tutakaponunua ndege zilizotumika. Lakini, Mheshimiwa Nundu anasahau kwamba alikuwa wapi kutumia utalaam wake pamoja na watalaan wenzake Serikali iliponunua ndege ya Rais ambayo haikuwahi kufanya kazi kwa ufanisi? Alitumia wapi utalaam wake Serikali yetu iliponunua helikopta za Jeshi na zikaanguka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri, akiri kwamba kuna udhaifu mkubwa katika sekta ya manunuzi na kuna udhaifu mkubwa hata kwa watalaan wetu kusema ukweli pale inapostahili. Angekuwa ana nia ya dhati, angeweza kumshauri Mheshimiwa Waziri wa Fedha kabla Muswada huu haujaletwa mezani au katika Bunge lako Tukufu kwamba lazima Muswada ueleze vigezo vya ubora kabla vitu havijawa vichakavu, naweza kusema, kwa sababu *used* inaweza kuwa chakavu kama haijawekewa vigezo kama nilivyosema. Tilitakiwa tuletewe vigezo au *life span* ya hivyo vitu ambavyo vinakusudiwa kuletwa na siyo Muswada uletwe jinsi ulivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ametwambia kwamba sisi tumetumwa. Ni kweli sisi tumetumwa na wananchi na wananchi wametutuma kutohana na mambo ambayo wanaona hali halisi inayotokea katika nchi yetu. Ndege ya Rais tuliambwa ikibidi tule majani tutakula, tulikula majani, ikanunuliwa, imefanya kazi kwa ufanisi? Wananchi wanashuhudia ufanisi wa *TRL* ambako Waziri Nundu ye ye ni Waziri katika sekta hiyo, imefanyaje ufanisi duni chini ya kampuni ile ya Wahindi? Kwa hiyo, ni kweli wananchi wametutuma tuje tupinge Muswada huu kwa sababu hatujawekewa mazingira, Muswada haujaleta vigezo vya vifaa vilivytumika vitakavyonunuliwa viwe na ubora gani kabla havijaliingizia Taifa hasara kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiachana na Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, naomba sasa ninukuu pia hotuba ya Mheshimiwa Waziri mwenzangu, Mheshimiwa Mkulo. Katika hotuba yake, Mheshimiwa Mkulo anatwambia kwamba Muswada huu utawezesha Waheshimiwa Madiwani...

## TAARIFA

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa! *Section 68*. Mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ziko chini yangu. Katika Wizara ya Uchukuzi, viwanja vya ndege na ndege za Serikali viko chini ya Kamati yetu. Mzungumzaji aliyetoka hapa anataka kuliambia Taifa, anataka kuliambia Bunge lako kwamba ndege ya Rais haitumiki na ilinunuliwa kwa pesa nyingi sana. Nataka kumpa taarifa, ndege ya Serikali ya *Gulf Stream* mpaka leo inatumika na inafanya kazi. Simzuii kupinga chochote anachotaka kupinga, lakini ni vizuri tuseme ukweli ndani ya Bunge hili. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lissu!

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante...

**MWENYEKITI:** Labda tutoe tafsiri nzuri ya mambo haya ili unapokuwa unakubali au unakataa, kiwe ni kitu kilichowekwa vizuri. Ndege ya Rais ni nzima kwa maana ya taarifa zilizopo za Kamati na inafanya kazi. Sasa kama hamuioni ikitumika kwa sababu watumiaji hawajaamua kuitumia na anayeitumia ni mmoja, ni Rais tu, hilo ni jambo lingine. Lakini, ikisemekana kwamba ni mbovu, hakika nadhani haiko sawa na pengine rekodi zitakuwa zinakaa vibaya kwa sababu taarifa tulizonazo ni kwamba inaruka na ni nzima na inafanya kazi na wala haikununuliwa mbovu. Sasa sijui taarifa hiyo unaikubali au unaikataa?

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hiyo wala siikubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee!

**MWENYEKITI:** Sasa, nitakutaka uthibitishe kama ni mbovu! (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni zilizopo na tunazotumia hapa siyo za masihara masihara. Kwa jambo ambalo ningekuwa mimi na sina uhakika, aha, unakubali tu. Tulipata mfano mzuri sana wa Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum kutoka Morogoro yule, alikuja kesho yake akakiri, akasema nilikosea, nilisema kitu ambacho... Huo ndio Ubunge. Sasa Mheshimiwa Lissu, kama una uhakika kweli, tukupe muda wa kuthibitisha unachokisema. (*Makof*)

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huwa namwona Rais akisafiri na ndege za kawaida za watu wengine. Kwa hiyo, kwa uchunguzi wangu nilifikiri hana ndege inayofanya kazi vizuri. Lakini kama ana ndege na inafanya kazi, basi taarifa hiyo naikubali. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Endelea! Endelea!

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilikodi ndege aina ya *Air Bus* kwa jumla ya shilingi bilioni 2.5 na ndege hiyo tunaambiwa hajawahi kufanya kazi na iko nchini Malta na Serikali imelipa hela nydingi kiasi hicho. Sasa hapa tunapata shaka ya kuamini uadilifu wa watalaan wetu. Kama tuliweza kukodi ndege mbovu, itakuwaje tuwaamini leo watalaan wetu kwamba tukawatungia sheria wakanunua ndege zilizotumika na zikafanya kazi kwa ufanisi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Waziri wa Fedha amesema kwamba Muswada huu pamoja na mambo mengine, utaruhusu Waheshimiwa Madiwani kuptitia Kamati za Mipango na Uchumi za Halmashauri kushiriki katika mchakato wa manunuvi, lakini nimeupitia Muswada huu, siaona kipengele ambacho kinasema Waheshimiwa Madiwani watashiriki katika mchakato wa manunuvi. Kwa hiyo, naomba nalo hilo Waziri aliweke wazi ni kipengele kipi na chini ya utaratibu upi Madiwani wataweza kushiriki mchakato wa manunuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine, kuna mchangiaji mmoja aliyejita amesema kwamba Wapinzani kazi yao ni kupinga tu, ni kupiga kelele, tena akaenda mbali zaidi, mtapiga kelele lakini Muswada huu utapita tu kwa sababu ulishaamuliwa kwenye Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri hili siyo sawa, kwa sababu ikiwa Miswada inapitishwa kwenye Kamati tunafanya nini sasa hapa, tumetumia siku mbili kujadili Muswada ambaa kumbe ulishapita kwenye Kamati, hapa hata tukijadiliana vipi hamna kitakachobadilika. Nafikiri hilo halikuwa sawa sawa, Bunge lako ni lazima liheshimiwe ndiyo maana tupo hapa siku ya pili tukijadili Muswada huu, pale ambapo tutakubaliana kutakuwa na *Schedule of Amendment* na marekebisho yatafanyika kwa kadri itakavyofaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine katika kipengele cha 66 cha Muswada huu ambacho kinahusu ununuvi wa vifaa vilivytumika katika mambo ya usafiri kama treni na injini zake, meli, ndege na kadhalika. Tunaambiwa kwamba Baraza la Mawaziri na Mamlaka husika ndiyo ambayo watatoa kibali au wata-*approve* manunuvi hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu kama tunavyojua uliletwa katika Kamati ya Fedha na Uchumi mara mbili na kwa sababu ulikuwa na upungufu mwingu, Kamati illiazimika kuurudisha Serikalini. Lakini Muswada huu pamoja na upungufu wake tayari ulikuwa umepitishwa na Baraza la Mawaziri, leo hii tutakubali vipi kulipa Baraza la Mawaziri dhamana ya kufanya manunuvi makubwa ya vifaa vilivytumika iwapo hawakugundua upungufu uliokuwepo katika Muswada huu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naomba nisitumie muda mwingu kwa sababu mengi yameshasemwa, naomba Serikali ijipange upya, tutakapokuwa tayari, tutakapokuwa na kanuni au taratibu na uadilifu wa kutosha, ndipo tufikirle kununua vifaa

viliviyotumika na siyo wakati huu ambapo kiwango cha kuzingatia sheria za manunuzi kinapuuza kwa asilimia 55, zaidi ya nusu ya sheria za manunuzi hazifuatwi. Jambo hili litatupeleka pabaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Christina Lissu kwa mchango mzuri. Sasa nitamwita Mheshimiwa Martha Mlata na Mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Jenista Mhagama.

**MHE. MARTHA J. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Nami namshukuru Mwenyenzi Mungu kwa ajili ya siku hii ya leo na baraka zake nyingi ambazo ananikirimia kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuunga mkono hoja Muswada huu uweze kupita ili utele tija kwenye nchi yetu. Naunga mkono kwa sababu kwanza katika Mkoa wangu wa Singida kuna reli ambayo inafika pale Mjini Singida, wananchi wa Mkoa wa Singida walikuwa wanafaidika sana na reli ile, lakini sasa hivi imesitishwa, kwa hiyo, naamini Muswada huu ukipita basi Singida pia itakuwa ni ya kwanza kwenye udharura ili tuweze kukuza uchumi wa wananchi wa Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi jana wakati nasikiliza michango ya Wabunge, Wabunge wengi wameongea, kila mtu ameongea kwa kadri anavyoelewa na yote ni kwa manufaa ya Taifa hili. Lakini napata wasiwasni na mashaka mengi sana kwa kuona Mtumishi wa Mungu anayeaminwa na watu wengi kwa kutumia maneno na lugha za matusi kwa kumnungu mu aliyetumia matusi kumtukana Mwafrika. Kama kweli ni mtumishi wa Mungu unaweza ukaingia ndani ya Bunge na ukatumia mfano wa lugha ya matusi, unatukana Watanzania na Waafrika wote hata wale unaowaongoza. Kwa kweli nina mashaka sana na utumishi huu. Sina uhakika hata hao anaowachunga kama kweli bado wapo au kondoo hawa walishatawanyika. Kwa sababu kazi ya mtumishi wa Mungu naamini hata Mungu amekuingiza ndani ya Bunge hili kwanza uweze kuliombea Taifa hili pale unapoona kwamba kuna upungufu, naamini hapo angeweza kutukuka katika utumishi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo nasikitika lakini namwomba akatubu kwa Mungu wake ili kazi yake iweze kuwa njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kuzungumza ni kuhusu suala la bidhaa ambazo zimetumika, siamini kama kweli Watanzania walio wengi wanapotusikiliza hapa wanatuelewa vizuri, nashukuru sana Wabunge wengine walliotangulia ambao wamefanua kuhusu vifaa au bidhaa ambazo zimetumika, kwamba Serikali yetu iruhusiwe iweze kununua. Maana unapotumia neno chakavu kwa kweli si sahihi kwa sababu hata kwenye mitumba, nguo za mitumba tunazonunua kuna mitumba ambayo kwa kweli ina *grade* tofauti tofauti. Kuna *grade* ambazo wanaita malapulapu yaani unaambiwa hizi ni za mwisho mwisho, basi watu wanakwenda kama wanaokotaokota kwa bei ya kutupa kabisa. Lakini kuna mitumba ambayo ni mizuri kabisa, mtu unanunua unapeleka *dry cleaner* na bado unaivaa nguo ile inakusitiri kwa muda mrefu. Kwa hiyo, bado naona kwamba Muswada huu tuupitishe kwa manufaa ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tunapotaka kukimbilia kununua vitu ambavyo ni vipyta, nchi yetu bado ni changa, tunahitaji mambo mengi sana, kwa ajili ya kusaidia nchi yetu. Watanzania ni wale wale, uzalishaji bado si wa kutosha sana kuweza kupata pato ambalo linaweza likanunua bidhaa zilizo mpya au kwa mfano, ndege mpya, hiyo hela Mtanzania utamkamua mpaka wapi ili aweze kutoa hela ya kununua ndege mpya? Kwa hiyo, bado naunga mkono hoja kwa ajili ya vifaa ambavyo vimeshatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua shetani mara nyingi sana anapokuona wewe unataka kufanikiwa, basi shetani atatanguliza vikwazo vingi sana mbele yako na anaweza hata akakukatisha tamaa kama una safari ya kwenda labda mahali ambapo pana mafanikio, shetani anaweza akakukatisha tamaa. Nawaomba Watanzania tushirikiane kwa pamoja, hebu tumkatae huyu shetani anayetaka kuirudisha nyuma nchi yetu. Kwa sababu tusipokwenda kwa pamoja

hakika hatutaweza kufika, maana tukianza kukwaruzana njiani, mara Watendaji hawafai, mara sijui huyu kaiba, mara sijui hiki kimekaa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi nina shaka hata Watendaji wetu Serikalini wamekuwa hawawezi kutoa maamuzi ipasavyo kutokana na woga wa maneno mengi. Yaani siasa zimekuwa nyingi kiasi kwamba watendaji wetu wanashindwa kufanya kazi ipasavyo. Mtu anaogopa kutoa maamuzi kwa sababu anajua ndani ya Bunge mle kutachemka au sijui itakuwaje kutachemka. Kwa hiyo, tunarudisha nyuma maendeleo ya nchi yetu. Hebu tuwape basi uhuru Watendaji wetu waweze kufanya kazi, kwani sheria tunatunga wenye, kama mtu atakiuka basi sheria hiyo ichukue mkondo wake, mtu aliyejiku aachukuliwe adhabu au jinsi atakavyostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ninachotaka kusema ni kwamba, Mheshimiwa Lucy Mayenga na Mheshimiwa Mpina walitangulia kusema kwamba, Tanzania bado hatuna ule mfumo wa kuwapa tuzo watu ambao wamefanya vizuri. Kuna mashirika mengine unakuta Mtanzania amekabidhiwa shirika, amefanya vizuri, shirika ile limekwenda vizuri, ni sawa kuna matatizo madogo madogo ambayo yanakuwa yakijitokeza, lakini unakuta mtu anakwenda kumshupalia mtu, anamlamu kuanzia mwanzo mpaka mwisho *as if* hajafanya kitu chochote, tunawavunja moyo. Naamini kabisa Serikali yetu kama itawezekana tuweke utaratibu wa kuweza kuwapa tuzo watu waliofanya vizuri ili waweze ku-perform vizuri hata wengine watakaokabidhiwa madaraka kwenye maeneo watakayokuwa wamepewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna suala lingine kwenye manunuzi ya vitu ambavyo vimetumika, kwa watendaji ambao si waaminifu, kwanza tunesema vifaa ambavyo vimeshatumika ni kwa udharura, si kwa sababu kila kitu tu kinunuliwe, ni pale inapotokea dharura. Juzi hapa tumepata udharura wa kutindikiwa na mitambo ya kufua umeme tukaanza kutazamana, tena nilikuwa ni mmoja wa wale nilioliza hivi kweli ile mitambo hatuwezi kuinunua? Nikajibowi kwamba hapana, sheria haituruhusu, wakati nikifika nyumbani kwangu ninakuta giza, ukienda huku giza, eti mitambo iko pale, lakini kwa sababu ya sheria huwezi kununua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie udharura unakuwa wapi, watu wengi wengine wamepoteza maisha, kwa sababu ya sheria hii tu, tumekwenda pale Muhibili umeme hamna, unakatika, lakini mitambo iko pale inatuangalia, eti kisa sheria hii iliyokuwepo ya manunuzi hairuhusu sisi kuweza kununua ile mitambo. Sasa tukipitisha yale masuala ya dharura basi tununue. Kama wazungumzaji walitangulia kusema kuwe na Kamati au Tume maalum ambayo itasimamia ununuzi wa vifaa vile, kutakuwa hakuna kuchakachuliwa, kwa sababu si kila siku na si mara kwa mara, si ajabu inaweza ikatokea kwa mwaka mara moja au baada ya miaka mitano au huwezi kujua Mungu anaweza akanusuru Taifa letu lisiingie kwenye udharura na sheria yetu ikabakia pale pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndugu zangu ninachowaomba jamani chonde chonde, kweli tumekuja hapa kwa ajili ya kuwatumikia Watanzania, tusiwapotoshe Watanzania kuwaonesha kwamba eti tunataka kuwaleta vitu vibovu! Si kweli. Ni kwamba hivi vitu ni kwa faida ya Mtanzania mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikwenda pale Dar es Salaam nikakuta saluni, watu wametandika tu kanga zao chini wamelala, unawauliza nini, wanasema umeme, mtambo upo pale umekaa umetulia hauzalishi, leo tunataka tupidisha sheria, mnawadanganya Watanzania mnawaambia ooh, mnaletewa vitu chakavu. Mtanzania anataka asaidiwe ili aweze kujikwamua katika maisha yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza tukasema labda kwa mfano MV Victoria ilizama halafu hakuna usafiri mwagine na tunataka usafiri pale, hivi tunafanyaje? Si lazima tufanye manunuzi ya udharura ambapo tunaweza tukapata kitu ambacho hata kimeshatumika lakini kwa ubora. Sasa tusiwarudishe na tusiwapotoshe Watanzania, Watanzania wajue kwamba tumeleta sheria hii kwa sababu tunataka kusaidia Taifa letu ili liweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanalamikia ndege, Baba wa watu amejieleza vizuri sana pale, ni mtaalam aliyesoma, amepoteza muda wake mwangi darasani, anaelewa ndiyo

watalaam tunaowategemea Tanzania lakini bado tunawabeza watalaam wetu wenyewe. Wapo wataalam wengi wamejaa kule wanafahamu lakini sasa hivi wanakunja mikono kwa sababu ya maneno yetu sisi wenyewe. Hebu tuwape nafasi waweze kufanya kazi vizuri. Hata sheria tunazopitisha hapa tutajuaje sasa kama sheria hii ime-perform namna gani? Tuwapeni nafasi ili na sisi tuweze kufaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli sitakuwa na mengi ya kusema, ninachosema naomba wote tuunge mkono sheria hii, iweze kupita, watendaji wetu ni wazuri, wamesoma ndio wameajiriwa. Ni kweli sisi kwetu tunasema unapochemsha kunde huwa kuna kunde ile ambayo huwa haiivi, wapo wengine wana matatizo sisi tunaita "*nsensela*". Kama wapo kama hao basi, wachambuliwe, watolewe, tuweke utaratibu ni namna gani tuwatoe, lakini tusije tukajinyima haki zetu wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chonde chonde nimtake Mchungaji akatubu, aliombee Bunge hili, aliombee na Taifa hili, aombee na sheria hii iweze kupita na Watanzania waweze kunufaika nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nasema Mungu aibariki sana Tanzania, abariki umoja wetu katika miaka hii hamsini ambayo tunakwenda kuiadhimisha, ni mambo mengi tumeyafanya, ni mambo mengi yametekelezeka na ndiyo maana mpaka sasa hivi kuna Wabunge wa Upinzani ndani ya Bunge, yote haya tunasema ni mafanikio ndani ya miaka hamsini. Basi tuanzie hapa tushikane kwa pamoja, tuache tofauti zetu ili tuweze kujenga Taifa letu. Asante sana. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mama Mchungaji. (*Kicheko*)

Sasa, nitamwita Mheshimiwa...

#### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika!

**MWENYEKITI:** Sijasikia!

**MHE. RAYA IBRAHIM HAMISI:** Mwongozo! Naomba Mwongozo!

**MWENYEKITI:** Hebu zima kwanza. Eee, halafu simama! Eee halafu, eehe mwongozo! Haya Mwongozo wa Spika!

**MHE. RAYA IBRAHIM HAMISI:** Kwa mujibu wa Kanuni ya 64(1)(g) inatwambia kwamba "Mbunge hatatumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine". Mbunge aliyetoka kuchangia mada hivi sasa ametumia lugha ambayo kwa kweli mimi binafsi, japokuwa sikuchangia, kwa Wabunge wengine imewaudhi kwa kuwaita Wabunge amba wana mawazo tofauti na ule Muswada amba umeletwa hapa, kuwaambia kwamba ni mashetani amba wana...yaani kama wanajaribu kuwafitinisha watu kwa kusema hilo. Nataka kuwaambia kwamba huu Muswada umeletwa hapa kila mtu atoe mawazo yake. Hayo ni mawazo ya Wabunge amba hawakubaliani na huu Muswada na kutaka baadhi ya vipengele vibadilishwe na ndiyo maana ukaletwa ili kila Mbunge atoe mawazo yake kwa mwono wake na ambavyo yeye anahisi iko sawa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka mwongozo wako kwa kauli ambayo Mheshimiwa Mbunge aliyetoka kuchangia kuita wenzie mashetani!

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mimi bahati mbaya ni kama ilineteza hiyo *statement*, sikuipata vizuri. Lakini, Mheshimiwa Mlata kama umesema hivyo, hebu tuwekee vizuri. Na kama ndivyo ulivyosema, basi unaweza ukaliondoa hilo neno, ukaifuta hiyo kauli ikawa imepunguza matatizo.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Kwanza, ninachotaka kusema, katika imani naamini kwamba, unapokuwa na lengo au unapokuwa na safari, mara nyingi shetani huwa anaweka vikwazo mbele yetu. Kwa hiyo na mimi nikawa nimetumia mfano huu kwamba kama Watanzania, tuangalie ni namna gani tusije tukafarakana mbele ya safari katika kutengeneza mambo yetu, basi!

**MWENYEKITI:** Sasa hapa mwamuzi wa yote ni *Hansard*. Kama ndivyo alivyosema kwa tafsiri hii ya mara ya pili, haina madhara, kama kuna kikwazo, sidhani kama ina madhara yoyote. Ila kama alisema kuna watu ni mashetani, hii ina madhara. Sasa kwa kuwa hatuna *Hansard* na hatuna nafasi hiyo kwa sasa, tuliashe tutalitolea mwongozo wake kesho.

**MBUNGE FULANI:** Jumatatu!

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia kwenye hoja iliyopo mbele yetu, nami niseme namwomba Roho Mtakatifu anisaidie ili niweze kuzungumza vizuri na ujumbe nitakaousema uweze kufika mahali pake. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napata shida sana. Kwanza napata shida kwa umaja wetu ndani ya Bunge hili, napata shida kujuu kama Watanzania wanatuelewa tunazungumza nini kuhusiana na mada iliyopo ndani ya Bunge letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema napata shida kwa sababu gani? Leo nimesikiliza baadhi ya vyombo vyoma habari, vyombo vyoma habari vinachukua kile ambacho sisi tumekuwa tukizungumza humu toka jana na toka jana ajenda ya Muswada huu imehamishwa kabisa. Ajenda ya hoja ya msingi kwenye Muswada wetu imebadilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Muswada huu ni njema. Wote tumelalamika miaka mingi sana kwamba Sheria ya Ununuzi wa Umma imekuwa ni kikwazo kwa maendeleo ya Taifa letu muda mrefu. Nasema sijui ni kwa nini tunashindwa kujenga umoja, kueleza kitu kilichopo kwenye huu Muswada kwa ukweli na hakika Mwenyezi Mungu atusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivyo? Hivi tabia zetu sisi Wabunge zitaendelea kuwa hivi mpaka lini? Nafikiri kuna umuhimu wa sisi wote kuelewa na kusema kwa ukweli kile kilichosemwa humu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na hiki cha kwanza, hatujitendei haki sisi wale tunaowawakilisha kwa kubadilisha mantiki ya Muswada huu kutoka katika umaana wa neno la ununuzi tena wa dharura wa vyombo viliviyotumika, lakini kwa makusudi mazima kwa sababu chombo kilichotumika kiko katika nafasi ya pili kutoka chombo kipywa. Tukahamisha mantiki ya Muswada huu hasa kifungu namba 65 na 66 tukahamisha hoja hiyo na kuipa jina kwamba hoja hii yaani sisi wote humu ndani leo tunatunga Muswada wa kununua vitu chakavu. Tutaendelea na tabia hii mpaka lini? Nadhani Wabunge wenzangu hapa leo tungkuja kwa pamoja, nashukuru sana waliochangia leo jioni siyo Kambi ya Upinzani, siyo Kambi ya Chama Tawala, nashukuru sana wamekubali kwamba tatizo la msingi siyo hoja yenyewe hii, tatizo la msingi je, uadilifu utakuwepo kwa huu utekelezaji wa hoja? Kumbe hapo ndipo *logic* ilipolala.

Sasa naomba kwanza niwaambie Watanzania hivi, anayewaambia mimi Mbunge wa Peramiho nawapenda wananchi wangu kufa na kupona, siwezi kusimama humu ndani ya Bunge nika-*support* ununuzi wa vitu chakavu. Ninaposimama kusema kwamba nina-*support* ununuzi wa vitu chakavu wananchi wangu wa Jimbo la Peramiho nitakuwa nimewakosea haki. Hatusemi vitu chakavu kwenye Muswada, naomba Watanzania mtuelewe, Wabunge mliotuleta humu ndani tuna akili timamu. (*Makof*)

Tunapozungumza, tena kitu cha ajabu huu Muswada wala haukatazi kununua kitu kipywa jamani wapi pamekatazwa humu ndani? Humu ndani hakuna kifungu kilichosema kuanzia sasa Serikali ya Tanzania ya Chama cha Mapinduzi ni marufuku kununua kitu kipywa hakuna humu ndani

mahali palipokataza. Hapa, Muswada huu umesema pale ambapo patatokea udharura, tena kwanza hivyo ni vifungu viwili tu kati ya vifungu vingapi vya Muswada huu. (*Makof*)

Muswada huu unasema hivi, pale ambapo patatokea dharura, kweli Waheshimiwa Wabunge wenzangu ndani ya Bunge hili dharura hatujui? Pale patakapotokea dharura na dharura ile inahusu Taifa letu.

## TAARIFA

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa kwa Kanuni ya 68(8), vile vile Mbunge yejote anaweza kusimama.

**MWENYEKITI:** Usisome, tunajua tupeleke kwenye hoja.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Msemaji anayesema sasa hivi anasema kwamba Wabunge, wanajaribu kupotosha umma na ana-quote kifungu 66, naomba nisome kifungu cha namba 66(1) anasema kwamba, Muswada ni kwa ajili ya dharura tu lakini ukisoma kile kipengele kinasema: "*Where the public interest demands that railway machinery, civilian or military ship and civilian or military aircraft that has been used be procured, the procuring entity may upon approval by the Cabinet and the Authority proceed with normal or emergency procurement. With normal, normal siyo dharura, normal ni manunuzi ya kawalda sasa naomba mzungumzaji asipotoshe umma. Tunavyozungumza pia mambo ya used au vilivytumika tunagusa na kipengele with normal.*" (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa mzungumzaji Mheshimiwa Mhagama umeipata hiyo taarifa? Je, unaipokea?

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namheshimu sana Mbunge kijana aliyeingia Bungeni kwa mara ya kwanza kwa taarifa aliyonipa. Lakini naomba nimwambie awe mvumilivu, sijamaliza hotuba yangu. Ameshanipa taarifa, atulie sijamaliza. Nimemwambia....

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, hoja hapa ni kwamba unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Kwanza taarifa hiyo siipokei. Kwa sababu gani siipokei? Kwa sababu nazungumzia kifungu 65 kinachozungumza *emergency*.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu kukurahisishia kazi kwamba iko tofauti kati ya kifungu cha 66 ya Muswada inayozungumzia *public interest* na kifungu cha 65 ya Muswada inayozungumzia *emergency procurement*.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ametupa jibu fupi, lakini lina *logic* sana. Kifungu cha 66 kinazungumzia *public interest* na hiki cha 65 kinazungumzia *emergency procurement*. Tunaweza kusema tu mchangaiji aliyekuwa anachangia alikuwa *within the context*, sana sana taarifa ya mtoa taarifa inamsaidia tu akae vizuri katika hiyo *context*. Mheshimiwa Mchangaiji endelea. (*Makof*)

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana nilikuwa nakwambia bado sijamaliza kwa sababu nilianza na 65 na wakati naanza nilisema nitazungumzia 65 na 66. Kwa hiyo, naomba niendelee kusema kwamba naelewa vifungu hivyo viwili vinamaanisha nini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea vifungu hivi vyote viwili wako wachangiaji hawavitaki na huu ndio ukweli na wala siyo siri na vimesemwa sana na wananchi wamepotoshwa sana. Vinapotoshwa kwa maana ile ile, narudia kusema hata kwenye yale manunuzi ya dharura wako wachangiaji, *hansard* inathibitisha, wanasema hayafai kufanyaika kwa kununua vitu vilivytumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwarudishe Watanzania, niwaeleze hivi leo *let say* kwamba rada imepigwa na radi, kwa hiyo hakuna kinachoonekana, hakuna suala la ulinzi litakalokuwa liko *controlled* na rada, hakuna suala la ndege kutua wala kuondoka katika nchi yetu, hakuna suala lolote lile la kuangalia ulinzi wa nchi yetu. Sisi Wabunge kazi yetu ni kutunga sheria. Tukishakataa kwenye sheria hii manunuzi hayo yasifanyike na *emergency* hiyo ikishatokea ina maana hapa ni lazima Bunge liitwe, tuje kwanza kubadilisha hiki kifungu, tumalize kukibadilisha halafu ndipo Serikali irudi ndipo ikaanze manunuzi, ulinzi wa Taifa hili utakuwa unasubiri hiyo *emergency* ifanyike kwa utaratibu huo?

Hivyo kama ndivo itakavyokuwa kwa maana hiyo ndege zote itabidi zisitue Tanzania uchumi wa Taifa hili utakuwaje? Ulinzi wa nchi yetu na hakuna kitu kikubwa sasa kinachotikisa Mataifa yote ulimwengu kama ulinzi na usalama wa Mataifa. Rada imekufa, Muswada leo hapa tumeshapitisha kwamba hatufanyi hayo manunuzi ya dharura kwa maana ya kuangalia kilichotumika, kwa maana ya kuangalia kitu kilichotumika na siyo uchakavu kama wanavyosema wale ambao wanapinga Muswada huu. Tutakuwa wageni wa nani? Narudia kuwaambia Watanzania...

Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika zangu ziongezeke. Narudia kuwaambia Watanzania nia yetu ni njema, hatuko hapa kuendesha ajenda hii kwa masuala mengine yoyote ya binafsi. Nakubaliana tena na wachangiaji waliosema kitu cha msingi cha kuangalia hapa ni namna ya kwenda kutekeleza sheria hii kwa uadilifu na uzalendo wa nchi yetu ya Tanzania. Hilo tukubaliane wote na hicho ndio kipaumbele. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo treni hapa inaanza safari na labda tumeshagharamia mabehewa yenye gharama, ndugu zetu wa Mikoa ya Mwanza, Kigoma wanapata shida na ajali ni wakati na saa yoyote. Kichwa cha treni kimekuwa, tunasema kwamba ni lazima tununue kichwa cha treni kipywa na tunajua kabisa sekta ya usafirishaji inaongoza kuendeleza uchumi wa nchi yetu na tunajua wote kichwa kipywa mpaka kiweze kuundwa hakiwezi kutumia miaka miwili wala mitatu. Sasa hiyo dharura tunafanya, miaka mitano tunangoja tununue kichwa? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kilichotumika, kikitumika siku moja kinaitwa ni *used*. Lakini cha msingi hapa kanuni itakayokuwa inalinda Muswada huu iwe ni kanuni kali, iwe ni kanuni ambayo kwa kweli itahakikisha uzalendo wa Tanzania unafuatwa kabisa. Narudia kusema kwamba, kwenye huu Muswada hakuna mahali tulipoambiwa kwamba haturuhuswi kununua kitu kipywa.

Ndugu Waheshimiwa Wabunge, wala sioni kama ina afya kwetu kuzungumzia kwamba uwezo wetu haupo, uwezo tunao, kuna maeneo tutanunua vitu vipywa uwezo tunao. Muswada unaturuhusu hauna mahali umesema kwamba kuanzia leo tuisinunue kitu kipywa. Kwa hiyo, tunao uwezo wa kununua vitu vipywa mahali pale tunapoona uwezo tunao na nawaambia ndugu zangu Watanzania uwezo wa kununua vitu vipywa tunao na uwezo huo tunaweza kuutumia sana wakati wowote na Muswada huu hautufungi na Watanzania mwelewe Muswada huu wala haufungi Serikali kununua kitu kipywa. Iwe kwenye matumizi ambayo ni *normal* iwe ni *emergency*, iwe ni nini hata kwenye *emergency* tunaweza kununua kitu kipywa kama kinapatikana. Wala Muswada hauhusiani eti kwenye *emergency* ndio tununue kitu kilichotumika, kama kuna kitu kipywa kuwe *emergency*, iwe kwenye matumizi ya kawaida, kama kiko kitu kipywa kinawenza kupatikana ndani ya siku mbili kinanunuliwa Muswada haukatazi. Kwa hiyo, naomba sisi wote tuelewe Muswada huu una ujumbe gani kwa Watanzania. Watanzania watuelewe, kama Watanzania watatuchukulia na kujumuisha tu hivi hivi kwamba tunapitisha ununuzi wa vitu chakavu si kweli. *Scrapers* hazipo kwenye huu Muswada. (*Makof*)

Narudia tena vitu chakavu haviko kwenye huu Muswada, Muswada hauzungumzi vitu chakavu. Kwa hiyo, cha msingi tukakae na nafurahi sana Mheshimiwa Mwenyekiti, umetoa Mwongozo hapa, yako maeneo kweli hayajakaa vizuri. Kamati ya Fedha irudi ikakutane kwenye kikao, ituletee hapa vitu ambavyo vimekamilika. Majedwali ya marekebisho yaje hapa yakiwa mazuri, yakiwa yamekamilika. Nakubali hilo wala sina upinzani nalo, yako mambo yameongelewa na Kamati hapa kwenye taarifa ni mazuri sana na mengine yaliongelewa na Kambi ya Upinzani. Tunaona hapa kuna vitu vingine kwa mfano, suala la Madiwani kuingizwa kwenye Muswada huu wa manunuzi na hasa kwenye Halmashauri zetu, ni mambo ya msingi. Lakini lengo letu liwe ni

kueleza namna halisi ya manunuzi tunayotegemea kuyafanya. Narudia tena Watanzania, Muswada hauzungumzii vitu chakavu tu. Huo ndio ujumbe amba nataka kuropa Watanzania ili waelewe Muswada huu, unaturuhusu kununua vitu ambavyo vimetumika, *used*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliona niyaseme haya kwa sababu nisingeyasema kwa kweli dhamira ilikuwa inanisuta, ilikuwa inaniuma sana na wananchi wangu wa Jimbo la Peramiko walini pigia simu na kuniuliza, hivi kweli Mbunge wetu na wewe unapitisha Muswada wa kununua vitu chakavu? Ikapaswa niombe nafasi haya niyaseme na nitakapopitisha Muswada huu, nikirudi Jimboni kwangu niwaambie, nilizungumza na mlinielewa Muswada ulikuwa unasema kitu gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuzungumza, lakini naomba nimalize kwa kusema kwamba, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia na naomba Waheshimiwa Wabunge, tupitishe Muswada huu na sisi wajibu wetu kama Wabunge ni kuisimamia Serikali. Kwa hiyo, katika utekelezaji wa Sheria hii tuwe wakali kweli kweli kuisimamia Serikali kusudi iendelee kufanya vizuri kama hivi tunavyoona kwamba kuna umuhimu wa kuupitisha huu Muswada. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. (*Makof*)

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako kuhusu jambo ambalo limetokea hapa, ukalitolea maelekezo lakini ningombwa Mwongozo wako kuhusu utekelezaji wa haya maelekezo.

**MWENYEKITI:** Kanuni ipi Mheshimiwa Mnyika?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Kanuni ya 68(7). Naomba Mwongozo wako kuhusiana na suala la Madiwani pamoja na Kamati ya Fedha za Uongozi na katika mwongozo wako ulielekeza kimsingi mambo mawili; moja kupata ufanuzi kutoka kwa Waziri wa Fedha ambaye alieleza kwamba kauli aliyoitamka kwenye hotuba yake ambayo iko kwenye ukurasa wa tano, kipengele (P) ilitokana na kusudio ambalo lilielezwa na Kamati husika iliyopitia Muswada. Lakini mwongozo wako vile vile ulielekeza kwenye kupata maelezo kutoka kwa Waziri wa TAMISEMI. Maelezo ambayo yalitolewa na Waziri wa TAMISEMI alishukuru Wizara ya Fedha kwa kuingiza suala la Madiwani na Kamati ya Fedha na Uongozi kwenye Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulisema tusubiri *schedule of amendment* ili tuone kama hili jambo Serikali imeliingiza au la, kama ambavyo ilielezwa na Kamati. Kwa mujibu wa *schedule of amendment* ambayo imesambazwa na Waziri wa Fedha, hili jambo halipo kabisa. Kwa hiyo, ningombwa Mwongozo wako ili mosi, Waziri wa Fedha apewe fursa ya kufuta ama kurekebisha kauli ambayo ameisema Bungeni, nanukuu: "Kuweka mfumo katika kanuni za sheria ya ununuzi wa umma wa Serikali za Mitaa utakaowezesha Madiwani kusimamia masuala ya ununuzi katika Halmashauri kupitia Kamati ya Fedha na Mipango na kuendelea. Kauli hii alitoa wakati akielezea mambo yaliyomo ndani ya Muswada, ndani ya Muswada hakuna jambo hili wala ndani ya *Schedule of Amendment* aliyoleta hakuna jambo hili. Kwa hiyo, ni vizuri akatoa kauli ya kurekebisha kauli hii.

Lakini la pili, naomba mwongozo wako sasa ili upande wa Serikali uweze kusema kuhusiana na jambo hili kama wanakusudia kuleta *schedule* nyingine ya *amendment*...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika unamaanisha kifungu kipi?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza na-refer kifungu cha kwenye sheria ukurasa wa 35, kifungu cha 31 cha sheria kipengele cha (3) kinachohusu uundaji wa Bodii za Zabuni yaani *Tender Board* kwenye *interest of time*, naomba nisikirudie kwa sababu nilishakisoma.

**MWENYEKITI:** Umeelewaka.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Ningombwa pamoja na haya yote tunayojadiliana kuhusu mitambo chakavu na nini ambayo bado tuna-*maintain position* yetu na tungependa Serikali ikaweke vifungu vya kurekebisha. Lakini ningependa *clarity* katika hili jambo ambalo linahusu kauli ambayo Waziri amelieza Bunge, hajatekelezwa.

**MWENYEKITI:** Umeeleweka. Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mnyika amerudia kile kile alichokisema wakati wa asubuhi, lakini mwongozo wangu kama uliuelewa vizuri nilisema bado fursa ya utungaji wa sheria tuko kwenye *process*. Kwa hiyo, tunaendelea na nika-*suggest* nikasema hata kama pamoja na maelezo ya nyongeza ya Mheshimiwa Waziri nilipompa fursa, nikasema na wewe Mheshimiwa Mnyika unaruhusiwa ku-*move schedule of amendment* na naamini na wewe ume-*move schedule*.

Kama mapendekezo hayo umeweka kwenye *schedule* yako Mheshimiwa Mnyika, wala huna haja ya kuomba upande wa mto hoja, yeye anaweza kusema, lakini wewe ukiweka hapa tuko kwenye *process*, ikitukwaa hiyo *amendment* uliyo-*move* wewe, itawekwa, lakini kwa kuonesha busara ya jambo hili sitaki kurudi kwenye kifungu hiki kwa sababu kwa kweli Waheshimiwa Wabunge kutunga sheria ni utaaliam mkubwa, sio kila mtu tu hapa tunasema tunatunga sheria, hapa tunaletewa na tunaongeza mawazo yetu kuboresha. *Provision* ya 31(3) inachodai tu hapa ni kanuni kwa ajili ya kutekeleza hii, lakini yenye tu hapa imesha-*accommodate* hiyo *Local Government*.

Sasa *clarity* yake inatakiwa ionekane kwa kiasi gani hiyo ni *process* ambayo tunai-*own* sis wote, tunaweza tukasema aah! Iseme vizuri zaidi kama ulipoonesha wakati ule wasiwasi wa kwamba mh! Hiyo *Local Government Finance Act* mbona haitoi ruhusa hiyo kwa Madiwani kushiriki katika manunuzi. Kwa hiyo, kunatakiwa na kule kwenye ile Sheria ifanyike *amendment*. Kwa hiyo, haya ni mambo yanayokuja tu, inaweza ikatungwa sheria moja ikafanya na zingine zibadilike. Kwa hiyo, jambo hili Mheshimiwa Mnyika wala si baya, fursa bado ipo na ndiyo maana Mheshimiwa Spika, alipoona mjadala umekolea, michango ni mizuri, akaongeza muda kwamba hoja hii tuimalize Jumatatu. (*Makof*)

Ni kwa nini amesema hivyo? Ni kwa sababu zimetoka *schedules* ambazo ni ndefu, Mheshimiwa Mnyika umeleta ya kwako ndefu, Mheshimiwa Zambi kaleta, upande wa watoa hoja wameleta *schedule*, sasa ni ndefu mno, tunadhani mkaziweke pamoja, mpate fursa *within* kesho na kesho kutwa, Jumatatu mkija angalau isije ikawa ni suala ya *scheduled* tu, kinaweza kitu kikatereza hapa tukawa hatujatunga sheria nzuri. Kwa hiyo, nadhani Mheshimiwa Mnyika unayo fursa nzuri, *schedule* yako umeleta, weka hicho ambacho wao hawajaweka, Bunge litakaa hapa litaamua. Hayo ndiyo maelezo yangu.

Sasa kwa muujibu wa taratibu nilizokuwa nazo hapa, miongozo miwili ambayo sijaitolea ufanuzi, itatolewa siku nyingine, lakini kwa leo shughuli yetu inaishia hapa. Nimeambwa niwatangazie kwamba, kesho tutakuwa na semina kuanzia saa nne asubuhi, semina hiyo ni kuhusiana na ule Muswada wa Katiba mpya wa sheria inayoweka utaratibu wa kutungwa kwa Katiba mpya. Kwa hiyo, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge tuhudhurie ili tuweze kuona tumefikia na ili tuweze kwenda kwenye mjadala huu wa sheria hiyo wiki ijayo huku wote tukiwa tunajua mambo ya msingi na muhimu yanayoweza kutusaidia kutunga sheria nzuri kwa maslahi ya Taifa letu.

Baada ya kusema haya, naahirisha Bunge hadi Jumatatu, saa tatu asubuhi.

(Saa 1.03 Usiku Bunge lilahirishwa Mpaka siku ya Jumatatu,  
Tarehe 14 Novemba, 2011 Saa Tatu Asubuhi)